ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI
ZANZIBAR

MHE. PANDU AMEIR KIFICHO - SPIKA

1.Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	MBM/Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa na Rais
2.Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Dimani.
3.Mhe. Omar Yussuf Mzee	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo/ Kuteuliwa na Rais
4.Mhe. Haji Omar Kheri	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora/Jimbo la Tumbatu
5.Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais/Kuteuliwa
6.Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa
7.Mhe. Abubakar Khamis Bakary	MBM/Waziri wa Katiba na Sheria/Jimbo la Mgogoni.
8.Mhe. Hamad Masoud Hamad	MBM/Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Ole.
9.Mhe. Ali Juma Shamuhuna	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Donge
10.Mhe. Juma Duni Haji	MBM/Waziri wa Afya/Kuteuliwa
11.Mhe. Zainab Omar Mohammed	MBM/Waziri wa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto/Kuteuliwa.
12.Mhe. Said Ali Mbarouk	MBM/Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo/Jimbo la Gando.
13.Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban	MBM/Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Kuteuliwa.
14.Mhe. Suleiman Othman Nyanga	MBM/Waziri wa Kilimo na Maliasili/Jimbo la Jang'ombe
15.Mhe. Nassor Ahmed Mazrui	MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Mtoni
16.Mhe. Abdillah Jihad Hassan	MBM/Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Magogoni
17.Mhe. Haroun Ali Suleiman	MBM/Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika/Jimbo la Makunduchi
18.Mhe. Mansoor Yussuf Himidi	MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Kiembesamaki
19. Mhe. Haji Faki Shaali	MBM/ Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Mkanyageni
20.Mhe. Machano Othman Said	MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Chumbuni.
21.Mhe. Othman Masoud Othman	Mwanasheria Mkuu
22.Mhe. Issa Haji Ussi	Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Chwaka

23.Mhe. Zahra Ali Hamad	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Nafasi za Wanawake
24.Mhe. Dr. Sira Ubwa Mamboya	Naibu Waziri wa Afya/Kuteuliwa na Rais
25.Mhe. Bihindi Hamad Khamis	Naibu Waziri wa Habari,Utamaduni,Utalii na Michezo/ Nafasi za Wanawake
26.Mhe. Haji Mwadini Makame	Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Jimbo la Nungwi
27.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi	Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Fuoni
28.Mhe. Abdalla Juma Abdalla	Jimbo la Chonga
29.Mhe. Abdalla Moh'd Ali	Jimbo la Mkoani
30.Mhe. Abdi Mosi Kombo	Jimbo la Matemwe
31.Mhe. Ali Abdalla Ali	Jimbo la Mfenesini
32.Mhe. Ali Mzee Ali	Kateuliwa na Rais
33. Mhe. Ali Salum Haji	Jimbo la Kwahani
34.Mhe. Amina Iddi Mabrouk	Nafasi za Wanawake
35. Mhe. Asaa Othman Hamad	Jimbo la Wete
36.Mhe. Asha Abdu Haji	Nafasi za Wanawake
37.Mhe. Asha Bakari Makame	Nafasi za Wanawake
38.Mhe. Ashura Sharif Ali	Nafasi za Wanawake
39.Mhe. Bikame Yussuf Hamad	Nafasi za Wanawake
40.Mhe. Farida Amour Mohammed	Nafasi za Wanawake
41.Mhe. Fatma Mbarouk Said	Jimbo la Amani
42.Mhe. Hamza Hassan Juma	Jimbo la Kwamtipura
43.Mhe. Hassan Hamad Omar	Jimbo la Kojani
44.Mhe. Hija Hassan Hija	Jimbo la Kiwani
45.Mhe. Ismail Jussa Ladhu	Jimbo la Mji Mkongwe
46.Mhe. Jaku Hashim Ayoub	Jimbo la Muyuni
47.Mhe. Kazija Khamis Kona	Nafasi za Wanawake
48.Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa	Jimbo la Kikwajuni
49.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk	Jimbo la Kitope
50.Mhe. Marina Joel Thomas	Kateuliwa na Rais

51.Mhe. Mbarouk Wadi Mussa Jimbo la Mkwajuni

52.Mhe. Mgeni Hassan Juma Nafasi za Wanawake

53.Mhe. Mlinde Mbarouk Juma Jimbo la Bumbwini

54.Mhe. Mohammed Haji Khalid Jimbo la Mtambile

55.Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali Jimbo la Uzini

56.Mhe. Mohammed Mbwana Hamad Jimbo la Chambani

57.Mhe. Mohammed Said Mohammed Jimbo la Mpendae

58.Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak Nafasi za Wanawake

59.Mhe. Mussa Ali Hassan Jimbo la Koani

60.Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa Nafasi za Wanawake

61.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi Nafasi za Wanawake

62.Mhe. Nassor Salim Ali Jimbo la Rahaleo

63.Mhe. Omar Ali Shehe Jimbo la Chake-Chake

64.Mhe. Panya Ali Abdalla Nafasi za Wanawake

65.Mhe. Rashid Seif Suleiman Jimbo la Ziwani

66.Mhe. Raya Suleiman Hamad Nafasi za Wanawake

67.Mhe. Rufai Said Rufai Jimbo la Tumbe

68.Mhe. Saleh Nassor Juma Jimbo la Wawi

69.Mhe. Salim Abdalla Hamad Jimbo la Mtambwe

70.Mhe. Salma Mohammed Ali Nafasi za Wanawake

71.Mhe. Salma Mussa Bilali Nafasi za Wanawake

72.Mhe. Salmin Awadh Salmin Jimbo la Magomeni

73.Mhe. Shadya Mohamed Suleiman Nafasi za Wanawake

74.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha Jimbo la Mwanakwerekwe

75.Mhe. Shawana Bukheti Hassan Jimbo la Dole

76.Mhe. Subeit Khamis Faki Jimbo la Micheweni

77.Mhe. Suleiman Hemed Khamis Jimbo la Konde

78.Mhe. Ussi Jecha Simai Jimbo la Chaani

79.Mhe. Viwe Khamis Abdalla Nafasi za Wanawake

80.Mhe. Wanu Hafidh Ameir Nafasi za Wanawake

Ndugu Yahya Khamis Hamad Katibu wa Baraza la Wawakilishi

Kikao cha Kumi na Sita – Tarehe 6 Julai, 2012

(Kikao kilianza saa 3:00 asubuhi)

DUA

Mhe. Mwenyekiti (Mgeni Hassan Juma) alisoma Dua

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 29

Uchimbaji wa Matofali Uwandani

Mhe. Jaku Hashim Ayoub (Kny: Saleh Nassor Juma) – Aliuliza:-

Katika kupunguza umasikini na kuongeza kipato wananchi walio wengi wa Jimbo la Wawi hasa katika vijiji vya Uwandani, Vitongoji, Kibokoni na Umangani, na wale wanaoishi katika Jimbo la Ole katika vijiji vya Ole Mahogoni, Kianga na Makumbi wameamua kujiajiri wenyewe kwa kuchimba matofali katika Kware iliyopo Uwandani. Kwa kuwa serikali imeshatoa masharti kwa wananchi hawa, na wamekubaliana nayo na wanayatekelea kila baada ya kipindi.

Je, ni sababu gani za msingi zilizopelekea serikali kuwadhalilisha wananchi hawa kwa kuwavunjia matofali yao kwa *Bulldozer*?

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais – Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, kwa idhini yako kabla ya kujibu swali la Mhe. Mwakilishi naomba nitoe maelezo yafuatayo:-

Watendaji wa Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais nikiwemo na mimi mwenyewe, na kwa kushirikiana na watendaji wa Wizara ya Kilimo na Maliasili, tumekuwa tukifika katika eneo la Kware ya Uwandani, ili kujionea wenyewe na kutoa maelekezo yanayohitajika katika zoezi zima la utekelezaji wa makubaliano na masharti yaliyofikiwa kati ya serikali na wananchi wanaojishughulisha na uchimbaji wa matofali katika eneo hilo.

Halikadhalika naomba nieleze kuwa katika kufanikisha mawasiliano na serikali, wananchi hao wa Uwandani wameanzisha Kamati yao yenye Wajumbe 10, ambayo kila mara mimi binafsi nikifika eneo hilo hunitembeza katika eneo lote, ili kujua mafanikio yaliyofikiwa na changamoto wanazokabiliana nazo.

Aidha wananchi hao hunipa salamu za Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Ali Mohammed Shein, wasaidizi wake pamoja na serikali kwa jumla kwa juhudi wanazoendelea kuzichukua katika usimamizi wa eneo la Kware ya Uwandani.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo, sasa naomba kujibu swali la Mhe. Mwakilishi kama ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, kwa makusudi nilifanya ziara maalum kwenye eneo la Kware ya Uwandani siku ya tarehe 05 Julai 2011, ili pamoja na mambo mengine kujiridhisha na hali halisi ya eneo hilo. Kwa kweli serikali haijafanya udhalilishaji kwa wananchi hawa kwa kuwavunjia matofali yao kwa *bulldozer* kwa njia nyengine yoyote.

Aidha naomba nilithibitishie Baraza lako tukufu pamoja na Waheshimiwa Wajumbe kwamba, kwa ujumla serikali haina nia ya kufanya udhalilishaji wa aina yoyote kwa wananchi hao, isipokuwa ni jitihada za kuwaelekeza, ili wawe walimu wazuri katika utunzaji na uhifadhi wa mazingira, sambamba na kuendelea na juhudi zao za kujitafutia maendeleo katika maisha yao.

Nimefanya ziara mimi mwenyewe, mazungumzo na Kamati ya Kware ya Uwandani pamoja na wachimbaji wa eneo hilo na nimethibitishiwa kwamba hakuna mtu yeyote aliyevunjiwa matofali yake kwa *bulldozer*. Aidha nimefarajika

sana na juhudi zinazoendelea za kulifukia eneo hilo, ambazo zinaendelea kwa mashirikiano mazuri baina ya taasisi za serikali na wachimbaji wa eneo hilo.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, ahsante pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri ambayo yamekidhi swali la msingi.

(a) Serikali imefanya utafiti gani kufahamu athari za kiuchumi wa kipato kwa wananchi waliokuwa wakifanya kazi hiyo kabla ya kuchukua uamuzi huo?

(b) Kwa kuwa serikali inawataka wananchi kujiajiri uamuzi huo unasaidia vipi mpango wa kuondoa umaskini kwa wananchi wake (MKUZA)?

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, serikali inaelewa kwamba wananchi wamekuwa wakijishughulisha katika shughuli hiyo ya uchimbaji wa matofali kwa muda mrefu kama kianzio cha kupata riziki kwa ajili ya kuendesha maisha yao. Kwa makusudi kabisa serikali imeamua kutopiga marufuku shughuli hiyo, lakini tulichokifanya ni kuiwekea masharti na kusimamia na kuona kwamba rasilimali hiyo ya matofali inapochukuliwa, basi maeneo yale hayafanyiwi uharibifu wa mazingira na mashimo yanayoachwa yanajazwa.

Vile vile katika mkataba wetu pamoja na wananchi wa eneo lile la Kware Uwandani na Kware nyengine, tumezungumzia suala zima la kima ambacho wananchi wanahitajika wasikizidi kukipita katika kuchimba matofali hayo ambayo ni mita tatu.

Masharti mengine ni pamoja na kutaka kuyafukia maeneo ambayo wamemaliza kuchimba wakati wanaendelea na sehemu nyengine. Kwa hivyo, serikali inathamini sana juhudi za wananchi katika kujitafutia riziki.

Sambamba na hilo Mhe. Mwenyekiti, nikizungumzia kuhusu swali lake la pili. Serikali kwa kushirikiana na Wizara ya Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika, Wizara ya Kilimo na Maliasili pamoja na Wizara ya Mifugo na Uvuvi, tunashirikiana katika kuwakusanya vijana ambao wanajiajiri katika shughuli ile, ili kujiundia vikundi.

Mhe. Mwenyekiti, kwa taarifa hivi sasa tayari vikundi vimeshaundwa, kwa ajili ya kuweza kuwatafutia shughuli mbadala na kuachana na shughuli ile, ambayo pamoja na kuwapatia riziki inaharibu kwa kiwango kikubwa afya zao kutokana na vumbi liliopo pale, lakini hata kipato wanachokipata ni kidogo mno.

Mhe. Kazija Khamis Kona: Mhe. Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa fursa ya kuuliza swali moja la nyongeza kwa Mhe. Waziri. Katika majibu ya Mhe. Waziri alisema kwamba wizara yake kwa kushirikiana na Wizara ya Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika, Wizara ya Kilimo na Maliasili pamoja na Wizara ya Mifugo na Uvuvi, zinashirikiana kuwahamasisha wananchi kukaa pamoja na kuunda vikundi, ili kuwasaidia kwa ajili ya kupata maendeleo pamoja na kipato.

Mhe. Mwenyekiti, je Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais imewasaidia nini wananchi hao kwa ajili ya kupata kipato cha kuendelea na kuondokana na uharibifu wa mazingira?

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais ikiwa ni mratibu wa shughuli zote za mazingira, tulichokifanya katika eneo hilo ilivyokuwa sisi ni jukumu letu kuhakikisha kwamba maendeleo endelevu yanatokea bila ya kuharibika mazingira.

Kwa hivyo, tuliwakusanya wananchi wa eneo hili la Kware na wakaunda umoja au kikundi chao na tuliwachukua viongozi wa kikundi kile cha Kware kwa kupitia Mradi *SMOLE* na kuwapeleka nchini Kenya katika Mji wa Mombasa, ili kujifunza namna bora ya kuchukua rasilimali na kuhifadhi mazingira. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, nataka nikuthibitishie kwamba baada ya ziara hiyo, na nitawaomba sana Waheshimiwa Wajumbe wa baraza lako tukufu wanapokuwa katika kazi zao za Kamati na hata wale ambao hawamo katika Kamati inayosimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa, ambao ndio wanaohusika na mazingira.

Kwa hivyo, ni vyema sana wakatenga muda na kwenda kulitembelea eneo hili la Kware, waone maendeleo makubwa ya uhifadhi wa mazingira yaliyoweza kufanyika baada ya wananchi wa sehemu hiyo kuweza kupatiwa taaluma na usaidizi kwa kupitia taasisi nyengine ya serikali na kuweza kuhifadhi eneo hilo.

Maeneo mengine ambayo hasa yanahusika katika kuwezesha wananchi kiuchumi yako katika wizara ya mwenzangu na jana alizungumza hapa Mhe. Haroun Ali Suleiman, Wizara ya Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika. Kwa kweli tunashirikiana nayo bega kwa bega kuona kwamba wananchi wale wataunda vikundi na tayari wako katika hatua za mwisho katika kusajili vikundi vyao, ili waweze kupatiwa shughuli mbadala zitakazowapatia kipato kikubwa kuliko ile ambayo wanayoifanya hivi sasa.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Mwenyekiti, nashukuru sana kupata nafasi ya kuuliza swali la mwisho la nyongeza. Wakati Mhe. Waziri alipokuwa akijibu swali hili kwa umakini kabisa, amesema kuwa kitendo cha wananchi hawa kudhalilishwa kwa kuvunjiwa matofali yao si cha kweli, na yeye alikwenda kule tarehe 05 Julai, 2011 kwa ajili ya kuhakikisha hali halisi ilivyo.

Mhe. Mwenyekiti, swali langu liko hivi, kwa vile Mhe. Mwakilishi aliyeuliza swali hilo anatoka katika jimbo hili na ameeleza mambo kama alivyoeleza, ambapo jibu lake si kweli.

(a) Je, Mhe. Waziri alipokwenda kule na kufanya utafiti alitaka kujua habari yoyote ya nyuma kwa sababu suali hili limeulizwa nyuma kuliko wakati aliokwenda yeye?

(b) Kama mwenyewe atakapokuja na kuthibitisha kuwa suala hili ni kweli na sisi tumeshaeleza suala hili si kweli katika majibu ni nini kitakachofuatia baadaye? *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, naomba Waheshimiwa Wajumbe wafahamu kwamba ofisi zinapopelekewa maswali huwa hazielezwi ni nani aliyeuliza swali lile.

Kwa hivyo, nataka nieleze kwamba kama ningejua kuwa ni la Mwakilishi wa eneo hili la Wawi, basi ningem-*contact* moja kwa moja, ili nikapata taarifa vizuri zaidi, maana yake inawezeka kwamba yeye anazo taarifa ambazo labda ofisi imefichwa. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, pamoja na Waheshimiwa Wajumbe kwa jumla tunachokiomba katika hili kwa kweli si vibaya kuuliza maswali hapa ndani ya Baraza, lakini mara nyingi yanapotokezea masuala mazito kama haya, ambayo yanawagusa wananchi wetu moja kwa moja ofisi zetu ziko wazi, tafadhalini mufike na mutupe taarifa, ili tuweze kushirikiana kwa ajili ya kutatua matatizo hayo. *(Makofi)*

Hata hivyo, Mhe. Mwenyekiti, naomba nikubali hapa kwamba Mhe. Mwakilishi wa Jimbo hili la Wawi kama anazo taarifa za kuthibitika uharibufu huu umetokea wa mali za wananchi ambao umefanywa na serikali, basi mimi niko tayari nikutane naye na anipatie taarifa hizi, ili tuweze kufanyia kazi. Kwa kweli nia na madhumuni ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ni kulinda haki ya kila Mzanzibari na kuleta utawala bora ndani ya visiwa vyetu. *(Makofi)*

Nam. 100

Changamoto Zinazoikabili Bodi ya Usafiri wa Barabara

Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa (Kny: Shadya Moh'd Suleiman) – Aliuliza:-

Miongoni mwa changamoto zinaoikabili Bodi ya Usafiri wa Barabara ni madereva wengi kutojuwa Sheria za Usalama Barabarani. Chanzo kikubwa cha changamoto hiyo ni kukosekana kwa alama za barabarani kwa Unguja na Pemba katika barabara zetu hasa sehemu za hatari kama kwenye mipindo mikali na madaraja mimbamba. Pamoja na kukosekana kwa *stand* zinazokidhi haja, sehemu ya kuegesha vyombo (*parking*) hasa katika miji ya Chake-Chake Pemba.

Je, Mhe. Waziri bodi yako inasemaje kuhusiana na utekelezaji wa haya?

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano – Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 100 kama ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, madereva wote wanajua Sheria za Usalama Barabarani, isipokuwa madereva wengi wamekuwa na desturi ya dharau juu ya Sheria za Usalama Barabarani. Ushahidi wa hayo ni kwamba makosa mengi ya usalama barabarani yanafanywa wakati Askari wa Usalama Barabarani hawapo njiani, na hata kama wapo njiani basi madereva hupeana taarifa (*signals*), ili wasawazishe makosa yao kabla ya kuwakuta Askari wa Usalama Barabarani.

Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyojibu swali Nam. 99 jana kwamba katika Bodi iliyomaliza muda wake kati ya mambo ambayo imeweza kumshauri Mhe. Waziri ni sehemu za kuweka alama barabarani, hivi sasa suala hilo limo katika hatua za utekelezaji, isipokuwa alama zetu nyengine zinaibiwa na wananchi na watumiaji wengine wa barabara hawazifuati.

Kuhusiana na sehemu za maegesho hususan katika Mji wa Chake-Chake. Tayari Manispaa ya Mji wa Chake-Chake imeanza kuchukua hatua za kuwahamisha wafanyabiashara waliokuwa wamejenga vibanda vya biashara katika maeneo ya maegesho huku wakiendelea na utafiti wa kupata sehemu nyengine kubwa ya kujenga maegesho hayo.

Mhe. Abdalla Juma Abdalla: Mhe. Mwenyekiti, ahsante kwa ruhusa yako naomba nimuulize Mhe. Waziri swali moja la nyongeza kama ifuatavyo. Kwa kuwa ni ukweli usiofichika kwamba katika Mji wa Chake-Chake nafasi za *parking* zimekuwa finyu sana, na kupelekea madereva wengi kutumia ile barabara ya kupitishia gari ndio eneo la *parking*.

Je, haoni kwamba hivi sasa wakati umefika wa kuanza kufikiria *underground park* kwa ajili ya kupata nafasi kubwa zaidi.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti, ni kweli kwamba eneo la *parking* katika mji wa Chake-Chake limekuwa finyu na jitihada zetu sisi ni kushirikiana na wenzetu wa Manispaa kwa kuona kwamba eneo lile linaongezeka.

Miongoni mwa jitihada zetu pamoja na Manispaa ni kuona kwamba wafanyabiashara waliopo pale wanaondoshwa, ili kuweza kupata eneo litakalokidhi maeneo ya *parking*.

Mhe. Mwenyekiti, wazo alilokuja nalo Mhe. Mjumbe ni zuri tena linafikirika, lakini sidhani kama kwa muda huu tutakuwa na uwezo wa kufanya hivyo. Kwa hivyo, naamini kwamba tukiongeza eneo liliopo basi linaweza kukidhi kwa matumizi ya muda huu na fikra zake za kujenga *underground* ni jambo la kuzingatia na linafikirika, na serikali ikifika wakati basi tutakwenda kwenye *underground parking*.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, ahsante jana hapa Mhe. Naibu Waziri alisema kwamba alama za barabarani zinaibiwa. Je, ni lini alama hizo zitarudishwa, ili ajali zipate kupungua ikiwemo pamoja na matuta?

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti, suala la uwekaji wa alama za barabarani ni jambo linaloendelea. Kwa mfano, tumeweka jana, leo zimeondoshwa tutaweka kesho, kesho kutwa zitaondoshwa ni jambo linaloendelea. Kwa hivyo, kuna maeneo ambayo tunaendelea kuweka *signals*, mabango, *zebra cross*, pia na zile sehemu ambazo *poles* kwenye madaraja tutaendelea kuweka.

Mhe. Mwenyekiti, naomba nimwambie Mhe. Mjumbe kwamba suala hili ni endelevu, kwa sababu maeneo yako mengi na wala hakuna eneo tunalosita, kila eneo na tunapopata fedha basi tutaendelea kuweka alama za barabarani, ili kunusuru maisha ya watumiaji wa barabara.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa fursa ya kuuliza swali moja la nyongeza kwa Mhe. Waziri. Pamoja na changamoto alizozieleza Mhe. Naibu Waziri, lakini Bodi hii ya Usafiri wa Barabarani inakabiliwa na madereva wetu wa Zanzibar kwenda mwendo wa kasi sana, ambapo tayari wameshapakia wananchi au abiria tena bila ya kujali wale abiria waliomo kwenye gari.

Lakini wenzetu wa Bara walipoona hali hii, basi wao walijaribu kuweka vidhibiti mwendo kwa ajili ya kupunguza. Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa sisi Zanzibar nchi yetu si kubwa na wala hatuna masafa zaidi ya kwenda kama wenzetu wa Bara.

(a) Je Mhe. Waziri, wizara yako ili kudhibiti mwendo wa kasi wa madereva na kutowajali wananchi waliomo kwenye magari, wizara yako imechukua jitihada gani?

(b) Je, unawaambia nini madereva wa Zanzibar, ili kupunguza ajali zinazokithiri zaidi? *(Makofi)*

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti, madereva waliopo Zanzibar wamepata leseni zao kwa mujibu wa taratibu na sheria ziliopo.

Kwa msingi huo utaratibu wa uendeshaji wa magari kila eneo unalopita katika barabara kuna alama na ishara zinazokuashiria mwendo wa kiasi gani unatakiwa kutumia. Kwa mfano, ukikuta bango ambalo linakuelekeza kwamba unatakiwa kwenda *speed* 60, basi dereva mwenye kuheshimu Sheria za Barabarani hatakiwi kuzidi mwendo wa *speed* 60.

Mhe. Mwenyekiti, imani yangu kwamba bado pamoja na upungufu tulionao, alama za barabara zimo na sheria hizo wanazijua. Kwa hivyo, naomba nitoe wito kwamba nawasihi sana madereva wetu pamoja na wenzetu wasimamizi wa sheria hii Jeshi la Polisi kuhakikisha kwamba sheria inafuatwa, lakini na madereva wafuate na watii sheria zilizopo, kwa ajili ya kunusuru maisha ya watu ambao hawana hatia.

Vile vile niwaombe sana abiria wanaopanda kwenye magari yanayokwenda vijijini, wanapoona au wapohisi kwamba huu ni mwendo wa kasi na kinyume na taratibu basi watoe taarifa katika vituo vya polisi, ili kuona madereva hao waliofanya uvunjaji wa sheria, basi hatua za kisheria zinachukuliwa dhidi yao, kwani kunyamaza kwao itakuwa wao ni kichocheo cha kuwahamasisha madereva kuendelea kuvunja sheria.

Mhe. Mwenyekiti, naomba wavunje ukimya na wakiona kama kuna dereva ambaye anaendesha gari kinyume na taratibu, basi wakatoe ripoti katika vituo vya polisi, ili kuona hatua za kisheria zinachukuliwa dhidi yake. *(Makofi)*

Nam. 186

Utatuzi wa Migogoro ya Ardhi

Mhe. Mohammed Said Mohammed – Aliuliza:-

Mhe. Mwenyekiti, kabla ya kuuliza swali langu naomba uniruhusu nilipongeze Baraza lako tukufu kwa kutekeleza vyema Azimio la Beijing. *(Makofi)*

Migogoro ya Ardhi imekithiri sana katika maeneo mbali mbali ya Zanzibar ikiwemo Nungwi, Mangapwani, Mpendae na sehemu mbali mbali. Serikali kupitia kwa Wakuu wa Mikoa iliagiza kutatua migogoro hiyo, lakini mpaka sasa Mikoa haijatekeleza maagizo hayo.

Je, serikali inatoa tamko gani kuhusu ahadi hiyo ya kutatua migogoro ya muda mrefu?

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maakazi, Maji na Nishati – Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 186 kama hivi ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, Tamko la Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati kwa kushirikiana na Ofisi za Wakuu wa Mikoa Unguja na Pemba tumeanza kuishughulikia migogoro hiyo. Kwa

mfano, mgogoro wa Ardhi ulioko Mkoa wa Kusini maeneo ya Kizimkazi Mchangamle uliodumu kwa muda mrefu baina ya wananchi na wakulima, na Kamati ya Maendeleo ya Kizimkazi tayari tumeshaupatia ufumbuzi na kumalizika.

Aidha zoezi hilo litaendelea hatua kwa hatua katika mikoa yote ya Unguja na Pemba, ili kuhakikisha Agizo la Serikali la kutatua migogoro ya ardhi ya muda mrefu iliyo nje ya Mahakama ya Ardhi inapatiwa ufumbuzi katika kipindi kifupi kijacho.

Mhe. Mohammed Said Mohammed: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri marefu ya kisiasa yasiyokuwa na matumaini, naomba nimuulize swali dogo sana la nyongeza.

Mhe. Waziri kwa kuwa Mhe. Rais alipoingia madarakani alitoa Tamko la Migogoro ya Ardhi ishughulikiwe katika mikoa yenyewe, lakini mpaka sasa na muda mrefu Wakuu wa Mikoa pamoja na taasisi nyengine zimeshindwa kutekeleza agizo hilo. Je, utakubaliana nami sasa Serikali itoe tamko hapa Barazani, kwamba itachukua hatua hizo serikali yenyewe kuliko kuwaachia Wakuu wa Mikoa.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Maakazi, Maji na Nishati: Mhe. Mwenyekiti, ni kweli Mhe. Rais ametoa agizo kwamba migogoro yote ya ardhi ishughulikiwe huko iliko kwa sababu imesababishwa na hao walioko huko.

Kwa taarifa Waheshimiwa Wakuu wa Mikoa hawajashindwa kiasi hicho, kwa sababu huo mgogoro uliotajwa wa Kizimkazi aliyeushughulikia mpaka ukafikia hatua hiyo ni Kaimu Mkuu wa Mkoa wa Kusini Maalim Abdalla Mwinyi Khamis, baada ya kupewa agizo hilo amelifanyia kazi suala hilo na kweli amelifikisha katika hatua nzuri. Kwa hivyo, hawajashindwa kama anavyosema Mhe. Mjumbe. *(Makofi)*

Mhe. Abdalla Juma Abdalla: Mhe. Mwenyekiti, ahsante kwa ruhusa yako naomba kumuuliza Mhe. Waziri swali moja la nyongeza. Kwa kuwa migogoro ya ardhi imekuwa sugu na hata kama wazee walisema kwamba *mwiba uchomeako ndiko utokeako*. Lakini kwa sababu hawa ambao serikali imewaagiza waitatue migogoro hiyo wao ni sehemu ya hiyo migogoro.

Kwa hivyo, haoni Mhe. Waziri kwamba hivi sasa kuna haja ya kuimarisha hizi Mahakama za Ardhi ambazo ziko duni sana, Mahakimu wa kushughulikia Migogoro ya Ardhi ni wachache, haoni kama kuna umuhimu wa kuongeza Mahakimu pamoja na hizi Mahakama za Ardhi, ili migogoro hii ipate ufumbuzi kuliko kutegemea Wakuu wa Mikoa?

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Mwenyekiti, nitakaposema bajeti yangu ataona kwamba sehemu ya mishahara kwa upande wa Mahakama ya Ardhi tumeiongeza, ili kuweza kuajiri hao Mahakimu katika maeneo yote kama inavyotakiwa. *(Makofi)*

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, ahsante.

(a) Napenda kufahamu kwa niaba ya wananchi eneo la *Residence Hotel* Kizimkazi amepewa nani na muwekezaji kutoka wapi na lini watamaliziwa kilio chao wakulima wa eneo lile?

(b) Kwa kuwa mgogoro huo umekuwa wa muda mrefu sana wala hakuna kinachoendelea. Je, Mhe. Waziri atakuwa tayari kuunda Kamati Teule kwa ajili ya kwenda kutatua tatizo hilo.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Mwenyekiti, nikiri kwamba kwenye *Residence Hotel* Kizimkazi simjui, isipokuwa najua kwamba kuna ardhi pale na ardhi hiyo ndio mgogoro tulioutaja kwenye jibu letu la msingi la Mchangamle ndipo ilipo hiyo hoteli.

Mgogoro ulianza kumalizika kwa upande wa Muyuni na ikabakia kwa upande wa Kizimkazi, juzi tu nao wa Kizimkazi umeelekea ndio umemalizika na hata juzi nilipokuwa Kizimkazi jioni waliniambia kwamba makubaliano tuliyofikia ni kuwa hivi sasa tuwe tunakatiwa sehemu zile kwa ajili ya kufanyia kazi zetu.

Mhe. Mwenyekiti, nawashukuru sana watu wa Kizimkazi wamefahamu kwa ile ardhi ni mali ya serikali. Kwa hivyo, lile tangazo la tarehe 08 Machi, 1964 wamelifahamu vizuri sana, kwa sababu hiyo wamekubali kwamba ardhi ni mali ya serikali na wao sasa wanataka wagaiwe kwa masharti ya kiserikali. *(Makofi)*

Nam. 179

Wizara za Serikali Kumiliki Nyumba

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa – Aliuliza:-

Kwa kawaida Wizara za serikali humiliki nyumba ambazo wafanyakazi wake huishi.

(a) Je, Mhe. Waziri, Wizara ya Afya ina nyumba ngapi na zipo katika maeneo gani.

(b) Katika nyumba hizo ni nyumba ngapi wanaishi Madaktari, na ngapi zinakaliwa na wasio madaktari.

(c) Wizara imechukua hatua gani kwa zile nyumba ambazo madaktari waliokuwa wakiishi ama wamefariki, wamestaafu au wameacha kazi.

(d) Je, kuna Madaktari wangapi ambao wamepewa nyumba za serikali lakini wanaishi katika nyumba zao na zile za serikali wanaishi jamaa zao.

(e) Hospitali Kuu ya Mnazi Mmoja ina madaktari wangapi wanaoishi katika nyumba za serikali kwa sasa, na wangapi wanaishi katika nyumba za kupanga.

(f) Ni lini Madaktari watapatiwa nyumba za kuishi.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: – Alijibu:-

Mhe. Mwenyeki, kwa idhini yako na kwa niaba ya Waziri wa Afya kabla sijajibu swali Nam. 79 naomba maelekezo. Mhe. Mwenyekiti, swali lilipoletwa kwangu lilikuwa na vingu (a), (b), (c) na (d), swali liliopo leo kwenye karatasi lina kifungu (a) mpaka (f). Sasa nataka nielewe kwa sababu katika maswali ambayo yameulizwa, katika niliyoletewa na mengine yaliyokuwepo leo, na mengine hayakuwemo kwa hiyo hayakupata jawabu. Nisingependa swali hilo liulizwe kama ni swali la nyongeza kwa sababu sitokuwa na jawabu.

Kama tumesoma kanuni Nam 36(d) peji 27, tunaambiwa maswali yasiwe marefu kiasi hicho wala yasiwe juu ya kejeli, sasa hili swali la (a), (b), (c), (d), (e), (f), (g) mpaka (z) nitalijibu vipi. Naomba maelekezo.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mheshimiwa kutokana na kanuni yetu ni kweli kwamba inakataza kuwa tuna maswali marefu. Lakini hiyo hoja yako ya msingi ni kuwa maswali ambayo umeletewa siyo hayo ambayo yamejitokeza. Hiyo ndiyo hoja yako ya msingi nafikiri hiyo ndiyo tuiangalie zaidi. Kwa sababu majibu yake huna, kwa hiyo nakuomba Mheshimiwa ujibu maswali yale ambayo umeletewa, ili hayo mengine yakija utakayoweza kujibu yakija kama maswali ya nyongeza basi utakayoweza kujibu utayajibu na mengine utayajibu kwa maandishi.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 179 lenye vifungu (a), (b), (c) na (d) kama hivi ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, Wizara ya Afya ni moja kati ya Wizara zilizopewa nyumba za serikali kwa ajili ya madaktari wake.

(a) Wizara ina nyumba 18 Unguja kwenye maeneo yafuatayo:-

- Mombasa kwa Mchina - 6
- Michenzani - 5
- Vuga - 2
- Kikwajuni - 5

Pia Wizara ina nyumba Pemba:

WETE		
Vuga flet 1 familia	-	6
Hospitali Nyumba	-	2
CHAKE CHAKE		
Madungu	-	4
Chakechake Hospital	-	2
MKOANI		
Mkoani Majenzi	-	1
Afisi ya RCH	-	1 Mbovu
Jumla ya Nyumba zote	-	15

Nyumba zinazokaliwa na daktari bingwa ni moja tu iko Wete.

(b) Hadi hivi sasa Unguja ni nyumba 15 ndizo zinazokaliwa na madaktari, na nyumba tatu zinakaliwa na wasiokuwa madaktari. Kwa Upande wa Pemba kati ya nyumba 15 ni nyumba moja tu ndiyo inayokaliwa na daktari, nyumba zilizobaki zinakaa madaktari wasaidizi na wauguzi.

(c) Baada ya zoezi la kuhakiki mali za serikali kukamilika, na baada ya kupata taarifa kamili tutawafuatilia wakaazi wasiostahiki ambao wanakaa kwenye nyumba hizo na kuzirudisha au kuzikabidhi Wizarani na kuwapatia madaktari wasiokuwa na nyumba hadi hivi sasa.

(d) Madaktari wengi waliokuwepo kwenye nyumba hizo Unguja wanakaa wenyewe, uhakiki unaendelea kuangalia wale waliowaachia jamaa zao. Kama watabainika wasiostahiki watahamishwa na kutoa nafasi kwa madaktari wasiokuwa na nyumba.

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Mhe. Mwenyekiti, kabla sijauliza swali langu la nyongeza nilikuwa naomba muongozo wako juu ya yale maswali ambayo nilipeleka, lakini Mhe. Waziri anasema kwake hayakufika lakini mpaka kwenye karatasi ya hapa ya *Order paper* yametokeza kwamba ni maswali. Sasa sijui atanijibu kwa njia ipi na mimi ndio nimeuliza lakini ndio sijapata jawabu. Nilikuwa nataka muongozo wako katika hili kwanza. Halafu ndio nije kwenye swali la nyongeza.

Mhe. Mwenyekiti: Mimi nilishamruhusu Mhe. Naibu Waziri kujibu yale maswali ambayo amepelekewa. Kwa hiyo huo ndio ulikuwa muongozo wangu wa awali. Baadaye nikamwambia kwamba kama litakuja swali jengine lolote ambalo linahusiana na hili la nyongeza basi ajibu, na kama kuna taarifa yoyote ambayo anaweza kuileta kwako kwa maandishi baadaye basi ailete. Huo ndio muongozo wangu.

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Nakubaliana na wewe Mhe. Mwenyekiti, lakini sikupata kauli ya Mhe. Waziri kwamba amekubali kama atayajibu kwa maandishi. Nije kwenye swali langu la nyongeza. Katika majibu yake Mhe. Waziri alikuwa anasema kwamba wanafanya zoezi la kuzihakiki hizo nyumba ambazo zipo lakini hazikaliwi ama na madaktari au hazikaliwi na watu wa Wizara ya Afya.

Nilikuwa nataka kujua hilo zoezi litakamilika lini ili kuweza kuzijua nyumba hizo ni ngapi.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Mwenyekiti, napenda kumwambia Mhe. Mtando wewe ukishakutoa idhini au ukishatoa muongozo hilo limeshatosha bila ya mimi kusema, na ndio maana niliomba muongozo wako. Kwa hivyo naomba aridhike na hilo bila ya mimi kusema.

Mhe. Mwenyekiti, zoezi la kuhakiki nyumba hatufanyi sisi, wanafanya Wizara ya Fedha, kwa hivyo watakapokamilisha shughuli hiyo watatuletea na sisi tutakufahamisha kama bado unahitaji.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Naibu Waziri wa Afya kwanza ukiri kuwa hizo nyumba zipo, na kuna wengine wanakaa lakini sio madaktari, lakini wamo na madaktari wanakaa.

(a) Ni sababu zipi zilizopelekea hao wengine waliokuwa si madaktari wakakaa katika nyumba hizo.

(b) Hesabu ya madaktari wangapi wako kwenye nyumba hizo bado hujatujibu. Sasa ni swali langu ni wangapi hivi sasa madokta ambao waliokubalika wakae nyumba hizo ni wangapi.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Mwenyekiti,

(a) Sababu zilizofanya hizo nyumba za madaktari zisikaliwe au waliokuwa wamekaa wakati huo walikuwa ni madaktari na waliwaachia jamaa zao, sio madaktari waliokuwepo sasa hivi. Kwa sababu nyumba zipo miaka mingi, kwa hiyo waliowaachia na wamekaa ni jamaa zao. Ndio maana sasa hivi uhakiki unaofanyika ni kwamba kwa kuwa hao hawastahiki hata kama waliachiwa na madaktari watatolewa ili wapewe madaktari waliopo.

(b) Hili ni moja katika swali yaliyokuwemo katika maswali hayo ambalo liloletwa katika maswali mengi. Taarifa hiyo kwa hapa sina nitamtafutia nitamletea kwa maandishi.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Mwenyekiti, nashukuru kupata nafasi ya kuuliza swali moja la mwisho la nyongeza.

Mhe. Mwenyekiti, nakumbuka pia ulitokea mradi wa kujenga nyumba za kuishi madaktari 20 Unguja na 20 Pemba, ningelimuomba Mhe. Waziri anieleze nyumba zile ngapi zimeshahamiwa na ngapi mpaka sasa hivi zimejengwa lakini hakuna madaktari, na zilijengwa kwa makusudi ya kuondoa shida za wananchi. Ana msimamo gani wa baadae kwa nyumba zile ambazo zimejengwa na madaktari mpaka leo hawajaenda.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru na pia ningependa kumjibu kwamba ni kweli Mradi wa ADB ulijenga nyumba 20 Unguja na 20 Pemba; ambazo zinakaa familia mbili mbili kwa hiyo hukukosea ni nyumba 40 kwa ajili ya kukaa madaktari au wafanyakazi wa Wizara ya Afya.

Kwa sababu sio vituo vyote vina madaktari, madhumuni ni kukaa wafanyakazi hasa wale hawana nyumba karibu na pale wanapoishi. Wakati nilipotembelea Pemba nilikuta kuna baadhi ya nyumba ambazo hazijakaliwa, kwa sababu katika sehemu zile wenyewe wana nyumba katika maeneo yale.

Kwa kuwa ni *program* ilikuwa imeandaliwa, nyumba ilibidi zijengwe kwa sababu wafanyakazi wanaokaa Pemba sio lazima wawe wao, anaweza akatoka mfanyakazi Unguja akaenda Pemba na akawa hana pa kukaa au anaweza akatoka Wilaya moja akaenda Wilaya nyengine akafika pahali akakosa pa kukaa. Unguja nimetembelea vituo vyote, nyumba zote zinakaliwa, ingawa kuna baadhi ya nyumba zinakaliwa nusu na wengine wanaokaa pale hawakuhamia.

Nam. 113

Pembejeo Katika Mapinduzi ya Kilimo

Mhe. Abdi Mossi Kombo – Aliuliza:-

Naipongeza Serikali kwa kuweka Mapinduzi ya Kilimo hasa katika kilimo cha mpunga. Hata hivyo, kilimo hiki kinahitaji pembejeo kama vile matrekta.

(a) Je, ni matrekta mangapi Serikali imenunua.

(b) Wakati serikali inapoleta matrekta hugaiwa kimkoa au Kiwilaya? Kama ni Kimkoa kila Mkoa umepewa matrekta mangapi.

Mhe. Waziri wa Kilimo na Maliasili – Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 113 lenye vifungu (a) na (b) kama hivi ifuatavyo:-

(a) Mhe. Mwenyekiti, mapinduzi ya kilimo yanakwenda sambamba na ununuzi wa zana za kisasa za kulimia na pembejeo. Kwa hiyo serikali kwa msimu huu wa 2011/2012 imenunua matrekta mapya 10 ya ziada ya kufanya jumla jumla ya matrekta 38. Kwa msimu ujao wa 2012/2013 serikali inakusudia kuongeza matrekta mengine 20 ili kukabiliana na mahitaji yanayoongezeka ya huduma hiyo.

(b) Mhe. Mwenyekiti, kuhusiana na utaratibu mpya umeandaliwa kuanzia msimu huu kwa kuyagawa matrekta kwa mujibu wa mahitaji ya bonde husika na si kwa Mkoa au Wilaya. Hii ina maana pale ambapo wakulima kwa wameshakuwa tayari na wamelipa fedha kwa ajili ya mafuta ya kulimia kwa mujibu wa utaratibu wa ruzuku, ndiko yatakapopelekwa matrekta hayo. Utaratibu huu ni mzuri kwa sababu unahamasisha wakulima kujitokeza mapema na kupata huduma haraka bila ya upendeleo.

Mhe. Abdi Mossi Kombo: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, naomba kumuuliza swali moja la nyongeza Mhe. Waziri. Kwa vile Zanzibar wakulima wengi wamekuwa wamehamasika kwa kilimo hichi cha mpunga. Je, utakubaliana nami kwamba idadi ya matrekta uliyoyataja hapa, kwa vile wakulima wengi sasa hivi wanahitaji haya matrekta kwa kulima kwa wakati huoni kama matrekta haya ni kidogo na wakulima watachelewa kulima kilimo hicho.

Mhe. Waziri wa Kilimo na Maliasili: Mhe. Mwenyekiti, ukweli kwa namna tumeyanunua au tulivyoyaongeza kwa hivyo suala la kuchelewa halitokuwepo. Kwa sababu matrekta yatakuwa ni mengi na watakapokuwa tayari kwa kulima matrekta itabidi yatapelekwa kwa sababu ya kilimo. Kwa hivyo sioni kama kutakuwa na ucheleweshaji wa aina yoyote ile.

Mhe. Hassan Hamad Omar: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana na mimi kunipa nafasi ya kumuuliza Mhe. Waziri swali moja la nyongeza. Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imekusudia kufanya Mapinduzi ya Kilimo, Mhe. Waziri kumekuwa na malalamiko makubwa kwa wananchi wa Unguja na Pemba dhidi ya wachunga au wafugaji wanaoharibu vipando vya wakulima wetu kwa makusudi. Je, Mhe. Waziri Wizara yako itachukua juhudi gani ili kukomesha jambo hili ili isiwe kurejesha nyuma juhudi za wakulima wetu.

Mhe. Waziri wa Kilimo na Maliasili: Mhe. Mwenyekiti, tunapoizungumzia hapa ni kuzungumzia masuala ya Kilimo cha Kisasa na kipi kitaendelezwa, na hivyo ndivyo ambavyo Wizara ya Kilimo itakavyofanya.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Mhe. Mwenyekiti, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika bajeti iliyopita kama hii ilitangaza Mapinduzi ya Kilimo kwa nia nzuri kabisa. Lakini kwa bahati mbaya katika azma ile kwa sababu haikusimamiwa kikamilifu tumefeli katika Mapinduzi ya Kilimo, kwa mwaka huu watu walio wengi wamefeli na wakulima wengi wa mpunga wamekata tamaa kwa kipindi hichi.

Sasa kwa sababu Serikali ya Mapinduzi Zanzibar imetangaza Mapinduzi ya Kilimo na kwa kuwa ina azma nzuri kabisa.

(a) Je, namuuliza Mhe. Waziri Wizara yake imejipanga vipi kwa kipindi kijacho ili tusije tukafeli kama tulivyofeli kipindi hichi.

(b) Je, kwa kuwa Mapinduzi ya Kilimo sio kilimo cha mpunga tu bali hata zile sehemu za maweni katika azma hiyo ya Mapinduzi ya kilimo, Je, Wizara yake imejipanga vipi kuwahamasisha wananchi ambao kuwa ni maeneo ya maweni ya kilimo cha mboga mboga kuwahamasisha ili waweze kulima kilimo cha mboga mboga kuondoa matatizo haya kuagizia vitu kutoka nje.

Mhe. Waziri wa Kilimo na Maliasili: Kwanza nataka nimuhakikishie kwamba tumefeli hiyo siyo sahihi. Wizara ya kilimo kwa kushirikiana na wakulima wametekeleza shughuli hizi ipasavyo. Kitu ambacho kilichokuwa

kimekosekana ni suala la vifaa au matrekta ambayo yalikuwa kidogo. Kutokana na hali hiyo serikali imekuwa ikiongeza matrekta hayo kufikia hesabu ambayo kwa uhakika itaendeleza kilimo cha kwenye mabonde na sehemu za juu.

Kwa hivyo kusema kwamba suala la kujipanga, tumeshajipanga vizuri sana, na suala hili kilimo kitakuwa Nam. 1 kwa wakati huu.

Nam. 78

Utengenezaji wa Program ya Uvuvi

Mhe. Jaku Hashim Ayoub – Aliuliza:-

Kupitia ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2010 – 2015 Serikali imeahidi kutengeneza program kabambe ya Uvuvi kama ilivyofanyika katika kilimo.

(a) Je, uanzishwaji wa program hiyo umefikia hatua gani na lini program hiyo itaanza kufanyika.

(b) Je, serikali itakuwa tayari kutenga fedha maalum kama ni ruzuku kwa wavuvi kwa ajili ya kupata mitaji na zana bora kama ilivyofanya katika sekta ya kilimo.

Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi - Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 78 lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Wizara yangu imeandaa program ya kuendeleza uvuvi hadi kufikia mwaka 2015 na itakamilisha malengo hayo yafuatayo.

i) Kushajihisha sekta binafsi kuelekea katika uvuvi wa bahari kuu.
ii) Kutengeneza / kununua vyombo (*fiber boat*)
iii) Kujenga viwanda vya Usarifu na kujenga getty
iv) Kufanya utafiti wa kiwango cha samaki kwenye Bahari Kuu.
v) Kutoa mikopo kwa wavuvi.
vi) Kuwajengea uwezo wavuvi wadogo wadogo na wafanyakazi.
vii) Kutafuta soko la samaki na mazao ya baharini.
viii) Kufuatilia na kufanya tathmini katika utekelezaji wa malengo yaliyopangwa.

(b) Kwa mwaka wa fedha 2012/2013, Wizara inakusudia kutekeleza mambo yafuatayo kwa bajeti ya Shs 300,000,000/:-

1) Kuwafundisha vijana sitini kuvua katika bahari kuu.
2) Kufanya doria ndani na nje ya maeneo ya hifadhi.
3) Kutoa taaluma juu ya uvuvi haramu.
4) Kuvunja jengo la iliyokuwa Kampuni ya Zafico (Malindi) na kutafuta msaada kupitia JICA kwa ujenzi wa *"Fish Market Complex"*

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Nakushukuru Mhe. Waziri kwa majibu mazuri, lakini hadi sasa inakaribia miaka miwili.

(a) Je, wawekezaji wangapi walioweka nia kuekeza katika Bahari Kuu ikiwemo pamoja na Viwanda vya Minofu ya Samaki.

(b) Kwa kuwa Zanzibar imezungukwa bahari, leo mwanza kunako ziwa tu kuna viwanda zaidi ya 11. Je, unatwambia nini Mhe. Waziri.

Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi: Mpaka hivi sasa bado hatujapata wawekezaji binafsi kutoka nje, lakini juhudi zinaendelea, tumefanya mazungumzo na Serikali ya Iran na wao wameonesha nia safi ya kuja kuekeza katika masuala haya ya uvuvi. Vile vile tumezungumza na wa – Oman na wao pia wameonesha nia ya kuja kuekeza.

Namuomba Mhe. Mjumbe tujenge subira na tuone nini kitafanyika. Naomba swali la pili kidogo alirejee Mhe. Jaku.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti kwa kuwa Mwanza kuna ziwa tu, sisi Zanzibar Mwenyezi Mungu katujaalia tumezungukwa na bahari, huoni kuna sababu ya haraka kuweza kujenga angalau kiwanda japo kimoja cha kusindika minofu ya samaki.

Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, ni kweli haja ipo tena ni kubwa tu. Tumeshafanya juhudi hizo, tulikwenda Sychelles mimi na Makamo wa Pili wa Rais na tukatembelea kiwanda kimoja kikubwa tu cha kudindika samaki. Pia aliyekuwa Mhe. Waziri aliyekuwa wa Wizara hii niliyokuwa nayo, na yeye alifanya mazungumzo nao ili kuwashajihisha ili kuja kufungua kiwanda chao hapa Zanzibar.

Naungana na Mhe. Mjumbe kwamba ipo haja, na ndio maana tupo katika juhudi hiyo kujaribu kuwashajihisha hata wawekezaji wa ndani na si vibaya lakini na wa nje tumeshawashajihisha ili waje kuwekeza. Haja ipo ila tujenge subra, asakheri huenda tukafanikiwa.

Mhe. Kazija Khamis Kona: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa fursa ya kuweza kumuuliza Mhe. Waziri swali la nyongeza kama hivi ifuatavyo.

Mhe. Serikali au Wizara yako ina dhamira ya kuwaendeleza wavuvi wadogo wadogo kuelekea kuvua uvuvi wa bahari kuu. Mhe. Waziri, hivi sasa kuna malalamiko makubwa kwa wavuvi wetu kutokana na sheria iliyopo ya uvuvi. Je, Mhe. Waziri ni lini hasa wizara yako itaifanyia marekebisho Sheria hiyo ili wavuvi na wao wajihisi wako katika faraja na nchi yao.

Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi: Ni kweli Mhe. Mwenyekiti iko migogoro kadhaa katika maeneo kadhaa na ni kawaida kwa kweli jambo linapokuwa jipya ambalo halijazoeleka huwa lina mashaka. Na siku zote jambo la kheri hupatikana ndani ya shari, kweli kuna migogoro na watu wanadai kwamba sheria inawakandamiza, lakini mimi niseme tu kwa kweli sheria hii haikuletwa kwa maana ya kuwakomoa watu au wavuvi imeletwa kwa nia safi tu na imeletwa hii kutokana na faida ya vizazi vilivyopo na vizazi vijavyo. Na ushahidi upo unaonekana kwamba hali ya mazao baharini kwa kweli yamepungua kwa sababu ya idadi ya wavuvi imekuwa kubwa zaidi na maeneo ni yale yale na kila mtu kumekuwa na kinyang'anyiro. Kwa hivyo kunapokuwa na kinyang'anyiro ina maana kila mtu atatumia silaha aliyonayo ikiwa halali ikiwa si halali ilimradi ahakikishe yeye anaondoka mshindi na anapata mazao mengi kama inavyowezekana.

Sasa imepelekea bahari kupungua sana kutokana na uvuvi haramu na kutokana na idadi ya wavuvi kuongezeka ndio maana tukaleta hii sheria kwa manufaa ya vizazi vinavyokuja, si kwa sababu ya kumkomoa mtu na hii sio itadumu tunaweka kwa muda angalau ile ardhi au ile bahari iweze kuji-*re establish* hata ardhi unapoilima nayo inachoka, unaambiwa ukiona ardhi imechoka hama tafuta ardhi nyengine ili hii ardhi baada muda miaka miwili mitatu unaweza ukarejea. Kwa hivyo ndio madhumuni ya sheria hiyo lakini siku zote hakuna anayekubali kiungo chake kukatwa lakini unapoambiwa kiungwe kikatwe ni kwa manufaa au faida kwa afya yako mwenyewe. La si hivyo basi baadae tutakuja kulia kilio cha mbwa.

Kwa hivyo, kwa sababu utungaji wa sheria hii sio kwamba imetungwa tu wameshirikishwa wana vijiji, wavuvi, na ndio maana kila kijiji kuna kamati zake za wavuvi wale wale ndio wanaolinda lakini kuna wengine ambao ni kawaida watakuwa hawaridhiki lakini pamoja na hivyo tutakaa tutizame nini ambacho kinaleta usumbufu. Ni binaadam, kwa hivyo tutakaa pamoja tutizame tena nashukuru.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Kwa kuwa mara nyingi sana tunapiga kelele kuhusu uvuvi bahari kuu na serikali imekusudia pia kuendeleza uvuvi wa bahari kuu, ili kutekeleza azma hiyo serikali imetenga kiasi gani kwa bajeti hii iliyopo ili kuendeleza uvuvi wa bahari kuu. Na lini hasa tutaanza kuvua uvuvi wa bahari kuu kwa ajili ya serikali

kujitolea kuonesha mfano kwa sababu sadaka huanza nyumbani ili na wawekezaji wengine waje waigize ili wananchi wetu wapate faida ya uvuvi wa bahari kuu na serikali pia ipate faida.

Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi: Nashukuru Mhe. Mwenyekiti naomba kumjibu Mhe. Mjumbe kwa kweli ni kwamba kwa mwaka wa fedha huu 2012/13 Wizara imekusudia kufanya mambo yafuatayo kwa bajeti ya shilingi milioni mia tatu ambayo itatoka chini ya Wizara ya Uwezeshaji Kiuchumi, yaani mradi huu tutauanza 2012 yaani bajeti itayoanza kesho kutwa shilingi milioni mia tatu kwa kushirikiana na Wizara ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Waziri Mhe. Mjumbe alikuwa na masuali mawili (a) na (b) sasa umejibu moja bado moja.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Suali la pili nimemuuliza Mhe. Waziri kwa kuwa sadaka huanza nyumbani halafu na watu wengine ndio wakapewa ile sadaka lakini unaanza nyumbani kuwapa watoto wako. Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar ni lini italeta chombo cha kuvua bahari kuu ili na wawekezaji wengine waige mfano wa serikali yetu.

Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi: Kwa kweli kwa sababu kwanza lazima wavuvi wapate na tunataka kuingia katika mkataba na bwana Badat ambaye ana meli za uvuvi na tumekusudia kuanza na vikundi 30 kutoka Unguja na Pemba ili meli mbili hizi zitakuwa tabaan darasa la kuwafundisha watu namna ya uvuvi wa bahari kuu kwa sababu suala hili linataka taaluma. Si kila mtu kwamba anaelewa hilo, baada ya kufanya hilo na sisi vile vile tunatafuta misaada tumeshazungumza na Serikali ya Oman ili kutuletea bodi si chini ya 100 ili kuanzia hizo kwa watu wetu baada ya kupata mafunzo hayo. Kwa hivyo usiwe na wasiwasi tuko katika harakati kubwa.

Nam. 143
Msaada na Udhamini kwa ZFA

(Mjumbe aliyeuliza swali hili ameliondoa)

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Mwaka wa Fedha 2012/2013 - Wizara ya Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana,
Wanawake na Watoto

Mhe. Waziri wa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana na Watoto: Mhe.Mwenyekiti, naomba kutoa hoja kwamba Baraza lako Tukufu likae kama Kamati ya matumizi ili niweze kutoa maelezo ya makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto kwa mwaka wa fedha 2012/2013.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kuchukua nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema na Utukufu kwa kutujaalia kukutana hapa leo, tukiwa na afya njema katika Baraza hili kwa lengo la kujadili masuala muhimu ya Maendeleo ya nchi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru kwa dhati kabisa kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuwasilisha Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2012/2013 mbele ya Baraza lako Tukufu.

Mhe. Mwenyekiti, kwa niaba ya wafanyakazi wa Wizara ya Ustawi wa jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto ninayo furaha na heshima kubwa kuchukua nafasi hii adhimu kumpongeza Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mheshimiwa Dkt. Ali Mohammed Shein kwa anavyoiongoza nchi yetu na jinsi anavyosimamia vizuri utekelezaji wa shughuli za Serikali na Wananchi kwa lengo la kuhakikisha ufanisi na Maendeleo. Jitihada zake na utaratibu anaoutumia wa kuongoza ni mfano mzuri wa kuigwa kwa viongozi wa ngazi zote nchini. Mabadiliko makubwa ya kiutendaji yanaoneka kufuatia utaratibu wake huo; nchi yetu bado ni tulivu na yenye Amani, Umoja na Mshikamano, Hongera Dkt. Shein.

Mhe. Mwenyekiti, hivi karibuni, Mhe. Rais wa Zanzibar ametowa tamko la kufuta Ada ya Uzazi kwa kinamama watakaokwenda kujifungua katika Hospitali za Serikali na kuamua gharama hizo zibebwe na Serikali. Hili ni jambo kubwa na la faraja kwani litapunguza vifo kwa kinamama na watoto. Wizara kwa niaba ya Wanawake wote na

kinababa wa Zanzibar tunampongeza na kumshukuru Mhe. Rais Dkt. Ali Mohammed Shein kwa uamuzi wake huo na Inshaallah Mwenyenzi Mungu amuwezeshe kutimiza azma yake hiyo.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Rais wetu Dkt. Ali Mohammed Shein tokea akae madarakani ameonyesha mapenzi na imani kubwa kwa Wazee wa Zanzibar. Kutokana na maelekezo yake hivi sasa Wazee wanaoishi katika nyumba za Wazee wameongezewa posho ya kila mwezi, ukarabati wa nyumba na kujenga ukuta kwa nyumba za Wazee Sebleni ili kuwaweka katika hali ya usalama. Aidha, kuanzia mwaka wa fedha ujao Mhe. Rais ameamua Wazee wapewe milo mitatu kwa siku. Hii ni kutokana na Uongozi bora na maelekezo mazuri ya Mhe. Rais wa Zanzibar. Wizara inafarijika sana na kumshukuru kwa hatua anazozichukuwa kuimarisha ustawi na hifadhi kwa Wazee.

Mhe. Mwenyekiti, Wizara inaishukuru na kuipongeza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kufanikisha zoezi la kuwafariji na kutowa misaada kwa Wahanga wa ajali ya MV Spice Islander ambapo Wanawake na Watoto wengi walipoteza maisha yao. Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais tunaipongeza kutokana na utaratibu mzuri waliouweka kusimamia zoezi hilo. Hongera sana Mhe. Makamo wa Pili wa Rais wa Zanzibar pamoja na Wafanyakazi wako.

Mhe. Mwenyekiti, **s**iku ya Jumaapili ya tarehe 26 mwezi wa Agosti mwaka huu wa 2012 tunatarajia kufanya Sensa ya Watu na Makaazi. Zoezi hilo ni muhimu kwa maendeleo ya nchi yetu kwani takwimu zitakazopatikana zitasaidia katika kupanga mipango ya maendeleo kwa mujibu wa mahitaji ya Walengwa wetu. Hivyo, napenda kutoa wito kwa Wanawake, Vijana, Wazee na Watoto wote kujitokeza na kuhakikisha kuwa kila mtu anahesabiwa ili kuwa na takwimu sahihi zinazohitajika kwa maendeleo ya nchi.

Mhe. Mwenyekiti, napenda kuchukuwa fursa hii kuwapa pole wananchi wa Majimbo ya Bububu na Uzini kutokana na vifo vya Waheshimiwa waliokuwa Wawakilishi wa Majimbo yao katika Baraza lako Tukufu. Hivyo, nawaombea marehemu hao walazwe mahali pema Peponi amin. Aidha, Mhe. Mwenyekiti, napenda kuwapongeza Wananchi wa jimbo la Uzini kwa kumchagua Mhe. Mohammed Raza kuwa Mwakilishi wao.

Mhe. Mwenyekiti, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii ya Baraza lako Tukufu chini ya Uenyekiti wa Mheshimiwa Amina Iddi Mabrouk, Mwakilishi viti Maalum vya Wanawake kwa jinsi tulivyoshirikiana nao kwa karibu katika kipindi chote cha utekelezaji wa shughuli za Wizara ambapo miongozo, ushauri na maelekezo yao tuliyokuwa tukiyapata kupitia Kamati yamepelekea kupata mafanikio makubwa ya kiutendaji. Aidha, nachukuwa nafasi hii pia, kuwashukuru Waheshimiwa Wajumbe wote wa Baraza lako Tukufu kwa miongozo na michango yao iliyotuwezesha kutekeleza majukumu ya Wizara kwa ufanisi.

Mhe. Mwenyekiti, hotuba hii ya Makadirio na Mapato ya matumizi imezingatia Mipango Mikuu ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ambayo ni Dira ya Maendeleo ya 2020, Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umasikini Zanzibar (MKUZA II), Malengo ya Milenia, Ilani ya Uchaguzi 2010-2015 ya Chama Cha Mapinduzi (CCM), Mwelekeo wa Sera za CCM 2010-2020, Mwelekeo wa Hali ya Uchumi na Mpango wa Maendeleo kwa mwaka 2011/2012, Sera za Kisekta pamoja na Mpango Mkakati wa Wizara.

MALENGO MAKUU YA WIZARA.

Mhe. Mwenyekiti, Wizara kwa kipindi cha mwaka 2011/2012 ilijipangia kutekeleza Malengo Makuu ambayo yamo katika Mpango Mkakati wa Wizara kama ifuatavyo:

1. Kuhakikisha kuwa Mapungufu katika Sera na Sheria zinazohusu Watoto, Wanawake, Vijana na Wazee yanafanyiwa kazi.
2. Kukuza uwezo wa Wizara kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.
3. Kuimarisha uratibu wa mwitiko wa Wadau na watoa huduma wa masuala yanayohusu Watoto, Wanawake, Vijana na Wazee.
4. Kukuza uelewa wa jamii kuhusu masuala ya Watoto, Wanawake, Vijana na Wazee.
5. Kuimarisha ufikiwaji na kuimarisha ubora wa huduma za uhifadhi na kinga kwa Watoto, Vijana, Wanawake na Wazee.
6. Kuhakikisha kuwa haki za Watoto, Wanawake, Vijana, na Wazee zinafuatiliwa na kutolewa taarifa mara kwa mara.
7. Kuimarisha hali za kiuchumi, utamaduni na maendeleo kwa Wanawake, Vijana, Watoto na Wazee.

UTEKELEZAJI WA MALENGO YA WIZARA KWA MWAKA 2011/2012.

IDARA YA MIPANGO SERA NA UTAFITI:

Mhe. Mwenyekiti, Idara ya Mipango, Sera na Utafiti ndio kiungo kikuu cha Wizara na ina jukumu la kuratibu utayarishaji wa Sera, Sheria, Mipango ya Maendeleo, kufanya ufuatiliaji na tathmini na tafiti mbali mbali zinazohusiana na walengwa wa Wizara. Pia inaratibu na kusimamia utekelezaji wa masuala ya kijinsia, miradi ya Wizara, mahusiano na mashirikiano ya Kitaifa, Kikanda na Kimataifa yanayohusu Wizara. Aidha, Idara inasimamia uingizwaji wa masuala mtambuka katika mipango na shughuli zote za Wizara.

Mhe. Mwenyekiti, katika kipindi cha mwaka 2011/2012, Idara hii ilijipangia kutekeleza malengo yafuatayo:

1. Kuhakikisha kuwa Mapungufu katika Sheria na Sera zinazohusu Watoto, Wanawake, Vijana na Wazee yanafanyiwa kazi.
2. Kukuza uelewa wa jamii katika masuala ya msingi yanayohusu Watoto, Wanawake, Vijana na Wazee.
3. Kuimarisha ukusanyaji wa taarifa, uwekaji wa kumbukumbu na kutayarisha mfumo wa mawasiliano wa Wizara.
4. Kusimamia uandaaji wa tafiti zinazohusu Watoto, Vijana, Wanawake na Wazee.
5. Kuimarisha mashirikiano ya Kitaifa, Kikanda na Kimataifa.
6. Kutekeleza Programu ya kupambana na UKIMWI katika maeneo ya kazi.
7. Kupanga na kusimamia utekelezaji wa miradi ya Wizara.

Utekelezaji wa malengo ya Idara ya Mipango, Sera na Utafiti:

Mhe. Mwenyekiti, Wizara imeifanyia mapitio Sera ya Maendeleo ya Vijana (2005) kwa kushirikiana na Wadau wa Maendeleo ya Vijana wakiwemo Watu wenye Ulemavu, Asasi za Kiraia, Wanafunzi wa Sekondari na Vyuo, Vyama vya Siasa na Viongozi wa Kidini. Tathmini ya Hali Halisi ya Vijana Zanzibar ilifanyika ambayo iliimarisha Rasimu ya Sera hiyo. Sera hiyo imeshajadiliwa katika kikao cha Kamati ya Uongozi na ipo katika hatua za mwisho za mapitio katika vyombo vya maamuzi ili iweze kupitishwa na kutumika.

Mhe. Mwenyekiti, Wizara inapitia Sera ya Uhai, Hifadhi, na Maendeleo ya Mtoto ya mwaka 2001, ili izingatie Sheria ya Mtoto ya mwaka 2011, masuala ya Malezi na Makuzi ya Watoto wenye umri kati ya miaka 0-8 “Early Childhood Development” na Watoto wanaokinzana na Sheria. Mtaalamu Mwelekezi amepatikana na ameshaanza mchakato wa kupitia sera hiyo. Aidha, Wizara ipo katika hatua ya kufanya utafiti mdogo juu ya Makuzi ya Awali ya Mtoto ili kuimarisha Sera hiyo.

Mhe. Mwenyekiti, Wizara katika kipindi cha mwaka 2011/2012 imemalizia utayarishaji wa Sera ya Jinsia. Hivi sasa, Sera hiyo tayari imeshatafsiriwa kwa lugha ya Kiswahili na inasubiri kupitiwa katika kikao cha Kamati ya Uongozi ya Wizara ili iwasilishwe katika Kikao cha Makatibu Wakuu.

Mhe. Mwenyekiti, Wizara inaendelea na utaratibu wa kuandaa Sera ya Hifadhi ya Jamii ambapo Rasimu ya awali iliyotayarishwa ilionekana kutozingatia maeneo ya Ustawi wa Jamii, Masuala ya Wazee, Watoto na makundi maalum. Hivyo, Wizara ilianza utaratibu mpya wa kuandaa Rasimu nyengine itakayozingatia mapungufu yaliyobainika. Kwa kushirikiana na wataalamu waelekezi tathmini imefanywa Unguja na Pemba ya kuangalia hali halisi ya umasikini katika jamii kwa lengo la kuoanisha na takwimu zilizopo na hatimae kuweza kushauri maeneo ya vipaumbele yatayozingatiwa katika mchakato wa kutayarisha Sera hiyo.

Mhe. Mwenyekiti, Wizara imefanya Mapitio ya Sheria ya Mahkama ya Kadhi ya mwaka 1985 ili iendane na hali halisi ya mabadiliko ya dhana ya usawa wa jinsia bila ya kukiuka misingi ya Dini ya Kiislamu. Kazi hiyo inafanywa kwa mashirikiano na Wizara ya Katiba na Sheria na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Uchambuzi wa Sheria hiyo umefanyika kwa kukusanya maoni ya wadau mbali mbali, wakiwemo Viongozi wa Dini, Taasisi na Asasi za Kiraia na Wanasheria chini ya Kamati ya Usimamizi. Hivi sasa mswada wa mapendekezo ya Sheria mpya ya Mahkama ya Kadhi umeandaliwa na unatarajiwa kupelekwa katika ngazi husika.

Mhe. Mwenyekiti, Wizara iliandaa Mpango Mkakati (2011-2015), kuchapisha nakala 500 za Mpango huo na kuzisambaza kwa Wadau kwa utekelezaji. Mpango Mkakati huo umeainisha majukumu ya kiutendaji kwa kila

Idara, rasilimali watu na vifaa vinavyohitajika. Pia, Wizara imetafsiri Mpango Mkakati kwa lugha ya Kiswahili. Aidha, Kamati Mtambuka ya Wizara imeundwa kwa lengo la kuratibu na kuzingatia masuala mtambuka katika Sera, Mipango na Bajeti ya Wizara. Wizara vilevile, ipo katika hatua ya kutayarisha kitini kitachozingatia masuala ya UKIMWI, Jinsia na Haki za binaadamu katika Sera, Mipango na Bajeti.

Mhe. Mwenyekiti, Wizara iliandaa Mpango wa Ufuatiliaji na Tathmini wa Wizara wenye lengo la kuzingatia utekelezaji wa Mpango Mkakati wa Wizara. Kupitia mpango huo Fomu maalum za ufuatiliaji wa utekelezaji wa Majukumu ya Wizara zimetayarishwa na kutafsiriwa kwa lugha ya Kiswahili. Vilevile, Mfumo huo umeoanishwa na mfumo wa kukusanya taarifa za utekelezaji wa MKUZA na Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya 2010-2015 . Hivi sasa tayari taarifa zote za Wizara zinawasilishwa kupitia Fomu hizo.

Mhe. Mwenyekiti, Wizara imeendelea kukiimarisha Kitengo chake cha Habari na Uwekaji wa Kumbukumbu. Makisio na mahitaji ya kukiimarisha Kitengo hicho yameandaliwa, ambapo baadhi ya vifaa tayari vimeshaanza kununuliwa. Vilevile, Wizara inaendelea na matayarisho ya uanzishaji wa jarida, ambalo linatarajiwa kutolewa mara moja kwa mwaka na litakuwa na taarifa na matukio muhimu ya Wizara yakiwemo yanayohusu maendeleo ya Wanawake, Vijana, Wazee na Watoto.

Mhe. Mwenyekiti, aidha, Wizara imetayarisha na kurusha hewani vipindi 31 kupitia redio na televisheni. Pia, imeandaa makala 27 na kuyachapisha kupitia gazeti la Zanzibar Leo. Habari 89 za matukio zimeandaliwa na kurushwa hewani kupitia redio na televisheni kwa lengo la kutoa habari

Mhe. Mwenyekiti, Wizara imeandaa maandiko ya miradi minane na kujumuishwa katika Mpango wa miaka mitano wa Kitaifa wa Utekelezaji wa MKUZA II. Maandiko hayo yalihusu programu za Kukuza ukusanyaji na Uchambuzi wa Takwimu Kijinsia, Kuanzisha Benki ya Wanawake, Kujenga uwezo wa jamii kupinga vitendo vya udhalilishaji kijinsia, Kilimo cha Rosella na Ujenzi wa Jengo la Wizara kwa Unguja. Vilevile, Wizara imeandaa na kuibua ajenda 9 za tafiti. Ajenda hizo ni pamoja na Tatizo la Ombaomba, Kuwawezesha Vijana na Wanawake Kiuchumi, Talaka na Athari zake na Tathmini ya Malezi na Makuzi ya Watoto wenye umri kuanzia mwaka 0-8 (**Angalia Kiambatanisho Nam. 1**). Wizara aidha, imo katika hatua ya kufanya utafiti wa omba omba ili kuangalia kiini cha tatizo na imefanya mafunzo ya siku tano ya utafiti kwa Wafanyakazi wa Wizara.

UTEKELEZAJI WA PROGRAMU ZINAZOSIMAMIWA NA IDARA YA MIPANGO SERA NA UTAFITI

Mhe. Mwenyekiti, Wizara katika kipindi cha mwaka 2011/2012 imesimamia utekelezaji wa Programu mbili zifuatazo:-

1. **Programu ya Jinsia Zanzibar.**

Mhe. Mwenyekiti, programu hii inatekelezwa na Wizara kwa kushirikiana na Shirika la Kimataifa la Idadi ya Watu Duniani (UNFPA), na ina madhumuni ya kuisaidia Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na wadau kuzingatia masuala ya kijinsia katika Mipango na Bajeti, kuzijengea uwezo taasisi mbalimbali na wananchi katika kupambana na udhalilishaji wa kijinsia.

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka 2011/2012, programu imetekeleza yafuatayo:-
Kuiwezesha Kamati ya Kitaifa dhidi ya ukatili wa kijinsia kufanya ukaguzi na tathmini ya huduma zinazotolewa kwa waathirika wa vitendo vya ukatili dhidi ya wanawake na watoto, kuupitia muongozo wa kufanya ukaguzi, ufuatiliaji na tathmini, kufanya zoezi la majaribio la Muongozo huo, kufanya ukaguzi wa huduma zinazotolewa katika vituo vitano vya Polisi na Hospitali tano Unguja na Pemba.

Mhe. Mwenyekiti, Wizara pia, imeandaa ripoti ya saba kwa upande wa Zanzibar ya utekelezaji wa Mkataba wa Kimataifa wa Kuondoa Aina Zote Za Ubaguzi Dhidi ya Wanawake (CEDAW) ya mwaka 2007-2010. Rasimu ya Ripoti hii ilijadiliwa katika mikutano miwili ya Wadau Unguja na Pemba. Ripoti hiyo itajumuishwa na ya Tanzania Bara kwa kuwasilishwa Umoja wa Mataifa.

Mhe. Mwenyekiti, Wizara imeandaa Muongozo wa Uzingatiaji wa Masuala ya Jinsia katika Sera, Mipango na Bajeti za Taasisi mbali mbali. Zoezi hilo limewahusisha Wakurugenzi Mipango na Maafisa Jinsia wa Sekta. Hatua iliyobaki ni kujadiliwa kwa mara ya mwisho na kupitishwa na Wadau.

Mhe. Mwenyekiti, Wizara imefanya mapitio ya Mfumo wa Ufuatiliaji na Tathmini wa Masula ya jinsia kwa kuingiza Viashiria vya MKUZA II pamoja na viashiria vya Mkataba wa Kuondoa Aina zote za Ubaguzi Dhidi ya Wanawake (CEDAW). Mfumo huo ulijadiliwa na wadau pamoja na kufanyiwa majaribio.

Programu ya Kukuza Ukusanyaji na Uchambuzi wa Takwimu Kijinsia.

Mhe. Mwenyekiti, programu hii inatekelezwa na Wizara kwa mashirikiano na Mfuko wa Jumuiya ya Ulaya (E.U) ambayo itatekelezwa kwa kipindi cha mwaka mmoja (Machi, 2012 - Machi, 2013). Lengo kuu la programu hii ni Kuisaidia Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika jitihada za kukuza usawa wa kijinsia na uwezeshaji wa Wanawake. Aidha, Programu itakuza uwezo wa Wizara pamoja na Sekta nyengine muhimu katika kukusanya, kuzichambua na kuzisambaza takwimu kijinsia. Matayarisho ya awali ya utekelezaji wa Programu hiyo ikiwemo ununuzi wa vifaa, utafutaji Wataalamu Waelekezi na kuunda Kamati ya Kitaalamu na Kamati ya Usimamizi wa Programu yamefanyika.

Mhe. Mwenyekiti, katika kipindi cha mwaka 2012/2013 Idara ya Mipango, Sera na Utafiti imekusudia kutekeleza shabaha zifuatazo ili kufikia malengo ya Wizara:-

1. Kuendelea kuratibu utayarishaji na upitiaji wa Sera, Sheria na tafiti mbali mbali kwa kuzingatia mikakati na malengo ya Wizara.
2. Kuratibu uandaaji wa Mipango na Bajeti ya Wizara.
3. Kuimarisha mashirikiano ya Kitaifa, Kikanda na Kimataifa.
4. Kusimamia uingizaji wa masuala mtambuka katika Bajeti, Programu na Mipango ya Wizara.
5. Kusimamia utekelezaji wa miradi ya Wizara.
6. Kuimarisha mfumo wa uratibu wa mawasiliano, ufuatiliaji na tathmini wa shughuli za Wizara.

Mhe. Mwenyekiti, ili Idara ya Mipango**,** Sera na Utafiti iweze kutekeleza malengo yake iliyojiwekea kwa mwaka 2012/2013, naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha jumla ya Shilingi Milioni Mia Tatu na Kumi na Nane, Laki Moja na Kumi na Tatu Elfu (318,113,000/=) kwa ajili ya matumizi ya Kazi za Kawaida na Mishahara na Shilingi Milioni Mia Sita na Kumi na Sita (616,000,000/=) kwa Kazi za Maendeleo.

IDARA YA UENDESHAJI NA UTUMISHI

Mhe. Mwenyekiti, Idara hii ina jukumu la kusimamia shughuli za kila siku za uendeshaji na utumishi za Wizara zikiwemo sheria na kanuni za utumishi, mafunzo, maslahi, kutunza kumbukumbu na maendeleo ya wafanyakazi pamoja na utunzaji wa mali za Wizara. Aidha, Idara inasimamia masuala ya ajira, haki, maslahi na nidhamu kwa Wafanyakazi wa Wizara.

Mhe. Mwenyekiti, katika kipindi cha 2011/2012, Idara ilijipangia kutekeleza malengo yafuatayo:

1. Kufanya Tathmini ya Uwezo wa Raslimali Watu katika Wizara.
2. Kutayarisha Mpango wa mafunzo wa Wizara na kuutekeleza.
3. Kukuza uwezo wa uendeshaji wa Wizara.
4. Kufuatilia suala la ujenzi wa majengo ya Wizara Unguja na Pemba.

Utekelezaji wa Malengo kwa Idara ya Uendeshaji na Utumishi

Mhe. Mwenyekiti, Wizara imefanya Tathmini ya Uwezo wake ili kujua mapungufu na mahitaji katika maeneo ya Rasilimali watu, fedha na vifaa. Tayari hatua ya kukusanya taarifa na uchambuzi imeshafanyika na zoezi la uandishi wa taarifa ya mwisho pamoja na Mpango wa Mafunzo linaendelea.

Mhe. Mwenyekiti, Wizara imeajiri wafanyakazi watano (5) na kupokea Wafanyakazi saba (7) waliohamishiwa kutoka Taasisi nyengine za Serikali Unguja na Pemba (Angalia Kiambatanisho namba 2a). Aidha, jumla ya Wafanyakazi wanne (4) walipatiwa uhamisho kwenda kuendelea na kazi katika taasisi nyengine za Serikali, wengine watano (5) walistaafu kisheria, Mfanyakazi Mmoja (1) kaacha kazi na Mfanyakazi mmoja (1) alifariki dunia (Angalia Kiambatanisho namba 2b).

Mhe. Mwenyekiti, Wizara iliwawezesha Wafanyakazi kumi na tisa (19) Unguja na Pemba kupata mafunzo ya muda mrefu na mfupi katika fani tofauti na vyuo mbalimbali ndani na nje ya nchi. (Angalia Kiambatanisho namba **3**). Pia Wizara iliendesha mafunzo maalum ya Sheria Nam. 2 ya Utumishi wa Umma na sheria nyingine za kazi kwa Maofisa Waandamizi sitini (60) Unguja na Pemba. Lengo la mafunzo ni kuwaelimisha na kuwakumbusha maofisa juu ya wajibu, nidhamu ya kazi, haki na maslahi ya wafanyakazi ili kufanyakazi kwa kufuata miongozo na taratibu za kisheria (G.O).

Mhe. Mwenyekiti, katika kuwaandaa Wafanyakazi wake kisayansi na kiteknolojia, Wizara imewapatia mafunzo ya kompyuta Wafanyakazi ishirini katika Chuo Kikuu cha Taifa, (SUZA). Wizara inalenga kuwapatia taaluma hii watendaji wake wote Unguja na Pemba.

Mhe. Mwenyekiti, Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Nchi (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora pamoja na Wizara ya Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo, imeshughulikia na kuanza kuwapatia posho la mazingira magumu Wafanyakazi mia moja na kumi na nane (118) wanaotoa huduma katika vituo vya kutunza Wazee vya Welezo na Sebleni kwa upande wa Unguja na Gombani na Limbani kwa upande wa Pemba. Posho kama hilo pia, limetolewa kwa Wafanyakazi wa nyumba ya kulelea Watoto Mazizini. Aidha, Wizara imelipa posho la saa za ziada kwa Walinzi, Madereva na Wahudumu wa Wizara wanaostahiki.

Mhe. Mwenyekiti, Wizara imetayarisha Mpango wa Manunuzi na kuweka Daftari la Kudumu la Hifadhi ya Mali za Serikali, kwa mujibu wa Sheria ya Manunuzi ya mwaka 2005. Kupitia Mpango huo, Wizara ilinunua vifaa mbalimbali iliojipangia kwa mwaka huu. Pia, Wizara inasimamia ukarabati wa Nyumba za Wazee Sebleni kwa kutafuta Mkandarasi wa kukarabati Ukumbi wa mikutano kwa mujibu wa taratibu za manunuzi na hivi saa kazi ya ukarabati inaendelea.

Mhe. Mwenyekiti, Wizara imeunda Bodi ya Zabuni na Kamati ya Ukaguzi wa ndani kwa mujibu wa Sheria za Manunuzi na Usimamizi wa Fedha za Umma za mwaka 2005, kwa ajili ya kusimamia vyema taratibu za fedha na manunuzi. Kamati hiyo na Bodi zimeanza kazi zake rasmi.

Mhe. Mwenyekiti, Wizara inakabiliwa na tatizo kubwa la ukosefu wa majengo ya ofisi Unguja na Pemba yanayofaa na kutosha kwa kufanyakazi. Kwa upande wa Pemba, Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo zimo katika hatua za kumpata Mshauri elekezi atakaesimamia ujenzi wa jengo la pamoja. Kwa upande wa Unguja, mahitaji ya Ofisi ya Wizara yametayarishwa na kuwasilishwa Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo kwa kupatiwa ufumbuzi.

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha wa 2012/2013 Idara ya Uendeshaji na Utumishi imejipangia kutekeleza shabaha zifuatazo ili kufikia Malengo ya Wizara:

1. Kusimamia shughuli za kila siku za uendeshaji na utumishi za Wizara ikiwemo sheria na kanuni za utumishi pamoja na uwekaji wa kumbukumbu za Wafanyakazi.
2. Kuwajengea uwezo wafanyakazi wa Wizara kwa kuwasaidia malipo ya mafunzo ya muda mrefu na mfupi kwa kufuata mpango wa mafunzo.
3. Kusimamia na kufuatilia suala la ujenzi wa majengo ya Wizara, Unguja na Pemba.

Mhe. Mwenyekiti, Ili Idara ya Uendeshaji na Utumishi iweze kutekeleza majukumu yake iliojiwekea kwa mwaka 2012/2013, Naliomba Baraza lako Tukufu liidhinishe jumla ya Shilingi Milioni Mia Sita na Ishirini na tano, Laki tatu na Tisini na Tano (625,395,000/-) kwa ajili ya matumizi ya Kazi za Kawaida na Mishahara.

IDARA YA USTAWI WA JAMII

Mhe. Mwenyekiti, Idara ya Ustawi wa Jamii ina lengo la kuhakikisha hali ya ustawi inapatikana katika jamii na kuimarisha uratibu na utoaji wa huduma za kijamii kwa Wazee, Watoto na makundi mengine yanayoishi katika mazingira magumu zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2011/2012, Idara ya Ustawi wa Jamii ilijipangia kutekeleza malengo yafuatayo:-

1. Kutoa misaada ya kiustawi kwa watoto wanaoishi katika mazingira magumu zaidi na watu walio katika makundi maalumu Unguja na Pemba.

2. Kuimarisha huduma kwa wazee.

3. Kutayarisha Sera ya Ustawi na Hifadhi ya Jamii, miongozo na tafiti na kusimamia utekelezaji wake.

4. Kutoa elimu kwa jamii na wadau juu ya umuhimu na wajibu wao katika kuwatunza watoto, wazee na walio katika mazingira magumu zaidi.

5. Kuimarisha huduma kwa watoto wanaolelewa katika vituo na Hifadhi ya Mtoto kwa ujumla.

Utekelezaji wa Malengo kwa Idara ya Ustawi wa Jamii

Mhe. Mwenyekiti, Wizara imeendelea kutoa misaada ya kijamii kwa watu wasiojiweza na walio katika makundi maalumu katika jamii. Jumla ya familia 107 (Pemba 45 na Unguja 62) zinazoishi katika mazingira magumu, zilisaidiwa (Angalia Kiambatanisho Nam. 4a na 4b). Aidha, Wizara iliwapatia watoto 50 wa Unguja wanaoishi katika mazingira magumu zaidi sare za skuli ambapo kila mtoto alipatiwa seti mbili za sare pamoja na vifaa vya kuandikia. (Angalia Kiambatanisho Nam. 5). Wizara kwa kushirikiana na Jumuia ya EPHAPHATHA ya Korea ilitoa msaada wa chakula na viatu kwa Watoto 662 Wanaoishi Katika Mazingira Magumu Zaidi Unguja na Pemba (Angalia Kiambatanisho Nam. 6).

Mhe. Mwenyekiti, Wizara imeendelea kutoa matunzo na huduma kwa Wazee wanaoishi katika Nyumba za Wazee Unguja na Pemba. Jumla ya Wazee 108 (Wanawake 50 na Wanaume 58) wanapatiwa huduma katika makao hayo. Aidha, Wizara imeongeza posho la Wazee wanaoishi katika Nyumba hizo, kutoka Shilingi 25,000/- hadi kufikia 40,000/- kwa Wazee wa Sebleni, Limbani na Gombani. Kutoka Shilingi 7,000/- hadi 15,000/- kwa Wazee wa Welezo. Pia, Wizara iliwanunulia Wazee nguo mpya kwa ajili ya Sikukuu ya Eid el Fitri. Aidha, iliendelea kuwapatia posho Wazee 62 ambao ni waathirika wa ugonjwa wa Ukoma walioko Makundeni Pemba shilingi 25,000/- kwa mwezi kila mmoja.

Mhe. Mwenyekiti, Wizara ilizika jumla ya maiti 20 zisizokuwa na wenyewe Unguja na Pemba. Wizara imeendelea kulipa fidia kwa Wafanyakazi waliopatwa na ajali wakiwa kazini. Hadi kufikia mwezi Aprili, 2012, jumla ya Shillingi milioni kumi na mbili na laki saba (12, 700,000/-) zimetumika kulipa Wafanyakazi kumi na tisa (19) kutoka katika maofisi ya Serikali Unguja na Pemba, (Angalia kiambatanisho Nam. 7).

Mhe. Mwenyekiti, Wizara imeanza ukarabati wa ukumbi wa Sebleni na tunatarajia kufanya ukarabati wa jiko hapo baadae. Kwa upande wa Makao ya Wazee huko Pemba, Wizara imefanya matengenezo madogo katika Makao ya Wazee Limbani na Gombani.

Mhe. Mwenyekiti, Siku ya Wazee duniani iliadhimishwa tarehe 1 Oktoba 2011, kitaifa katika Makao ya Wazee Sebleni. Viongozi mbali mbali wa Serikali, Wastaafu pamoja na Wanajamii walihudhuria. Ujumbe wa mwaka huu ulikuwa ni “Kuongezeka kwa Changamoto na Fursa kwa Wazee Duniani”.

Mhe. Mwenyekiti, Wizara ilifanya uzinduzi na kutoa mafunzo kwa wakufunzi juu ya Muongozo wa Kitaifa wa Hifadhi na Ustawi wa Watoto Zanzibar. Muongozo huo unalenga kutoa muelekeo wa kushughulikia masuala yanayohusu Hifadhi na Ustawi wa Mtoto. Wakufunzi watatoa mafunzo kwa Kamati katika kila Wilaya za Unguja na Pemba na kujengewa uwezo wa namna ya kutumia muongozo huo.

Mhe. Mwenyekiti, Wizara imepokea jumla ya malalamiko 215 ya udhalilishaji wa watoto yanayohusu kubakwa, kulawitiwa, kupewa ujauzito, kudhalilishwa kimwili na kukashifiwa (Angalia Kiambatisho Nam. 8). Aidha, Kituo

Rafiki Mkono kwa Mkono (*One Stop Centre*) kinaendelea kupokea kesi mbali mbali za udhalilishaji wa Watoto. Jumla ya kesi 689 za udhalilishaji wa Watoto zilipokelewa na kushughulikiwa. (Angalia kiambatanisho Nam. 9).

Wizara imepokea jumla ya malalamiko 393 yanayohusu matunzo na kugombania Watoto kwa Unguja na Pemba. Wizara hupokea malalamiko hayo na kuyatafutia ufumbuzi kwa kushirikiana na walengwa wa pande zote mbili (Mlalamikaji na mlalamikiwa) na inaposhindikana kufikia makubaliano Wizara huwashauri wahusika kwenda katika mahakama ili kulishughulikia tatizo husika kisheria (Angalia Kiambatanisho Nam. 10).

Mhe. Mwenyekiti, Wizara iliupatia Uongozi wa Nyumba ya Kulelea Watoto Mazizini, Shilingi milioni tatu (3, 000,000/-) kila mwezi kwa ajili ya uendeshaji, na kuwanunulia watoto wote 47 (W'ume 19 na W'ke 28) nguo za Sikukuu. Vile vile, Wizara ilifanya utanuzi wa jiko la nje pamoja na kuliwekea zege eneo la nyuma ya nyumba hiyo. Wizara ililipa ada ya chuo na posho la Mwanafunzi anaesoma Chuo Kikuu, Wanafunzi wa Skuli za msingi pamoja na kuwanunulia sare na vifaa vya Skuli. Kutokana na kuongezeka kwa bei za bidhaa, Wizara inakusudia kuongeza ruzuku kwa nyumba hiyo kutoka Shilingi milioni tatu (3,000,000/-) hadi (4,000,000/-) kwa mwezi.

Aidha, Wizara ilikisaidia Kijiji cha Kulelea Watoto cha SOS kwa kuwapatia jumla ya Shilling milioni moja (1,000,000/-).

Mhe. Mwenyekiti, Wizara ilifanya ukaguzi wa Vituo vyote vya kulelea Watoto Unguja na Pemba. Jumla ya Vituo vinane (8) kwa Unguja na vitano (5) kwa Pemba vilitambuliwa, kukaguliwa na kupatiwa miongozo ya uendeshaji. (Angalia kiambatanisho Nam. 11).

Wizara pia, ilifanya Mkutano na wadau kusambaza Miongozo ya uanzishaji na uendeshaji Vituo vya kulelea Watoto yatima. Miongozo hiyo ina lengo la kuweka uwiano na ubora wa utoaji wa huduma kwa taasisi zote zinazoendesha Vituo vya kulelea watoto hapa Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, Wizara ilifanya mikutano sita ya Kamati ya Kitaifa ya Hifadhi ya Mtoto ili kujadili na kufuatilia kesi mbali mbali zinazohusu udhalilishaji wa Watoto. Pia, Wizara ilipitia Mfumo wa kuhifadhi taarifa za Watoto Wanaoishi katika Mazingira Magumu Zaidi (*Database*). Aidha, Wizara ilifanya Mkutano mmoja wa mashirikiano na Wadau wanaoshughulikia masuala ya Watoto wanaoishi katika Mazingira Magumu zaidi ili kujadili maendeleo na kadhia mbali mbali zinazowahusu watoto. Sambamba na hayo, Wizara ilifanya Mkutano na Watendaji wa Ofisi za *WAKF*, Vizazi na Vifo na Ofisi ya Mufti ili kujadili masuala ya utoaji huduma kwa Watoto wanaoishi katika Mazingira Magumu zaidi na namna ya kuboresha huduma hizo.

Mhe. Mwenyekiti, Kituo cha Mkono kwa Mkono katika Hospitali ya Chake Chake Pemba tayari kimekamilika na Wizara ipo katika hatua ya kuanzisha vituo kama hivyo katika Wilaya za Wete, Kusini na Kaskazini Unguja.

Mhe. Mwenyekiti, Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2012/2013 Idara ya Ustawi wa Jamii imejipangia kutekeleza shabaha zifuatazo ili kufikia Malengo ya Wizara:-

1. Kuimarisha, kuratibu na kujenga mazingira mazuri ya Hifadhi ya Mtoto.
2. Kuratibu utekelezaji wa Sera ya hifadhi ya Jamii kwa kushirikiana na taasisi husika.
3. Kuimarisha huduma na ustawi kwa Wazee.
4. Kuratibu na kutathmini masuala ya Makuzi ya Awali (0-8) kwa Mtoto.
5. Kusimamia masuala ya fidia kwa Wafanyakazi wanaopata ajali kazini.
6. Kuimarisha mfumo wa kuhifadhi taarifa za watoto.

Mhe. Mwenyekiti, Ili Idara ya Ustawi wa Jamii iweze kutekeleza vyema malengo yake kwa mwaka 2012/2013, naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha matumizi ya jumla ya Shilingi Milioni Mia sita na Kumi na sita, laki tatu na sabini na tisa elfu (616,379,000/-) kwa kazi zake za kawaida na Mishahara na Shilingi Milioni Mia Tano na Sabiini na Laki Sita (570,600,000/-) kwa kazi za Maendeleo.

IDARA YA MAENDELEO YA VIJANA

Mhe. Mwenyekiti, Idara ya Maendeleo ya Vijana ina jukumu la kuratibu na kusimamia utekelezaji wa Sera ya Maendeleo ya Vijana na kujenga mazingira endelevu ya kuwawezesha Vijana kujiimarisha Kiuchumi, Kiutamaduni na Kijamii.

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2011/12, Idara ilijipangia kutekeleza malengo yafuatayo:-

1. Kukuza uwezo wa Kiutendaji wa Idara.
2. Kukamilisha Uundaji wa Baraza la Vijana Zanzibar.
3. Kuratibu Mbio za Mwenge wa Uhuru na Wiki ya Vijana Kitaifa.
4. Kuendeleza na kuimarisha vikundi vya Vijana vya Uzalishaji mali kwa kutoa mafunzo ya uanzishaji na uendelezaji wa *SACCOS*, Ujasiriamali, Uongozi na Utunzaji wa Hesabu.
5. Kutayarisha Mpango wa Maendeleo ya Vijana.
6. Kufanya mapitio ya Sera ya Maendeleo ya Vijana.
7. Kujenga Uwezo wa Vijana kupitia Stadi za maisha, Vita dhidi ya UKIMWI na Dawa za Kulevya.
8. Kuendeleza Mashirikiano na Uhusiano wa Taasisi za Vijana ndani na nje ya Nchi.

Utekelezaji wa Malengo ya Idara ya Maendeleo ya Vijana:

Mhe. Mwenyekiti, Rasimu ya Katiba ya Baraza la Vijana Zanzibar imejadiliwa kupitia vikao mbali mbali vya wadau ikiwemo Watu Wenye Ulemavu, Taasisi zisizo za Kiserikali, Wanafunzi wa Sekondari na Vyuo, Kamati Tendaji na Kamati ya Uongozi ya Wizara. Rasimu hiyo imeshajadiliwa katika Kikao cha Makatibu Wakuu na kwa mapendekezo ya Kikao hicho, Wizara imeiwasilisha kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ushauri wa kitaalamu.

Mhe. Mwenyekiti, Wizara imeshiriki kikamilifu katika maandalizi, uzinduzi na tathmini ya Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa mwaka 2011 pamoja na kilele cha Mbio hizo. Mbio hizo ziliambatana na Maadhimisho ya Miaka 50 ya Uhuru wa Tanzania Bara. Kufuatia tathmini ya Mbio za Mwenge za mwaka 2011, Mkoa wa Kusini Pemba ulitangazwa rasmi kupata ushindi kwa Kanda ya Zanzibar.

Aidha, Miradi 33 yenye thamani ya Tsh. Bilioni moja, milioni mia mbili na sabini na tatu, laki mbili na kumi na nne elfu, mia sita na thamanini na moja (1,273,214,681/-) ilizinduliwa na kuwekewa Mawe ya Msingi na Tshs. Milioni thalathini na nane, laki nane na ishirini na sita elfu na mia saba (38,826,700/-) zimechangwa Unguja na Pemba (Angalia Kiambatanisho Nam. 12a na 12b).

Mhe. Mwenyekiti, Wizara imesimamia upatikanaji wa fedha kwa vikundi 6 vya vijana (Unguja 2 na Pemba 4) vilivyobahatika kupata Ruzuku ya Dola za Kimarekani 85,000 kupitia Mfuko wa Vijana wa *UN Habitat* kutoka Serikali ya Norway (Angalia Kiambatisho Nam. 13), asilimia 60 ya fedha hizo tayari zimetolewa na asilimia 40 zitatolewa baada ya kupeleka ripoti ya matumizi. Pamoja na mikopo hiyo, vikundi 9 vilipatiwa mafunzo ya kuendesha miradi (Angalia Kiambatanisho Nam. 14).

Wizara aidha, imetoa mafunzo kwa Viongozi wa Vikundi vya Vijana 40 (Wanawake 19 na Wanaume 21) Pemba. Pia, jumla ya vikundi 170 vya Vijana (71 Unguja na 99 Pemba) vilitembelewa na kupewa ushauri na maelekezo jinsi ya kuendesha miradi yao. (Angalia Kiambatanisho Nam. 15). Sambamba na mafunzo hayo, Wizara kwa kushirikiana na Mradi wa ujenzi wa Barabara 5 za Mkoa wa Kaskazini Pemba (*Millenium Challenge Account, MCA-T*) imetoa mafunzo kwa viongozi wa vikundi 8 kwa lengo la kuwajengea uwezo viongozi hao waweze kufanya shughuli zao kwa ufanisi na kuepuka migogoro (Angalia Kiambatanisho Nam. 16).

Mhe. Mwenyekiti, Mpango wa Serikali wa Mikopo kwa Vijana umezinduliwa na Makamo wa Pili wa Rais, Balozi Seif Ali Iddi mwezi Januari, 2012 na mafunzo ya Ujasiriamali kwa Vijana *SACCOS* yametolewa Unguja na Pemba, mafunzo hayo yamepelekea kuanzishwa kwa *SACCOS* Mbili kubwa; moja Unguja na moja Pemba ambazo zitawaunganisha Vijana na kuweza kupata Mikopo kupitia Benki ya *CRDB*. Jumla ya Shilingi Milioni 60 za Mikopo zimeshatolewa. Aidha, Kamati ya Uongozi na Usimamizi wa mpango wa mikopo imezinduliwa mwezi Machi, 2012.

Mhe. Mwenyekiti, Wizara imewezesha na kufanikisha upatikanaji wa eneo la kilimo kwa Vijana. Eneo hilo litatumika kwa kilimo cha mauwa ya Karkadei (*Rosella*) na mbogamboga huko Tunguu kwa Unguja na Mbuzini Pemba. Jumla ya Vijana 20 (wanaume 15 na wanawake 5) Unguja kupitia Jumuiya ya *ZASOSE* watanufaika na kilimo cha maua. Kwa upande wa Pemba kazi ya kuwahamasisha na kuwasajili vijana kujiunga na kushiriki katika kilimo hicho imeshafanyika.

Mhe. Mwenyekiti, Wizara ilifanya mazungumzo na Wafanyabiashara wa ndani pamoja na Mashirika ya Umma juu ya upatikanaji wa ajira kwa Vijana na kuchangia uimarishaji wa Usafi wa Mji wa Zanzibar. Aidha, Vijana 700 kutoka Jumuiya ya *ZASOSE* wamehamasishwa katika Kampeni ya kupambana na uchafu katika Mji wa Zanzibar iliyozinduliwa mwezi Julai, 2011. Kupitia Kampeni hiyo, Vijana 135 wamepata ajira za muda, kati ya hao 45 wamepata ajira ya usafi wa Mji na kupatiwa vitendea kazi vyenye thamani ya sh. 8,500,000/= zilizotolewa na Wahisani wa ndani. Vijana 90 wamepata ajira za muda na Vijana 5 wamepata ajira ya kudumu katika Shirika la Simu la Zantel. Aidha, Vijana 100 wamepata ajira ya kulinda minara ya Zantel (Pemba 40 na Unguja 60), Vijana 30 wamepata ajira ya kusimamia eneo la soko la *Sunday Market* Michenzani, Vijana 15 wamepata ajira ya ulinzi katika hospitali ya Mnazi mmoja, Vijana 20 kufanya usafi Wilaya ya Magharibi na Vijana 40 wamepata ajira ya kutengeneza Mkaa kwa kutumia takataka.

Mhe. Mwenyekiti, Wizara imewaunganisha Vijana kupata fursa ya kushiriki katika Makongamano mbali mbali ndani na nje ya nchi kwa lengo la kuwaunganisha vijana wa Zanzibar na nchi mbali mbali duniani kuzungumzia mustakbali wa maendeleo yao. Jumla ya vijana 2 (1 Unguja na 1 Pemba) walishiriki katika Makongamano na Mikutano.

Aidha, Kambi 16 za Kimataifa za Vijana zimeandaliwa Maungani, Bambi, Bwejuu, Fuoni kwa Unguja; Ngo'mbeni na Kiwani kwa Pemba zenye idadi ya Vijana 221, (Wanawake 120 na Wanaume 101) kutoka Korea, Ufaransa, Tanzania, Ujerumani, Kenya na Ubeligiji kwa lengo la kuendeleza mashirikiano na uhusiano uliopo kati ya nchi hizo. Pia, Vijana 5 (Wanawake 3 na Wanaume 2) wa Zanzibar wamepata fursa ya kushiriki katika Kambi kama hizo Nchini Kenya, Msumbiji na Afrika Kusini (Angalia Kiambatanisho Nam.17).

Mhe. Mwenyekiti, Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2012/2013, Idara ya Maendeleo ya Vijana itatekeleza shabaha zifuatazo ili kufikia Malengo ya Wizara:-

1. Kuratibu na kufuatilia utekelezaji wa Sera ya Maendeleo ya Vijana.
2. Kuratibu Mpango wa Mikopo kwa Vijana na kuwahamasisha kujiunga na vyama vya ushirika na mikopo.
3. Kuratibu mbio za Mwenge wa Uhuru na wiki ya Vijana.
4. Kuratibu na kufuatilia utekelezaji wa Mpango wa Stadi za Maisha kwa Vijana walio nje ya Skuli.
5. Kuratibu uanzishwaji wa Baraza la Vijana.
6. Kuimarisha mashirikiano na uhusiano wa Taasisi za Vijana ndani na nje ya Nchi.

Mhe. Mwenyekiti, Ili Idara ya Maendeleo ya Vijana iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi mwaka 2012/2013, Naliomba Baraza lako tukufu liidhinishe jumla ya Shilingi Millioni Mia moja na Sabini na Moja, Sitini na Nane Elfu (171,068,000/) kwa kazi za kawaida na Mishahara na Shilingi Milioni mia moja (100,000,000/-) kwa kazi za Maendeleo.

IDARA YA MAENDELEO YA WANAWAKE NA WATOTO

Mhe. Mwenyekiti, Idara ya Maendeleo ya Wanawake na Watoto ina jukumu la kuratibu na kusimamia utekelezaji wa haki za Wanawake na Watoto ikiwa ni pamoja na utekelezaji wa Sera, Sheria, Programu na Mikataba ya Kitaifa, Kikanda na Kimataifa.

Mhe. Mwenyekiti, katika kipindi cha mwaka 2011/2012 Idara ya Maendeleo ya Wanawake na Watoto ilijipangia kutekeleza malengo yafuatayo:

1. Kuratibu na kusimamia Haki za Wanawake na Watoto.
2. Kuratibu utekelezaji wa Sheria ya Mtoto Zanzibar ya 2011.
3. Kuhakikisha kwamba Mabaraza ya Watoto yanafanya kazi katika Wilaya zote.
4. Kuwainua Wanawake kiuchumi pamoja na kuanzisha Benki ya Wanawake.
5. Kuimarisha mashirikiano ya Kitaifa, Kikanda na Kimataifa katika kuhakikisha kuwa haki za Wanawake na Watoto zinalindwa.

Mhe. Mwenyekiti, Wizara imezindua rasmi matokeo ya Utafiti wa Udhalilishaji wa Watoto (*VAC*) Mwezi Septemba, 2011 ambapo wadau kutoka Sekta ya Afya, Elimu, Ustawi wa Jamii, Polisi na Asasi za Kiraia walichukua dhamana ya kupambana na vitendo vya udhalilishaji wa Watoto kupitia Taasisi zao. Shughuli hiyo ilitanguliwa na Warsha ya waandishi wa habari kwa lengo la kuyafikisha matokeo hayo kwa jamii kupitia vyombo vya habari.

Mhe. Mwenyekiti, Wizara inaendelea na kazi yake ya kuyapokea na kuyafanyia kazi malalamiko yanayowahusu Wanawake, yanayoletwa Wizarani na Ofisi za Wilaya na Mikoa. Katika kipindi cha mwaka mmoja uliopita, jumla ya malalamiko 132 ya Wanawake yalipokelewa na kupatiwa ushauri na maelekezo yanayofaa Unguja na Pemba. Malalamiko hayo yalihusu; kutelekezwa, mgawanyo wa mali, mimba nje ya ndoa, kupigwa, shambulio la vitisho, shambulio la matusi na kukashifiwa (Angalia Kiambatanisho Nam. 18).

Mhe. Mwenyekiti, Wizara imeandaa taarifa ya utekelezaji wa Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Mtoto (*CRC*) ya kipindi cha miaka minne 2008-2012. Taarifa hiyo imejumuishwa na ile ya Tanzania Bara kuifanya taarifa moja ya kitaifa na kuwasilishwa Umoja wa Mataifa mwezi Januari, 2012.

Aidha, Wizara imefanya mikutano mitatu ya Kamati Maalum ya Baraza la Mapinduzi kufuatilia na kujadili ukubwa wa tatizo la udhalilishaji wa Watoto imefanyika. Kamati imepitia tafiti na taarifa zinazohusu udhalilishaji wa Watoto kwa lengo la kulishauri na kupendekeza kwa Baraza la Mapinduzi kuchukua hatua muafaka za kushughulikia suala hilo. Miongoni mwa mapendekezo yaliyotolewa ni kufanyika kwa utafiti utakaoonyesha ukubwa wat atizo kwa Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, Wizara imekamilisha utengenezaji wa Rasimu ya awali ya Mpango Kazi wa Utekelezaji wa Sheria ya Mtoto Zanzibar, Mpango Kazi huo ulijadiliwa na wadau kwa ajili ya kuimarishwa. Aidha, Wizara imeendelea kushajihisha uanzishwaji wa Mabaraza ya Watoto Unguja na Pemba na kutoa mafunzo kwa Viongozi wa mabaraza. Jumla ya Mabaraza 51 yameanzishwa (Unguja 20 na Pemba 31). Lengo la kuanzishwa kwa Mabaraza hayo ni kuwawezesha Watoto kuwa na chombo chao cha kusimamia masuala yao, kujiamini na kutambua haki zao.

Mhe. Mwenyekiti, Wizara imetembelea vikundi 189 Unguja na Pemba vya uzalishaji mali na kutathmini mahitaji, maendeleo na changamoto zinazowakabili katika uendeshaji ili kuyatafutia ufumbuzi. (Angalia Kiambatanisho Nam. 19).

Aidha, Wizara imetoa ushauri na maelekezo kwa *SACCOS* 11; Meli nne, Mwanakwerekwe, Hiari ya Moyo, Waride na Matemwe kwa Unguja; Swahiba, Konde, Tibirinzi, Mkipi Mzambarauni, Jondeni na Mkoani kwa Pemba. Lengo la ziara hizo ni kuzihamasisha *SACCOS* za Wanawake na kuziimarisha ili ziwe msingi wa kuanzisha Benki ya Wanawake Zanzibar. Pia, Wizara imewawezesha Wajasiriamali 6 kushiriki katika maonyesho ya nchi za Afrika Mashariki yaliyofanyika Kigali Rwanda mwezi Agosti, 2011 na vikundi 54 (42 kutoka Unguja na 12 kutoka Pemba) vilishiriki katika maonesho ya 35 ya Sabasaba Dar-es-Salaam.

Mhe. Mwenyekiti, Wizara ilifanya ziara katika taasisi za kifedha na *SACCOS* ili kupata uzoefu juu ya kuendesha mchakato wa uanzishwaji wa Benki ya Wanawake. Hadi hivi sasa tayari Mtaalamu muelekezi kwa ajili ya kufanya tathmini ya uanzishaji wa Benki hiyo ameshapatikana na ameanza kazi katika hatua za awali.

Mhe. Mwenyekiti, Tarehe 8 Machi ya kila Mwaka Nchi yetu huungana na Nchi nyengine duniani kwa kuadhimisha siku ya wanawake Duniani ambapo kwa mwaka huu ujumbe wa Maadhimisho hayo ulikuwa ni “ONDOA UKATILI DHIDI YA WANAWAKE TANZANIA. Kwa upande wa Zanzibar Maadhimisho hayo yalifanyika katika Wilaya Kusini, Mkoa Kusini Unguja na Wilaya ya Wete Mkoa wa Kaskazini Pemba. Katika kuadhimisha Siku 16 za

kupinga ukatili dhidi ya Wanawake, Wizara iliandaa vipindi na kuvirusha kwenye vyombo vya Habari. Wizara pia, iliadhimisha siku ya Mtoto wa Afrika tarehe 16 Juni na kusoma tarifa ya Maendeleo ya Mtoto mbele ya Baraza lako Tukufu. Ujumbe wa mwaka huu ni "HAKI ZA WATOTO WENYE ULEMAVU NI JUKUMU LETU KUZILINDA, KUZIHESHIMU, KUZIENDELEZA NA KUZITEKELEZA".

Mhe. Mwenyekiti, Wizara ilishiriki katika Mkutano wa 56 wa Kamisheni ya Hali na Hadhi ya Wanawake (*Comission on the Status of Women - CSW*) Umoja wa Mataifa mjini New York nchini Marekani. Mkutano wa Mwaka huu ulilenga katika kuwawezesha Wanawake wa Vijijini kujua wajibu wao katika kutokomeza umaskini, kuleta maendeleo pamoja na kukabiliana na changamoto zilizopo. Ripoti ya safari hiyo imeshawasilishwa katika kikao cha Baraza la Mapinduzi.

Mhe. Mwenyekiti, Kwa kipindi cha mwaka 2012/2013, Idara ya Maendeleo ya Wanawake na Watoto imepanga kutekeleza shabaha zifuatazo ili kufikia Malengo ya Wizara:

1. Kuratibu na kufuatilia utekelezaji wa Sera na Sheria Mtoto.
2. Kuimarisha mashirikiano ya Kitaifa, Kikanda na Kimataifa yanayohusu Wanawake na Watoto.
3. Kuimarisha uratibu wa masuala ya Wanawake na Watoto.
4. Kuhamasisha uanzishwaji wa Benki ya Wanawake na kuwahamasisha Wanawake katika shughuli za ujasiriamali.
5. Kukuza uelewa wa jamii katika masuala yanayohusu Watoto na Wanawake.
6. Kuratibu na kusimamia uanzishwaji wa mabaraza ya watoto katika ngazi zote.

Mhe. Mwenyekiti, Ili Idara ya Maendeleo ya Wanawake na Watoto iweze kutekeleza malengo yake kwa mwaka wa fedha 2012/2013, naliomba Baraza lako Tukufu liidhinishe kiasi cha Shilingi Milioni Mia Mbili na Ishirini na Saba, Laki Saba na Sabini na Saba Elfu, (227,777,000/) kwa kazi za kawaida na Mishahara na Shilingi Milioni Mia Tatu na ishirini (320,000,000/-) kwa kazi za Maendeleo.

OFISI KUU PEMBA

Mhe. Mwenyekiti, Ofisi kuu Pemba inasimamia shughuli zote za Wizara na kutekeleza malengo ya Idara zote yaliyojipangia kwa upande wa Pemba. Utekelezaji wa majukumu na shughuli kwa mwaka 2011/12 na malengo ya Ofisi kwa mwaka 2012/2013 tayari yameshaelezwa katika Idara husika ambazo zinahusisha na Ofisi kuu Pemba.

Mhe. Mwenyekiti, Ili Ofisi Kuu Pemba iweze kutekeleza malengo yake kwa mwaka wa fedha 2012/2013, naliomba Baraza lako Tukufu liidhinishe kiasi cha Shilingi Milioni Mia nne na Hamsini, Laki mbili na Sitini Elfu, (450,260,000/-) kwa Kazi za Kawaida na Mishahara.

MUHTASARI WA MAPATO NA MATUMIZI

Mhe. Mwenyekiti, Kwa mwaka wa fedha 2011/2012, Wizara ilifanya Makadirio ya Matumizi ya Kazi za Kawaida pamoja na Mishahara ambayo yalikuwa ni Shilingi Bilioni Moja, Milioni Mia Nane na Sita, Laki Nane na Ishirini Mia Nane na Tisini na Nane (1,806,820,898) na hadi kufikia Juni 2012, fedha zilizotolewa ni Shilingi Bilioni Moja na Milioni Mia Tano na Tisini na Nane, Laki nane na Elfu Moja, Mia Mbili Thamanini na Moja (1,598,801,281) ambayo ni sawa na asilimia 88%. Aidha, Wizara ilitengewa jumla ya Shilingi Bilioni Moja, Milioni Sabini na Mbili na Laki Mbili Hamsini Elfu (1,072,250,000) kwa Kazi za Maendeleo. Fedha zilizotolewa kwa kazi hizo mpaka kufikia Juni, 2012 ni Shilingi Milioni Mia Sita na Kumi na Tatu, Laki Nane Sabini na Sita na Tisini na Moja (613,876,091) ambazo ni sawa na asilimia 57%. (Angalia Kiambatanisho Nam. 20a na 20b).

HITIMISHO:

Mhe. Mwenyekiti, Naomba uniruhusu nitoe salamu na pongezi zetu za dhati kwa Mheshimiwa Makamo wa Kwanza wa Rais Mhe. Maalim Seif Sharif Hamad pamoja na Makamo wa Pili wa Rais Mhe. Balozi Seif Ali Iddi kwa kazi nzuri wanazozifanya za kumsaidia Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Juhudi zao za kila siku zinaonekana na zinaleta matumaini makubwa kwa Wananchi kupata maendeleo. Sote tunawaombea uzima,

afya njema, nguvu na maarifa ili waendelee kumsaidia Mhe. Dkt Shein na kuwaletea Maendeleo Wananchi wa Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, Naomba kuchukua nafasi hii kuwashukuru na kuwapongeza Wafanyakazi wote wa Wizara ya Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto kuanzia Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu, Wakurugenzi, Afisa Mdhamini na Maafisa wa ngazi zote kwa kufanya kazi nzuri, makini na juhudi kubwa zilizotuwezesha kutekeleza malengo na majukumu yetu kwa ufanisi. Aidha, nawaomba wazidishe juhudi zaidi katika kutekeleza malengo yetu ya mwaka huu na kuwaletea Maendeleo endelevu Wanawake, Watoto, Wazee na Vijana. Nataka nikiri kuwa Umoja, Mashirikiano, Upendo na Nidhamu ndio siri kubwa ya mafanikio yetu. Nawaomba tuyaendeleze.

Mhe. Mwenyekiti, Nachukua fursa hii adhimu kwa niaba ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kuzishukuru Nchi, Mashirika ya Kimataifa na Kitaifa pamoja na Taasisi mbali mbali zisizo za Kiserikali ambazo zilishirikiana na Wizara ya Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto katika kutekeleza majukumu ya Wizara na kuleta Maendeleo ya Kiuchumi na Kijamii kwa Wananchi wa Zanzibar. Nchi hizo ni kama zifuatazo; Serikali ya India, Misri, Marekani, *Uingereza na Jamhuri ya Watu wa China. Taasisi za Kimataifa ni**;*** *ILO, UNDP, UNFPA, UNICEF, SAVE THE CHILDREN, FHI*, Tunajali Program, *CHAI, UNESCO, ADB*, DFID, Benki ya Dunia, Umoja wa Ulaya, Jumuiya ya Afrika ya Mashariki, na Jumuiya ya Madola.

Taasisi za Kitaifa ni; *ZAYADESA, BOT, PBZ, ZACA, ZAIADA, ZAWDO, ZAFELA, ZAWCO, ZAMWASO, ZANGOC, ZLSC, COWPZ, PIRO, UVIKIUTA, WEDTF, TAWLA, TAMWA, CHANGAMOTO, PRIDE, TMC, TGNP, UWT, CRDB, AKIBA BANK, ACTION AID na POSTAL BAN*K.

Mhe. Mwenyekiti, Naomba kuchukua nafasi hii kuvishukuru vyombo vya habari ikiwemo Televisheni, Redio na Magazeti ambavyo vimetoa mchango mkubwa katika kuhamasisha na kuelimisha jamii juu ya masuala mbalimbali yanayotekelezwa na Wizara.

Kabla sijamaliza Hotuba yangu naomba nikushukuru Mhe. Spika kwa kunipa nafasi hii adhimu. Aidha, nikupongeze kwa dhati kwa jinsi unavyoliendesha Baraza lako Tukufu. Ni matumaini yetu kwamba chini ya Uongozi wako tutaendelea kupata mafaniko makubwa.

Mhe. Mwenyekiti, Kwa heshima na taadhima nawaomba Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako Tukufu Wapokee, Wajadili, Watupe ushauri na Maelekezo, hatimae kupitisha Makadirio na kuidhinisha jumla ya Shilingi Bilioni Mbili na Milioni Mia Nne na Tisa (2,409,000,000/=) ikiwa ni fedha za Kazi za kawaida na Mishahara na Shilingi Bilioni Moja, Milioni Mia Sita na Sita na Laki Sita (1,606,600,000/=) zikiwa ni fedha za kazi za Maendeleo kwa kipindi cha mwaka 2012/2013. (Angalia Kiambatanisho Nam. 21).

Mhe. Mwenyekiti, Naomba kutoa hoja.

VIAMBATANISHO

Kiambatanisho Nambari 1

AGENDA ZA TAFITI ZILIZOIBULIWA NA WIZARA KWA MWAKA 2011/2012

S/N	AGENDA ZA TAFITI ZILIZOIBULIWA
1.	Mambo yanayochangia kiwango cha juu ya talaka na athari zinazohusiana nazo.
2.	Mambo yanayochangia ukosefu wa ajira kwa vijana katika sekta rasmi na isiyo rasmi Zanzibar.
3.	Utafiti juu ya uelewa, matendo, mtazamo na tabia katika kukuza fursa na usawa wa kijinsia na uwezeshaji wa Wanawake (utafiti pia utalenga masuala ya uratibu na mitandao).
4.	Tathmini juu ya fursa na changamoto zinazowakabili Wanawake na Vijana katika kuwawezesha kiuchumi.
5.	Uchambuzi wa hali halisi ya Wanawake Zanzibar.
6.	Uchambuzi wa hali halisi ya Maendeleo ya awali ya Watoto Zanzibar
7.	Utafiti juu ya kuongezeka kwa idadi ya omba omba Zanzibar.
8.	Tathmini juu ya ushiriki wa Vijana katika vyombo vya maamuzi.
9.	Mambo yanayoathiri maendeleo (Kwa maeneo ya mipango, miundo, mifumo na taratibu) katika kushughulikia unyanyasaji wa kijinsia na udhalilishaji wa Watoto.

Kiambatanisho Nambari 2a

AJIRA MPYA NA UHAMISHO 2011/2012 UNGUJA NA PEMBA

PAHALI	**UNGUJA**			**PEMBA**			**JUMLA KUU**		
JINSI	**WKE**	**WME**	**JUMLA**	**WKE**	**WME**	**JUMLA**	**WKE**	**WME**	**JUMLA**
AJIRA MPYA	01	03	04	01	0	01	02	03	**05**
AJIRA KWA NJIA YA UHAMISHO	02	02	04	01	02	03	03	04	**07**
JUMLA KUU	**03**	**05**	**08**	**02**	**02**	**04**	**05**	**07**	**12**

Kiambatanisho Nambari 2b.

WAFANYAKAZI WALIOONDOKA WIZARANI KWA NJIA MBALIMBALI 2011/2012

AINA YA UTOKAJI	UNGUJA			PEMBA			JUMLA KUU		
JINSI	**WKE**	**WME**	**J**	**WKE**	**WME**	**JUMLA**	**WKE**	**WME**	**JUMLA**
UHAMISHO	1	2	3	1	0	1	2	2	**4**
KUSTAAFU	1	2	3	2	0	2	3	2	**5**
KUFARIKI	0	1	1	0	0	0	0	1	**1**
KUACHA KAZI	0	1	1	0	0	0	0	1	**1**
JUMLA KUU	**2**	**6**	**8**	**3**	**0**	**3**	**5**	**6**	**11**

Kiambatanisho Nambari 3

MAFUNZO YA MUDA MREFU NA MFUPI KWA WAFANYAKAZI MWAKA 2011/2012

AINA YA MAFUNZO	UNGUJA			PEMBA			JUMLA KUU		
	WKE	**WME**	**JUMLA**	**WKE**	**WME**	**JUMLA**	**WKE**	**WME**	**JUMLA KUU**
MUDA MREFU	2	4	6	6	2	8	8	6	**14**
MUDA MFUPI	4	0	4	0	1	1	4	1	**5**
JUMLA	**6**	**4**	**10**	**6**	**3**	**9**	**12**	**5**	**19**

Kiambatanisho Nambari 4a

FAMILIA ZINAZOISHI KATIKA MAZINGIRA MAGUMU ZILIZOPATIWA MSAADA KWA MWAKA 2011/2012 UNGUJA

MWEZI	MAPACHA	MAISHA	MAYATIMA	JUMLA	GHARAMA
JULAI	4	31	18	53	795,000
AGOSTI	3	31	18	52	780,000
SEPTEMBA	3	31	18	52	780,000
OKTOBA	3	31	18	52	780,000
NOVEMBA	3	33	19	55	825,000
DISEMBA	2	33	21	56	840,000
JANUARI	2	33	21	56	840,000
FEBRUARI	3	33	21	57	855,000
MACHI	4	36	21	61	915,000
APRIL	4	36	21	61	915,000
MEI	4	36	22	62	930,000
JUNI	2	36	24	62	930,000
JUMLA					**10,185,000**

Kiambatanisho Nambari 4b

FAMILIA ZINAZOISHI KATIKA MAZINGIRA MAGUMU ZILIZOPATIWA MSAADA KWA MWAKA 2011/2012 PEMBA

MWEZI	MAPACHA	MAISHA	MAYATIMA	JUMLA	GHARAMA
JULAI	3	38	-	41	820,000
AGOSTI	3	38	-	41	820,000
SEPTEMBA	3	39	-	42	840,000
OKTOBA	3	39	-	42	840,000
NOVEMBA	3	40	-	43	860,000
DISEMBA	3	42	-	45	900,000
JANUARI	3	42	-	45	900,000
FEBRUARI	3	42	-	45	900,000
MACHI	3	42	-	45	900,000
APRIL	3	42	-	45	900,000
MEI	3	42	-	45	900,000
JUNI	3	42	-	45	900,000
JUMLA	**3**	**42**		**45**	**10,480,000**

Kiambatanisho Nambari 5

SHEHIA ZILIZOPATIWA MSAADA WA SARE ZA SKULI KWA MWAKA 2011/2012 UNGUJA

SHEHIA	WANAWAKE	WANAUME	JUMLA
KINUNI	15	15	30
PANGAWE	5	5	10
MAUNGANI	5	5	10
JUMLA	**25**	**25**	**50**

Kiambatanisho Nambari 6

MSAADA WA CHAKULA KWA FAMILIA ZINAZOISHI KATIKA MAZINGIRA MAGUMU UNGUJA NA PEMBA KWA MWAKA 2011/2012

PAHALI	SHEHIA	IDADI YA WATOTO WALIOSAIDIWA		
		ME	KE	JUMLA
UNGUJA	KIJITOUPELE	58	61	119
	MTOPEPO	79	76	155
	JUMLA:	**137**	**137**	**274**
PEMBA	MWAMBE	56	70	126
	JOMBWE	61	76	137
	SHENGEJUU	69	56	125
	JUMLA:	**186**	**202**	**388**

Kiambatanisho Nambari 7

WAFANYAKAZI WALIOPATA FIDIA UNGUJA NA PEMBA KWA MWAKA 2011/2012

SEHEMU	KESI ZILIZO RIPOTIWA	THAMANI YA KESI ZILIZO RIPOTIWA	FEDHA ZILIZO FIDIWA	KESI ZILIZO BAKIA	THAMANI ZILIZOBAK
UNGUJA	22	5,680,941/-	4,000,000/-	59	33,608,947/-.
PEMBA	12	22,963,050/-	8,700,000/-	23	55,730,849/-
JUMLA	**34**	**28,643,991/-**	**12,700,000/-**	**82**	**89,339,796/-**

Kiambatanisho Nambari 8

MALALAMIKO YA UDHALILISHAJI WATOTO UNGUJA NA PEMBA KWA MWAKA 2011/2012.

WILAYA	AINA YA UDHALILISHAJI							JUMLA
	KUBAKWA	UJAUZITO	KULAWITIWA	MVUTANO WA MALEZI	KIMWILI	KUKASHIFIWA	UTELEKEZWAJI	
MJINI	9	-	2	-	1	-	-	**12**
MAGHARIBI	20	3	2	-	2	2	-	**29**
KASKAZINI A	3	2	2	-	-	-	-	**7**
KASKAZINI B	1	-	-	-	-	-	-	**1**
KATI	4	1	1	-	-	-	-	**6**
MKOANI	1	1	-	1	-	-	9	**12**
CHAKECHAKE	17	2	5	7	-	-	56	**87**
WETE	12	-	5	1	-	-	21	**39**
MICHEWENI	14	-	4	-	-	-	2	**20**
KUSINI	2	-	-	-	-	-	-	**2**
JUMLA	**83**	**9**	**21**	**9**	**3**	**2**	**88**	**215**

Kiambatanisho Nambari 9

KESI ZA UDHALILISHAJI WATOTO ZILIZOPOKELEWA ONE STOP CENTRE UNGUJA KWA MWAKA 2011/2012

AINA YA UDHALILISHAJI	**WANA UME**	**WANA WAKE**	**JUMLA**
KUBAKWA	0	287	287
UJAUZITO	0	82	82
KULAWITIWA	61	0	61
KUKASHIFIWA	4	247	251
JUMLA	**62**	**627**	**689**

Kiambatanisho Nambari 10

MALALAMIKO YA MATUNZO YA WATOTO UNGUJA NA PEMBA KWA MWAKA 2011/2012

YALIYORIPOTIWA	**YALIYOPATIWA UFUMBUZI**	**YANAYOENDELEA KUSHUGHULIKIWA**	**YALIYOSHINDIKANA NA KUELEKEZWA MAHAKAMANI**	**JUMLA**
KUGOMBANIA WATOTO	64	14	24	**102**
KUKOSA MATUNZO	198	25	68	**291**
JUMLA	**262**	**39**	**92**	**393**

Kiambatanisho Nambari 11

UKAGUZI WA VITUO VYA KULELEA WATOTO UNGUJA NA PEMBA KWA MWAKA 2011/2012

SN	**JINA LA KITUO**	**PAHALA KILIPO NA WILAYA**	**IDADI**		
			KE	**ME**	**JUMLA**
01	NYUMBA YA KULELEA WATOTO MAZIZIINI	MAZIZINI, WILAYA YA MJINI	24	24	48
02	SOS	MOMBASA, WILAYA YA MAGHARIBI	55	93	148
03	OMAR BIN AL-KHATWAB	FUMBA, WILAYA YA MAGHARIBI	00	60	60
04	FYSABILILLAH TABLIGH MARKAZ	FUONI, WILAYA YA MAGHARIBI	09	09	18

05	ONAIZA ORPHANAGE HOUSE	MWANAKWEREKWE, WILAYA YA MAGHARIBI	00	62	62
06	ST. MONTESOORY	BUBUBU, WILAYA YA MAGHARIBI	12	08	20
07	AL-MAZRUI ORPHANAGE HOUSE	MAZIZINI, WILAYA YA MJINI	00	16	16
08	PEFA – REHEMA HOME	MTONDOONI, WILAYA YA MAGHARIBI	05	03	08
09	ISTIQAMA	WILAYA YA CHAKE CHAKE	00	24	24
10	AFRICAN MUSLIM AGENCY	MABAONI - WILAYA YA CHAKE CHAKE	00	114	114
11	ALFANURANIA	PUJINI – WILAYA YA CHAKE CHAKE	12	10	22
12	MADRASAT AL FAROUQ	MAGOME – WILAYA YA CHAKE CHAKE	00	32	32
13	MADRASAT AL ULUMI	MAGOME – WILAYA YA CHAKE CHAKE	28	00	28
JUMLA			**145**	**455**	**600**

Kiambatanisho Nambari 12a

MIRADI ILIYOZINDULIWA NA KUWEKEWA MAWE YA MSINGI KUPITIA MBIO ZA MWENGE WA UHURU UNGUJA NA PEMBA 2011/2012

MKOA	**JINA LA MRADI**	**MAHALA ULIPO**
KASKAZINI- PEMBA	Kuweka jiwe la Msingi chinjio	Msitu Jangwani Micheweni
	Tangi la Maji	Gongoni
	Jiwe la Msingi	Skuli ya Micheweni
	Jiwe la Msingi	Skuli ya Tumbe Sekondari
	Kutembelea SACCOS ya Muambe	Shehia ya Bopwe Wete
	Kutembelea Ofisi ya Wasioona	Jamhuri Hall Wete
	Mpiki Miliki Jiwe la Msingi	Machengwe
	Upandaji Miti ya Misitu	JKU – Msaani
Thamani ya Mradi hiyo Tshs. 502,919,000/=		
MKOA	**JINA LA MRADI**	**MAHALA ULIPO**
KUSINI - PEMBA	Jiwe la Msingi Kinu cha Nafaka	Ngwachani
	Jiwe la Msingi	Skuli ya Mtambile
	Kutoa Mikopo kwa kikundi cha SACCOS	Skuli ya Mtambile
	Jiwe la Msingi kisima cha Maji Safi na umwagiliaji Mashamba	Gae la Mtungi
	Uzinduzi wa kikundi cha Vijana cha kuhifadhi Mazingira	Kituo cha Afya Chonga
	Uzinduzi wa Barabara ya ndugu kitu	Machomane
	Uzinduzi wa Kisanduku cha malalamiko ya Rushwa	Wawi Halmashauri
	Uzinduzi wa kikundi cha Vijana cha uhifadhi wa Mazingira	Vikunguni
	Jiwe la Msingi Mradi wa Nyumba bora	Mbuzini
	Uzinduzi wa Matone ya Vitamin A	Kituo cha Afya Mbuzini

	Kukagua Vijana waliacha Utumiaji wa Dawa za Kulevya (SOBERHOUSE)	Kituo cha Afya Mbuzini
	Kukagua shughuli za ushauri nasaha na Upimaji wa VVU kwa hiari	Gombani
Thamani ya Mradi hiyo Tshs 237,210,000/=		
MKOA	**JINA LA MRADI**	**MAHALA ULIPO**
MJINI MAGHARIBI	kukagua Vijana waliacha Dawa za kulevya (SOBER HOUSE)	Tomondo
	Kukagua Vikundi vya Ushirika	Mwanakwerekwe
	Uwekaji Jiwe la Msingi Skuli ya Hifadhi	Mwnakwerekwe
	Kukagua Ushirika wa Juwapo/Juwafu	Fuoni
	Upandaji Miti	Skuli ya Jang'ombe Msingi
	Kuzindua kisima cha Maji Safi na Salama	Kwahani
	Kukagua shughuli za mapambano ya VVU na Upimaji wa hiari	Skuli ya Msingi Muungano
Thamani ya Mradi hiyo Tshs.		
MKOA	**JINA LA MRADI**	**MAHALA ULIPO**
KUSINI - UNGUJA	Kuweka jiwe la msingi mkulima SACCOS	Mchangani
	Jiwe la msingi Jengo la usanifi wa maziwa	Mpapa
	Kukabidhi vifaa jengo la kiwanda cha Usarifu wa matunda	Chwaka
	Jiwe la Msingi Skuli ya Muungoni	Muungoni
	Ujenzi wa Tangi la Maji	Kizimkazi Mkunguni
	Uzinduzi wa Barabara	Mzuri Makunduchi
Thamani ya Miradi hiyo ni Tshs.95,693,750/=		
MKOA	**JINA LA MRADI**	**MAHALA ULIPO**
KASKAZINI UNGUJA	Kukagua Mradi wa Maji safi	Makoba
	Skuli ya Msingi Mfuru Matonga	Matemwe
	Ujenzi wa Hospitali	Kivunge
	Kutoa Vyandarua kwa mama wajawazito	Shehia ya Mbaleni
	Ujenzi wa Soko	Shehia ya Mkataleni
	Mafunzo kuhusu Rushwa	Shehia ya Kitope
	Mdahalo miaka 50 uhuru wa Tanganyika	Misufini
Thamani ya Miradi hiyo ni Tshs.62,920,931/=		

Kiambatanisho Nambari 12b

FEDHA ZILIZOCHANGWA KUPITIA MBIO ZA MWENGE WA UHURU UNGUJA NA PEMBA MWAKA 2011/2012

MKOA	**FEDHA ZILIZOCHANGWA**
Kusini Unguja	4,892,000/=
Kaskazini Unguja	9,606,000/=
Kaskazini Pemba	5,598,000/=
Kusini Pemba	11,630,000/=
Mjini/Magharibi	6,500,000/=
JUMLA	**38,226,700/=**

Kiambatanisho Nambari 13

VIKUNDI VYA VIJANA VILIVYOPATA RUZUKU KUPITIA MFUKO WA UN HABITAT MWAKA 2011/2012

S/N	JINA LA KIKUNDI	PAHALA	KIASI CHA FEDHA (US $)
1.	ZASEA	MPENDAE	12,000
2.	Mpiki Miliki Company ltd	MACHENGWE - WETE	12,000
3.	MLAEE	MATEMWE	20,000
4.	LDS	PANDANI - PEMBA	10,000
5.	Selem Women Centre	WETE - SELEM	16,000
6.	Mshikamano youth Centre	CHAKE CHAKE - MBUZINI	15,000
JUMLA KUU:			**85,000**

Kiambatanisho Nambari 14

VIKUNDI VILIVYOPATIWA MAFUNZO YA UENDESHAJI MIRADI UNGUJA NA PEMBA 2011/2012

S/N	JINA LA KIKUNDI	MAHALA KILIPO
1.	Selem Women Centre	Wete Pemba
2.	ZASEA(Zanzibar Scrapes and Environment Association	Mpendae
3.	Mpiki Miliki Company Limited (Mpiki)	Machengwe Wete
4.	Matemwe control Aids, Education and Environment (MCAEE)	Matemwe.
5.	Lions of Development Cooerative Society (LDCS)	Pandani Wete
6.	Mshikamano Youth Centre (MYC)	Mbuzini Pemba
7.	Good Hope	Mlandege
8.	ZECOSAC	Saateni
9.	Sedo	Chumbuni

Kiambatanisho Nambari 15

VIKUNDI VYA VIJANA VILIVYO TEMBELEWA KWA MWAKA 2011/2012 UNGUJA NA PEMBA

S/N	JINA LA KIKUNDI	SHUGHULI	WILAYA
1.	MOTOMOTO	UVUVI	KUSINI
2.	INSHAALLAH METAL WORKS		MJINI
3.	LETU MOJA	BIASHARA NDOGO NDOGO	“
4.	SISI KWA SISI	BIASHARA NDOGO NDOGO	“
	UMOJA NI NGUVU	BIASHARA NDOGO NDOGO	“
5.	TUSHIKAMANE	BIASHARA NDOGO NDOGO	“
6.	POLEPOLE NDIO MWENDO	UCHONGAJI	“
7.	TUAMINIANE	BIASHARA YA DAGAA	“
8.	UKOMBOZI GROUP	KUHIFADHI MAZINGIRA	“
9.	JUMUIYA YA MAENDELEO	KILIMO CHA MBOGA MBOGA	“
10.	TUPENDANE/KOMBENI SASA	KILIMO CHA MBOGA MBOGA	MAGHARIBI

11.	SAFCO	BIASHARA NDOGO NDOGO	“
12.	CHEMUCHEMU BEKARY	BIASHARA YA MIKATE	“
13.	UWEZENI GROUP	BIASHARA YA VIFAA VYA KUANDIKIA	“
14.	NURU DAU	UVUVI NA KUTENGENEZA BOTI	KASKAZINI
15.	BAHARI HAIKAUKI	UVUVI NA KILIMO CHA MBOGA MBOGA	KASKAZINI
16.	JUMUIYA YA KUHIFADHI MAZINGIRA NA UFUGAJI WA NYUKI (JUKUNUM)	UFUGAJI WA NYUKI NA UHIFADHI WA MAZINGIRA	CHAKE CHAKE
17.	MKOROSHONI TAILORING CENTER	USHONAJI WA NGUO ZA KIKE KILIMO	“
18.	PEACE AND HOPE	KILIMO CHA MIGOMBA NA MIHOGO	“
19.	MTAJI WA MASKANI	KILIMO CHA MBOGA MBOGA MBOGA	“
20.	KIJILI COOPERATIVE SOCIETY	KILIMO CHA MIVINJE, MIGOMBA, MIBUYU NA MAHINDI	“
21.	KUMBUKA WAJIBU WAKO	NGO’MBE WA MAZIWA	“
22.	MSHIKAMANO YOUTH CENTER	USHONAJI NA UCHONGAJI	“
23.	SI VIBAYA	UCHONGAJI	“
24.	YOUTH INTERFAITH DIALOGUE	KUTOA ELIMU YA UKIMWI, MADAWA YA KULEVYA NA KUWAUNGANISHA VIJANA	“
25.	MKIZANI	KILIMO CHA MIGOMBA	“
26.	VIJANA ALEO	KILIMO NA UFUGAJI	“
27.	JIIMARISHE	UFUGAJI WA KUKU WA MAYAI	“
28.	MJA HAKOSI RIZIKI	UFUGAJI NA KILIMO	“
29.	RIZIKI ZINA MOLA	KILIMO NA UFUGAJI	“
30.	PEMBA SEA FOOD PROCESS	UKAUSHAJI WA MADAGAA	“
31.	NIA SAFI	USHONAJI NA BIASHARA NDOGO NDOGO.	“
32.	NA SI NDIO	UFUGAJI WA KUKU WA KIENYEJI	“
33.	MAKUBADHI	UTENGENEZAJI WA VIATU VYA MAKUBADHI	“
34.	VIJANA SACCOS	KUWEKA NA KUKOPA	“
35.	KIBOKONI POULTRY CO-OPERATIVE	UFUGAJI WA KUKU WA MAYAI	“
36.	NDUGU NJOONI SACCOS	KUWEKA NA KUKOPA	“
37.	MAMBO CO-OPERATIVE SOCIETY	UCHONGAJI	“
38.	CHONGA YOUTH	KILIMO, USHONAJI NA MAIIGIZO	“
39.	UKIONA VYAELEA	UVUVI.	“
40.	SUBIRA NI MALI	UFUGAJI WA KUKU WA KIENYEJI, NG’OMBE NA KILIMO CHA MBOGA MBOGA	MKOANI
41.	KITANDU	KILIMO CHA MBOGA MBOGA	“
42.	BORA UTU	UFUGAJI WA MBUZI, NYUKI NA KILIMO CHA MIHOGO NA MIGOMBA	“

43.	BORA HIARI	UFUGAJI NA KILIMO	“
44.	UDUGU NI KOVU	UCHONGAJI WA MADIRISHA NA UPASUAJI WA MBAO	“
45.	MTAKAA YOUTH	KILIMO, UFUGAJI AWA KUKU NA NG’OMBE NA UTUNZAJI WA MAZINGIRA	“
46.	NILEKIPI	UTENGENEZAJI WA CHUMVI, UFUGAJI WA SAMAKI NA UPANDAJI MITI KWA AJILI YA KUHIFADHI MAZINGIRA	“
47.	JAALA COOPERATIVE SOCIETY	UVUVI WA BAHARI KUU	“
48.	SIHILIBIKI	UVUVI NA UFUGAJI WA SAMAKI KATIKA BWAWA LA KIMAUMBILE	“
49.	YAMUNGU MENGI	KILIMO CHA MIGOMBA	“
50.	JUHUDI NI UWEZO	UFUGAJI WA NYUKI PAMOJA NA KILIMO CHA MATUNDA NA MBOGA MBOGA	“
51.	TAJIRIKA	UUNDAJI WA VITU VYA VYUMA	“
52.	KISIMA MCHELE CO-OPERATIVE	UCHONGAJI	“
53.	BADURU CO-OPERATIVE	KILIMO	“
54.	CHOLE NASI WAZALENDO	UFUGAJI	“
55.	CHOTARA	UFUGAJI	“
56.	JIENDELEZENI CO-OPERATIVE	UFUGAJI	“
57.	SANAA GROUP	KILIMO NA KUTOA ELIMU JUU YA UKIMWI	“
58.	TUNAWEZANA CO-OPERATIVE	UVUVI	“
59.	UKWELI CO-OPAERATIVAE	KILIMO	“
60.	NA SIE TUPATE	KILIMO	“
61.	KWA DAWA CO-OPERATIVE	KILIMO	“
62.	WEMA	UTENGENEZAJI WA SIAGI, MTINDI NA MAZIWA.	WETE
63.	PEMBA HYGENIC	KILIMO CHA VIUNGO NA MATUNDA	“
64.	MISTO WORK SHOP	UTENGENEZAJI WA MAGETI. MADIRISHA, MILANGO NA MAGARI	“
65.	MDOGO GEREJI	UTENGENEZAJI WA VESPA, PIKIPIKI NA MASHINE ZA BOTI	“
66.	PEMBA CLOVE HONEY	UFUGAJI WA NYUKI KWA AJILI YA KUTENGENEZA ASALI	“
67.	KILA ALIAE	UFUGAJI WA KUKU NA KILIMO CHA MBOGA MBOGA	“
68.	VIJANA MBELE	KUTOA ELIMU YA KUENDELEZA VIJANA	“
69.	MTANI GEREJI	UTENGENEZAJI WA BAISKELI	“
70.	MTEMANI WORK SHOP	UTENGENEZAJI WA MAGARI	“
71.	LION DEVELOPMENT	UFUGAJI WA KUKU WA MAYAI	“
72.	SELEMU WOMEN CENTRE	USHONAJI NA UFUGAJI	“
73.	MKIPI MILIKI	UTENGENEZAJI WA SABUNI	“

74.	WEZA	KILIMO NA UFUGAJI	“
75.	JUMUIA YA MAENDELEO KAMBINI	KUTOA ELIMU YA UJASIRI AMALI, UTAMADUNI, AFYA, UKIMWI NA UHIFADHIJI WA MAZINGIRA	“
76.	TUNDWA CO-OPERATIVE SOCIETY	UFUGAJI WA KUKU NA KILIMO CHA MIGOMBA.	“
77.	NGUVU HAZIKOPWI	UTENGENEZAJI WA VESPA NA PIKI PIKI.	“
78.	TUTAWEZANA	USHONAJI NA UFUMAJI	“
79.	ULIZENI CO-OPERATIVE SOCIETY	KILIMO CHA MBOGA MBOGA	“
80.	HALIFICHIKI	UVUVI	“
81.	PADEP	UKOBOAJI NA USAGAJI WA MAHINDI NA MPUNGA	“
82.	WALEMAVU NAO NI WATU	USHONAJI NA KUTOA MAFUNZO YA USHONAJI	“
83.	COBEKA	UFUGAJI WA NYUKI NA UTUNZAJI WA MAZINGIRA	“
84.	KICHAKAA SI SHANGI	UFUGAJI WA SAMAKI NA UTENGENEZAJI WA CHUMVI	“
85.	NIA NJEMA	UFUGAJI WA KUKU NA KILIMO CHA MBOGA MBOGA	“
86.	KUPATA SIKUWANA	KILIMO CHA MIGOMBA NA MIHOGO	“
87.	KIVUNIE	KILIMO CHA MBOGA MBOGA NA MAUA.	“
88.	TUSHIKAMANE	KILIMO CHA MBOGA MBOGA	“
89.	TUMEAMUA	KILIMO CHA MBOGA MBOGA.	“
90.	CHWALE CO-OPERATIVE	KILIMO NA UVUVI	“
91.	HABA NA HABA	UATIKAJI WA MICHE YA MIKARAFUU NA MATUNDA	“
92.	WEMA CO-OPERATIVE SOCIETY	KILIMO CHA MBOGA MBOGA	“
93.	KUPATA SI KUWANA	KILIMO CHA MIGOMBA	“
94.	MSAWASE SACCOS	KUWEKA NA KUKOPA	“
95.	MLEZI SACCOS	KUWEKA NA KUKOPA	“
96.	JIPE MOYOCO-OPERATIVE	KUWEKA NA KUKOPA	“
97.	MUGETA GROUP	UFUGAJI WA KUKU NA UTENGENEZAJI MIKUNGU, MAKARAI NA VYUMA VYA MIKATE	MICHEWENI
98.	HIRIMU NIFASI	UCHONGAJI WA MAGETI	“
99.	TUSHIRIKIANE	UFUGAJI WA KUKU	“
100.	JITIHADA	UFUGAJI WA NG’OMBE WA MAZIWA NA KILIMO	“
101.	WIVU NI KUONA	KILIMO CHA MBOGA MBOGA	“
102.	JIENDELEZE A	UCHONGAJI NA KILIMO CHA MIGOMBA	“
103.	KWA MOGA	UFUGAJI WA KAA NA UHIFADHI WA MAZINGIRA	“
104.	YARABI SALAMA	UVUVI NA UPANDAJI WA MITI YA MIKOKO	“
105.	AWEZAE	KILIMO CHA MIVINJE NA	“

		MIGOMBA	
106.	COJIFA	KILIMO CHA MINANASI	“
107.	SARAKASI	UBANJAJI WA KOKOTO NA UFUGAJI WA KUKU	“
108.	UMOJA NA MSHIKAMANO	KILIMO NA UFUGAJI	“
109.	KIDUTANI CO-OPERATIVE	KILIMO CHA MIVINJE NA UFUGAJI AWA MBUZI WA KIENYEJI	“
110.	TAKASA	UTENGENEZAJI WA SABUNI	“
111.	MWENDA POLE CO-OPERATIVE	UFUGAJI WA KUKU WA KIENYEJI	“
112.	BAADA YA DHIKI	UFUGAJI WA MBUZI	“
113.	KICHAKA CO-OPERATIVE	UFUGAJI WA KUKU	“
114.	JAMBO NIA	KILIMO CHA MWANI NA UFUGAJI WA KUKU	

Kiambatanisho Nambari 16

VIKUNDI VILIVYOPATIWA MAFUNZO KUPITIA PEMBA MILLENIUM CHALLENGE ACCOUNT TANZANIA (MCTA).

S/N	**JINA LA KIKUNDI:**	**MAHALA KILIPO**
WILAYA YA WETE		
1.	Kutoa ni moyo	Pandani
2.	Mwanzo mgumu	Mpambani
3.	Pemba Hygienic Fruit and Spices	Bwagamoyo
4.	Maskini hachoki	Kinazini
5.	Jali wakati	Nyali
6.	Azimio	M/Ole
WILAYA YA MICHEWENI		
1.	Tubadilike kiuchumi	Kinyasini
2.	Mapofu Co-operative Society	Mapofu

Kiambatanisho Nambari 17

NCHI ZILIZOSHIRIKI KAMBI ZA KIMATAIFA ZA VIJANA UNGUJA NA PEMBA KWA MWAKA 2011/2012

S/N	NCHI	WANAWAKE	WANAUME	JUMLA KUU
1.	Korea Kusini	5	3	8
2.	Spain	4	10	14
3.	Mexico	4	2	6
4.	USA	3	2	5
5.	Ufaransa	4	4	8
6.	Belgium	4	2	6
7.	Denkark	4	5	9
8.	Italy	3	2	5
9.	Nertherland	3	1	4
10.	Ireland	2	2	4
11.	Switzerland	4	2	6
12.	Greece	4	7	11
13.	Russia	6	3	9
14.	UK	4	4	8
15.	Canada	10	4	14
16.	China	4	4	8
17.	Kenya	18	22	40
18	Tanzania	35	22	57
	JUMLA	**120**	**101**	**221**

Kiambatanisho Nambari 18

MALALAMIKO YA WANAWAKE YALIYOWASILISHWA WIZARANI KWA MWAKA 2011/2012 UNGUJA.

WILAYA	KUTELEKEZWA	UDHALILISHWAJI	KUBAKWA	MADAI	HUDUMA YA MAKAZI	MGAWANYO WA MALI	MIMBA NJE YA NDOA	MIGOGORO NDANI YA NDOA	KUPIGWA	SHAMBULIO LA VITISHO	SHAMBULIO LA MATUSI	KUKASHIFU	JUMLA
MAGHARIBI	8	-	-	-	-	7	3	11	6	-	-	-	**35**
MJINI	6	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	**6**
KASK "A"	-	-	-	-	-	-	-	-	3	-	3	1	**7**
KASK "B"	2	-	-	-	-	-	-	-	1	1	2	1	**7**
KUSINI	2	-	-	-	-	-	-	-	1	-	-	-	**3**
KATI	2	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	**2**
WETE	1	2	1	3	-	-	-	4	4	-	-	-	**15**
MICHEWENI	2	1	-	2	-	-	-	1	3	-	-	-	**9**
MKOANI	-	-	-	-	-	-	-	3		-	-	-	**3**
CHAKECHAKE	8	-	-	8	1		2	24	2	-	-	-	**45**
JUMLA	**31**	**3**	**1**	**13**	**1**	**7**	**5**	**43**	**20**	**1**	**5**	**2**	**132**

Kiambatanisho Nambari 19

VIKUNDI VYA WANAWAKE VILIVYOTEMBELEWA KWA MWAKA 2011/2012 UNGUJA NA PEMBA.

WILAYA YA MAGHARIBI:

S/N.	JINA LA KIKUNDI	PAHALA	SHUGHULI
1	TUWE MACHO	DOLE	UFUMAJI
2	DOLE IWE IMARA	DOLE	UFUGAJI KUKU
3	KIUMBE MZITO	DOLE	KILIMO CHA MUHOGO
4	MNYONGE HANA SHAURI	DOLE	UFUGAJI MBUZI
5	UMOJA NI NGUVU	DOLE	UFUGAJI KUKU
6	CHAZA NYAMANZI	NYAMANZI	KILIMO CHA CHAZA
7	BWELEO TUSIFE MOYO	BWELEO	KILIMO CHA MWANI
8	BADO TUPO	BWELEO	UTENGEZAJI SABUNI ZA MWANI, VYAKULA VYA MWANI, VYAKULA NA ACHARI
9	UKWELI NI NJIA SAFI	BWELEO	UVUVI WA CHAZA ZA

			LULU, SABUNI, MWANI NA MAFUTA YA MWANI
10	CHETU BWELEO	BWELEO	UVUVI
11	IMANI MOYONI	BWELEO	MAPAMBO YA CHAZA
12	NIA NJEMA	TOMONDO	USUKAJI MIKOBA NA UPIKAJI SABUNI
13	NURU NJEMA	TOMONDO	UFUMAJI, USUKAJI MIKOBA, MKAHAWA NA BIASHARA NDOGO NDOGO
14	TUPENDANE	MAGOGONI	UFUGAJI KUKU NA KAZI ZA SANAA
15	NACE SOAP	PANGAWE	UPIKAJI SABUNI
16	TUSIACHANE	FUONI MICHENZANI	KILIMO CHA MBOGA MBOGA, KUKOPESHANA NA BIASHARA NDOGO NDOGO
17	MSHIKAMANO DAIMA	MTOPEPO	KAZI ZA MIKONO
18	HATURUDI NYUMA	MTOPEPO	UFUGAJI KUKU NA KAZI ZA MIKONO
19	MTARAZAKI NI MOYO	WELEZO	KAZI ZA MIKONO
20	MKOROFI HATUFAI	MWERA	BIASHARA NDOGO NDOGO
21	MWERANJEMA SACCOS	MWERA	KUWEKA NA KUKOPA
22	MWANAKWEREKWE SACCOS	MWANAKWEREKWE	KUWEKA NA KUKOPA
23	MELINNE SACCOS	MELI NNE	KUWEKA NA KUKOPA
24	CHAZA MKOMBOZI	FUMBA	UFUGAJI CHAZA
25	CAHZA NJEMA	FUMBA	UFUGAJI CHAZA
26	LANGU MOYONI	FUMBA	UFUGAJI KUKU
27	DAIAMA TUWE IMARA	FUMBA	UFUGAJI KUKU

WILAYA YA MJINI:

S/N	**JINA LA KIKUNDI**	**PAHALA**	**SHUGHULI**
1	TUJIWEZESHE	SEBLENI	KUKOPESHANA VIFAA
2	UMOJA NI NGUVU	M/SHAURI	KUKOPESHANA VIFAA
3	TUJINASUE	SEBLENI	KUWEKA NA KUKOPESHANA PESA
4	FAHARI YA SEBLENI KAZI YAO	SEBLENI	KUTENGENEZA SABUNI
5	RIZIKI CHANZO CHA CHUKI	CHUMBUNI	KUTENGENEZA SABUNI NA KUKOPESHANA BIDHAA
6	AMANI NA UTULIVU	CHUMBUNI	KUTENGENEZA SABUNI, ACHARI NA VYAKULA VIKAVU
7	BORA IMANI	CHUMBUNI	KUTENGENEZA SABUNI, MIKOBA NA KUKOPESHANA
8	NIA SAFI HAIROGWI	CHUMBUNI	KUSUKA MIKOBA, KUFUMA NA KUKOPESHANA VIFAA
9	SAMIRA	CHUMBUNI	UFUGAJI NA KUKOPESHANA KANGA

10	TUAMKE	M/SHAURI	KUTENGENEZA BIDHAA ZINAZOTUMIA UKILI
11	MTAJI WA MASKINI	JANG'OMBE	BIASHARA NDOGO NDOGO ZA KUUZA VYAKULA
12	MSHIKAMANO GROUP	JANG'OMBE	BIASHARA NDOGO NDOGO ZA KUUZA VYAKULA
13	TUPO TAYARI	MAGOMENI	BIASHARA NDOGO NDOGO NA KUKOPESHANA
14	HARAKATI KINAMAMA	MAGOMENI	BIASHARA NDOGO NDOGO NA KUKOPESHANA
15	TUJIELIMISHE	MAGOMENI	BIASHARA NDOGO NDOGO NA KUKOPESHANA
16	BIENZI TAILORING	KWAHANI	KUSHONA NA KUFUMA
17	UKOMBOZI	KWAHANI	KUKOPESHANA BIDHAA

WILAYA YA KUSINI:

S/N	JINA LA KIKUNDI	PAHALA	SHUGHULI
1	TUJIKOMBOE	MUUNGONI	ASALI
2	MSHIKAMANO	PETE	UPANDAJI WA MIGOMBA
3	NIA NJEMA	MUYUNI 'B'	KILIMO CHA VIAZI, MUHOGO NA BIASHARA NDOGO NDOGO
4	TUWE SAFI	MUUNGONI	MAZINGIRA
5	CHETU SISI	MUUNGONI	UFUGAJI KUKU
6	SAFARI NJEMA	MUUNGONI	BIASHARA NDOGO NDOGO
7	NIA SAFI	MUYUNI 'B'	KUWEKA NA KUKOPA
8	YAONENI	MUYUNI "B"	MAZINGIRA
9	GREEN GROWERS	KITOGANI	KUTENGENEZA MAFUTA YA MKARATUSI NA MCHAI CHAI

WILAYA YA KASKAZINI "B":

S/N	JINA LA KIKUNDI	PAHALA	SHUGHULI
1	TUSIVUNJE MAADILI	GE NJIA YA MTONI	MO CHA MBOGA MBOGA
2	MKATALENI COOPERATIVE	TALENI	KA ACHARI
3	KERO LAO	GE MNYIMBI	MO CHA MBOGA MBOGA
4	NUSURA YETU	GE MNYIMBI	MO CHA MBOGA MBOGA
5	MTATUONA HIVIHIVI	GE MNYIMBI	MO CHA MBOGA MBOGA
7	SAA NJEMA	BWINI MISUFINI	MO CHA MUHOGO
8	TUWAMBIE NINI	BWINI MISUFINI	MO CHA MUHOGO
9	CHURURU SI NDO NDO NDO	BWINI MABUZINI	GA MBOGA NA MUHOGO

WILAYA YA KASKAZINI "A":

S/N	JINA LA KIKUNDI	PAHALA	SHUGHULI
1	NDANE	AURI	GAJI KUKU WA MAYAI
2	RI YA MOYO	RI	KILIMO CHA MBAAZI VIAZI

			VIKUU NA MUHOGO
3	USHIRIKA WA UFUGAJI NG'OMBE	EZA SHAURI	GAJI WA NGO'MBE
4	EMWE SACCOS	EMWE	EKA NA KUKOPA NA KUPIKA MIKATE
5	ALIPO	AURI	GAJI WA NGO'MBE
6	ULIWALO LIFANYWE	NGE	ZA MIKONO

WILAYA YA CHAKE CHAKE

S/N	JINA LA KIKUNDI	PAHALA	SHUGHULI
1.	TUSISHINDWE	TIBIRINZI	U/SABUNI/BIASHARA N
2.	PENYE NIA	TIBIRINZI	USHONAJI
3.	TARATIBU	WESHA	UPANDAJI MITI
4.	NIA SAFI	MADUNGU	USHONAJI
5.	TUVUMILIANE	DODO	USHONAJI
6.	WEMA UDUMU	DODO	UFUGAJI KUKU
7.	TUSITIRI SACCOS	DODO	K/KUKOPA
8.	MTAJI WA MASIKINI	KIJILI	KILIMO
9	TUPENDANE	BIRIKAU	KILIMO
10.	MWENYE KUSUBIRI	TIBIRINZI	BIASHARA NDOGO NDO
11.	MAISHA NI SIRI	MKOROSHONI	SABUNI/UFUGAJI
12.	MACHOMANE WOMEN	WARA	BIASHARA NDOGO NDO
13.	KICHANGANI WOMEN	WAWI	KILIMO/USASI
14.	JUMAWA	WAWI	USHONAJI
15.	BAADA YA DHIKI	TIBIRINZI	UFUGAJI KUKU
16.	TAHFIFU	MUHARITANI	USHONAJI
17.	KOMBANI	WESHA	KILIMO MIGOMBA
18.	YATAKA MOYO	NDAGONI	UFUGAJI SAMAKI
19.	UELEWANO	NDAGONI	UFUGAJI KUKU
20.	BORA UHAI	NDAGONI	UFUGAJI SAMAKI
21.	JUHUDI HULETA MAENDELEO	WARA	SABUNI/K/MIKONO
22.	TAKDIRI	MATALE	UFUGAJI KUKU
23.	MUWEZA	KUNGENI	KILIMO CHA MIHOGO N
24.	SHIKAMANENI	TUNDAUWA	UFUGAJI WA CHANZA N
25.	TUWE NA UMOJA	KIBOKONI	UFUAGAJIWA KUKU WA
26.	HONGERA STORE	VIKUTANI	DUKA

27.	JAMBO NIA	WAWI	USHONAJI
28.	CHANJAMJAWIRI TAILORING	CHANJAMJAWIRI	USHONAJI
29.	TEKELEZA WAJIBU WAKO	WAWI	UFUGAJI WA NGOMBE
30.	TUSHIKAMANE CO-OPEARATIVE	GOMBANI	USHONAJI, BIASHARA UTENGENEZAJI WA SAB

WILAYA YA MKOANI

S/N	JINA LA KIKUNDI	PAHALA	SHUGHULI
1.	NIA NJEMA	CHANGAWENI	ASAJI
2.	JITUME SACCOS	MWAMBE	O CHA KUNDE
3.	MIKARAFUUNI CO-OPERATIVE	MIKARAFUUNI	AJI KUKU
4.	NIA YETU SACCOS	MBUGUANI	KA NA KUKOPA
5.	TUAMINIANE	MTAMBILE	IAWA
6.	MWANZO MWEMA	JONDENI	O CHA MINANASI
7.	TUISHI KWA USALAMA SACCOS	UWELENI	NAJI KUWEKA NA KUKOPA
8.	UWZ – WANAWAKE	MWAMBE	ECHEA NA KILIMO
9	TUJIKOMBOE	MAKOMBENI	IMA NA CHANZA
10.	USHIRIKA WA USHONI	MICHENZANI	NAJI
11.	TUMAINI	MICHENZANI	ZA NA UKULIMA
12.	SHWAHIBA	MWAMBE	ANZI
13.	UKWELI	N'GOMBENI	I
14.	WATOTO YATIMA	MBUGUANI	AJI
15.	SUBIRA NJEMA	CHANGAWENI	LIA YA KUFUTIA MIGUU.
16.	WATOTO YATIMA	MWAMBE	AJI WA KUKU
17.	MAONI YETU	CHOKOCHO	NAJI
18.	JONDENI SACCOS	N'GOMBENI	KA NA KUKOPA
19.	VUNAVUNA	CHAMBANI	MBA
20.	TUPENDANE	CHAMBANI	MBA
21.	WALEMAVU	NGWACHANI	AJI WA KUKU
22.	UMOJA NI NGUVU	CHAMBANI	O NA UFUGAJI
23.	CHASASA	CHAMBANI	AJI
24.	NURU NJEMA	MBUGUANI	AJI WA KUKU
25.	TUUTUMIE WAKATI	MAKOMBENI	O NA USHONAJI
26.	MWENYE KUSUBIRI	CHANGAWENI	GENEZAJI SABUNI
27.	MWANZO MGUMU SACCOS	MKANYAGENI	A NA KUKOPA
28.	JAMBO GROUP	WAMBAA	AJI WA KUKU NA SAMAKI
29.	NIA KWENDA MBELE	WAMBAA	AJI WA KUKU NA KILIMO
30.	NGUVU MTEGO	WAMBAA	O CHA MIHOGO NA MIGOMBA
31.	WAMBAA SACCOS	WAMBAA	KA NA KUKOPA
32.	SISI KWA SISI	WAMBAA	UFUGAJI WA NGOMBE, UVUVI WA MAJONGOO NA UFUGAJI WA SAMAKI
33.	NIA NJEMA	KIWANI	O NA KUWEKA NA KUKOPA
34.	UZURI WA MTU IMANI	KIWANI	KILIMO CHA MIGOMBA, MIHOGO NA KUWEKA NA KUKOPA.
35.	SINALO	KIAWANI	KILIMO CHA MIGOMBA NA MIHOGO
36.	BORA LIWE SACCOS	WAMBAA	KUWEKA NA KUKOPA
37.	HATWEBU SHARI SACCOS	WAMBAA	KUWEKA NA KUKOPA

WILAYA YA WETE

S/N	JINA LA KIKUNDI	PAHALA	SHUGHULI
1.	HATUFI MOYO	M/TAKAO	U/KUKU
2.	TUNDWA CO-OPERATIVE	TUNDWA	U/KUKU NA KILIMO CHA MIGOMBA
3.	UWAPI CO-OPERATIVE	PILI	U/KUKU NA U/SABUNI
4.	KIMANGO CO-OPERATIVE	KIUNGONI	UPANDAJI WA MWANI
5.	SAFINA CO-OPERATIVE	JADIDA	UTENGENEZAJI SABUNI
6.	KAMBINI SACCOS	KAMBINI	KUWEKA NA KUKOPA
7.	M/MDOGO SACCOS	M/MDOGO	KUWEKA NA KUKOPA
8.	JUHUDI NI NGUVU	KISIWANI	UFUGAJI KUKU
9	UTAANI CO-OPERATIVE	UTAANI	USHONAJI, UFUGAJI NA BIASHARA NDOGO NDOGO.
10.	NIA NJEMA	KAMBINI	UPANDAJI WA MWANI
11.	MASHUGA CO-OPERATIVE	MASHUGA	UFUGAJI WA KUKU
12.	KILA ALIYAE HULILIA MAISHA	LIMBANI	UFUGAJI WA KUKU NA KILIMO CHA MBOGA MBOGA
13.	USIACHE MBACHAO	KISIWANI	UPANDAJI WA MITI
14.	MTOAJI NI MOLA	KISIWANI	KILIMO CHA MBOGA MBOGA
15.	MKIPI MILIKI	MACHENGWE	UTENGENEZAJHI SABUNI
16.	TUVUMILIANE	KIPANGANI	KAZI ZA MIKONO
17.	UMOJA GROUP	SELEMU	KUWEKA NA KUKOPA
18.	SELEMU WOMEN CENTRE	SELEMU	UTENGENEZAJI WA SABUNI
19.	MTAFURAHI TAILOARING	GOMBEUME	USHONAJI
20.	UMOJA NI NGUVU	BAGHANI	USHONAJI NA K/MBOGA MBOGA
21.	ALLAH KARIM	KIZIMBANI	KAZI ZA MIKONO NA USHONAJI
22.	KIVUNIE	KAMBINI	KILIMO CHA MPUNGA
23.	MUWAPE SACCOS	KILIMANDEGE	KUEKA NA KUKOPA
24.	MWIMO	KANGAGANI	UPANDAJI MITI
25.	YATAKA MOYO	PANDANI	UTENGENEZAJI SABUNI
26.	APENDWAE	PANDANI	UPANDAJI MITI
27.	MASKINI HACHOKI	KINAZINI	UFUGAJI KUKU
28.	RIZIKI MINLLAH	SHENGEJUU	UFUGAJI KUKU
29.	HALI WAKATI	NYALI	UFUGAJI SAMAKI
30.	MWANZO MGUMU	MPAMBANI	UVUVI
31.	KIBAYA CHAKO	KOJANI	KAZI ZA MIKONO
32.	MTU NI CHAKE	KOJANI	KAZI ZA MIKONO
33.	AZIMIO	M/OLE	UFUGAJI MBUZI

WILAYA YA MICHEWENI:

S/N	JINA LA KIKUNDI	PAHALA	SHUGHULI
1.	TAKASA	MSUKA	USUKAJI KAMBA NA U/MWANI
2.	MTU KAPUYE	MSUKA	KILIMO CHA MBOGA MBOGA
3.	MIN-AJIL-HUBI	MSUKA	USUKAJI WA KAMBA NA ZANA ZA MNAZI (VIFUU)
4.	MAJENZI SACCOS		KUWEKA NA KUKOPA NA UTENGENEZAJI WA SABUNI
5.	MICHEWENI SACCOS	MICHEWENI	KUWEKA NA KUKOPA
6.	TUJUANE SACCOS		KUWEKA NA KUKOPA NA KILIMO

			CHA MBOGA MBOGA
7.	SASA KAZI	MICHEWENI	KUWEKA NA KUKOPA NA KILIMO CHA MBOGA MBOGA
8.	MWENDA POLE	MICHEWENI	KILIMO CHA MBOGA MBOGA
9	KULEGA LEGA SIKUNG'OKA	MAJENZI	KILIMO CHA MBOGA MBOGA
10.	AWEZAE	KONDE	KILIMO CHA MITI
11.	YARABI SALAMA	TUMBE	UTENGENEZAJI MIKATE
12.	TUIMARIKE	W/NJUGUNI	UFUGAJI WA N'GOMBE WA MAZIWA NA UFINYAZI
13.	TUHAMASIKE	W/NJUGUNI	UFUGAJI WA KUKU WA KIENYEJI
14.	NIA NJEMA	MJANAZA	UFUGAJI WA KUKU WA KIENYEJI
15.	MWANZO HUWA MGUMU	SIZINI	UFUGAJI SAMAKI
16.	TUBADILIKE KIUCHUMI	KINYASINI	UTENGENEZAJI WA VIUNGO.
17	MOTO MOTO	KIFUNDI	KILIMO CHA MIGOMBA NA MIWA
18.	MAENDELEO BORA	FINYA	KILIMOMIHOGO NA MIGOMBA
19.	SAFINA	FINYA	KILIMO CHA MIGOMBA
20.	TUJALI WAKATLI	MAPOFU	KILIMO CHA MBOGA MBOGA
21.	MGOGONI WOMEN GROUP	MGOGONI	KUWEKA NA KUKOPA

Kiambatanisho Nambari 20a

MCHANGANUO WA FEDHA NA MATUMIZI KWA KAZI ZA KAWAIDA NA MISHAHA KWA MWAKA WA FEDHA 2011/2012.

MAKADIRIO 2011/2012					**FEDHA ZILIZOPATIKANA JULAI**		
FUNGU	**IDARA**	**JUMLA**	**MSHAHARA**	**M/MENGINEYO**	**JUMLA**	**MSHAHARA**	**M**
03	**PEMBA**	**340,995,133**	**170,995,133**	**170,000,000**	**284,091,991**	**149,359,733**	**1**
04	**M/S/UTAFITI**	**513,933,007**	**253,933,207**	**260,000,000**	**446,618,076**	**227,962,333**	**2**
05	**M/W/WATOTO**	**160,716,234**	**85,716,234**	**75,000,000**	**127,532,946**	**77,694,280**	**4**
07	**M/VIJANA**	**146,592,930**	**71,592,930**	**75,000,000**	**126,521,540**	**64,352,230**	**6**
11	**U/JAMII**	**508,783,594**	**328,783,594**	**180,000,000**	**483,184,616**	**309,274,538**	**1**
12	**U/UTUMISHI**	**135,800,000**	**75,800,000**	**60,000,000**	**128,852,112**	**73,461,144**	**5**
JUMLA		**1,806,820,898**	**986,820,898**	**820,000,000**	**1,598,801,281**	**902,104,258**	**6**

Kiambatanisho Nambari 20b

MCHANGANUO WA FEDHA NA MATUMIZI KWA KAZI ZA MAENDELEO KWA MWAKA 2011/2012.

FUNGU	IDARA	MAKADIRIO		KILICHOPATIKANA			
		SERIKALI	WAHISANI	SERIKALI	%	WAHISANI	%
04	M/S/UTAFITI	30,000,000	471,000,000	30,000,000	100	238466,400	51
12	U/UTUMISHI	-	-	-	-	-	-
05	M/W/WATOTO	30,000,000	297,000,000	30,000,000	100	78,374,800	26
07	M/VIJANA	20,000,000	-	20,000,000	100	-	-
11	U/JAMII	150,000,000	74,250,000	144,434,491	41	72,600,400	96
JUMLA		230,000,000	842,250,000	224,434,491	98	389,441,600	46

Kiambatanisho Nambari 21

MAKADIRIO YA MATUMIZI KWA MWAKA 2011/2012

	IDARA	MISHAHARA	OC	WAHISANI	F/MAENDELEO	JUMLA
1.	M/S/UTAFITI	78,113,000	240,000,000	556,000,000	60,000,000	934,113,000
2.	UTUMISHI NA UENDESHAJI	358,395,000	267,000,000	-	-	625,395,000
3.	USTAWI WA JAMII	306,379,000	310,000,000	230,600,000	340,000,000	1,186,979,000
4.	M/VIJANA	76,068,000	95,000,000	-	100,000,000	171,068,000
5.	M/W/WATOTO	100,777,000	127,000,000	300,000,000	20,000,000	347,777,000
6.	OFISI KUU	200,268,000	250,000,000	-	-	450,268,000
	JUMLA	1,120,000,000	1,289,000,000	1,086,600,000	520,000,000	3,915,600,000

Mhe. Amina Iddi Mabrouk (Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii): Mhe. Mwenyekiti, awali ya yote nichukue nafasi hii nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia uzima na afya njema. Aidha, kwa heshima nachukua fursa hii kukushukuru kwa niaba ya Kamati kunipa nafasi ya kuweza kuwasilisha maoni ya Kamati yangu juu ya makadirio ya bajeti ya Wizara ya Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto.

Mhe. Mwenyekiti, pia natoa shukurani zangu za dhati kwa Wajumbe wa Kamati yetu kwa kuweza kupitia Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo na kuweza kuishauri Serikali kadiri inavyostahili.

Mhe. Mwenyekiti, napenda kuwatambua kwa kuwataja Wajumbe wa Kamati yangu walioshiriki kuipitia bajeti ya Wizara ya Ustawi wa Jamii kama ifuatavyo:-

1.	Mhe. Amina Iddi Mabrouk	Mwenyekiti
2.	Mhe Hija Hassan Hija	Makamo Mwenyekiti
3.	Mhe. Asha Abdu Haji	Mjumbe
4.	Mhe. Ashura Sharif Ali	Mjumbe
5.	Mhe. Jaku Hashim Ayoub	Mjumbe
6.	Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa	Mjumbe
7.	Mhe. Nassor Salim Ali	Mjumbe
8.	Mhe. Saleh Nassor Juma	Mjumbe
9.	Ndg. Asha Said Mohamed	Katibu
10.	Ndg. Talib Enzi Talib	Katibu

Mhe. Mwenyekiti, nianze kwa kuipongeza Wizara ya Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto kwa mashirikiano makubwa wanayotupa wakati wote katika kazi zetu za Kamati. Muda mwingi Mhe. Mwenyekiti, tumekuwa tukisema
wizara hii ni wizara mama kwa vile inasimamia ustawi wa maisha na maendeleo ya watu, na ni wizara yenye nidhamu ya kupigiwa mfano kiutendaji.

Mheshimiwa labda niseme ni kwa sababu inaongozwa na mtu mzima na mtu mzima tunaambiwa ni dawa, lakini zaidi kwa sababu inaongozwa na mwanamama. Mara nyingi sisi akinamama tukipewa majukumu basi huwa tunakuwa makini zaidi kwa sababu ya woga. (*Makofi*).

Baada ya hayo sasa nianze katika usimamizi wa sera na sheria. Mhe. Mwenyekiti, miongoni mwa malengo ya bajeti ya wizara hii katika mwaka uliopita ni kurekebisha mapungufu ya sera na sheria za watoto, wanawake, vijana na wazee ili sera na sheria hizi ziweze kulinda haki za wahusika hao ipasavyo.

Kamati yetu inaipongeza wizara kwa kuweza kufanya mapitio na utayarishaji wa sera mbali mbali ikiwemo sera ya maendeleo ya vijana ya mwaka 2005 na sera ya uhai, hifadhi na maendeleo ya mtoto 2001 kwa lengo la kuzingatia sheria ya mtoto ya mwaka 2011.

Hata hivyo kamati yetu inaishauri serikali kuona umuhimu wa kuzingatia sekta husika katika kusimamia miradi ama programu zinazoihusu sekta hiyo moja kwa moja. Kwa mfano, kamati yetu haioni umuhimu kwa Afisi ya Rais ya Fedha na Mipango ya Maendeleo kuendelea kuendelea kusimamia programu ya uhai, maendeleo ya mama na mtoto badala ya usimamizi huo kuachiwa wizara husika ya ustawi wa jamii.

Mhe. Mwenyekiti, Wizara ya Ustawi wa Jamii ina jukumu zito la kutoa matunzo na huduma kwa wazee wanaoishi katika nyumba za wazee Unguja na Pemba. Tunaiomba serikali kuendelea kuendelea kuijengea uwezo wizara ili iweze kutoa huduma bora kwa wazee hao.

Mhe. Mwenyekiti, kazi ya kutoa matunzo na huduma kwa wazee na watoto kwa kweli ni kazi ngumu, ingawa malipo makubwa zaidi yapo kwa Mwenyezi Mungu lakini Wizara yetu ya Ustawi wa Jamii inastahiki kupongezwa kwa kusimamia na kuhakikisha kuwa watoa huduma nao katika nyumba maalum za watoto na wazee wetu wasiojiweza Unguja na Pemba wanapata posho maalum. Kazi hiyo tayari tumeanza ambapo wafanyakazi 118 tumearifiwa kuwa wameanza kupata posho la mazingira magumu.

Mpango wa Kuwatambua Watoto wanaoishi katika Mazingira Magumu zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, bado kuna changamoto katika kuwatambua watoto wanaoishi katika mazingira magumu zaidi. Hii inachangiwa kwa njia moja au nyengine na kukua kwa ongezeko la watu katika jamii. Tunaishauri wizara kuharakisha utekelezaji wa mpango wa kitaifa katika kuwatambua watoto hao ili kuepuka athari ya kuendelea kuwa na ongezeko kubwa la watoto wanaoishi katika mazingira magumu zaidi kwenye jamii bila ya kuwatambua.

Aidha Mhe. Mwenyekiti, kupitia zoezi la sensa linalotarajiwa kufanyika nchini ipo haja kwa wizara kutafuta namna ya kuweza kuitambua jamii ya watoto wa aina hiyo, ili kuweza kuwasaidia katika kuwaandalia mipango mizuri ya maendeleo ya baadae.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri ametueleza kuwa mchakato wa kutayarisha sera ya hifadhi ya jamii ambayo itatoa miongozo ya hifadhi ya jamii ya makundi yote, ikiwemo wazee na watoto wanaoishi katika mazingira magumu inaendelea.

Mhe. Mwenyekiti, wakati umefika wa kukamilisha sio sera hiyo tu bali hata kuanza matayarisho ya kuwa na sheria kamili itakayotoa fursa ya uhifadhi watu waliokuwa katika mazingira magumu. Watoto wengi na hata watu wazima wanahangaika katika mitaa na omba omba wanaongezeka kila kukicha katika jamii. Kukamilika kwa sera na sheria kutasaidia kuwepo kwa hifadhi ya jamii iliyorasmi na inayofahamika.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati yetu inaipongeza serikali kuona umuhimu pia kuanza kusajili watu wenye ulemavu wakiwemo watoto kwa lengo la kusaidia kutambua na kupatikana kwa haki zao. Matokeo ya majaribio yameonesha kuwa kuna zaidi ya watoto 800 wenye ulemavu katika mkoa ya Kaskazini Unguja.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati yetu imevutiwa kuwepo kwa utaratibu wa huduma ya marekebisho kwa watoto wenye ulemavu ambapo zaidi ya watoto 2000 wenye ulemavu wenye umri kati ya miaka 0 – 17 katika wilaya nne za Zanzibar wameweza kufaidika na huduma hizo. Tunaishauri Wizara ya Ustawi wa Jamii kushirikiana na Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais inayosimamia huduma za watu wenye ulemavu kuwa wabunifu katika kutafuta miradi ili iweze kusaidia watu wenye ulemavu wakiwemo watoto.

Kuhusu kesi za malalamiko juu ya udhalilishaji wa watoto na ongezeko la udhalilishaji wa watoto kijinsia:

Mhe. Mwenyekiti, Wizara ya Ustawi wa Jamii imekuwa mstari wa mbele katika kuhakikisha haki dhidi ya udhalilishaji wa watoto inatendeka. Licha ya juhudi hizo kamati yetu inasikitishwa na kuendelea kuwepo idadi kubwa ya kesi za udhalilishaji watoto.

Upande mmoja hali hiyo inaonesha kuwepo kwa kiashiria cha mwamko wa jamii katika kuvitumia vituo rafiki vya mkono kwa mkono (One Stop Centre) katika kuripoti kesi hizo. Upande wa pili ni kwamba serikali na taasisi za kijamii lazima zitafute namna ya kulisimamia suala hili kwa ukubwa na uzito wake la si hivyo watoto wetu wataendelea kuteketea.

Mhe. Mwenyekiti, tunaipongeza wizara kwa kukamilisha kituo cha mkono kwa mkono Chake-Chake Pemba. Tunaiomba wizara iharakishe utekelezaji wa lengo la kuanzisha vituo kama hivyo katika Wilaya za Wete, Kusini na Kaskazini Unguja.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusu uendelezaji na uimarishaji wa vikundi vya vijana vya uzalishaji mali:

Kamati yetu inasisitiza wizara kuwa na mpango na programu iendelevu na za muda mrefu katika kuendeleza na kuimarisha vikundi hivyo kwa kuwapatia mafunzo ya uanzishaji na uendelezaji wa SACCOS, ujasiriamali, uongozi na utunzaji wa hesabu. Vikundi vingi bado vinahitaji elimu hiyo ili viweze kumudu na kuwa na sifa za kutatua mikopo kutoka kwa washirika wa maendeleo na hata kuweza kujiendeleza na kujiimarisha kiuchumi.

Mhe. Mwenyekiti, tumevutiwa na juhudi za Wizara katika kufanikisha upatikanaji wa eneo maalum la kilimo cha mauwa na mboga mboga kwa vijana huko Tunguu na Mbuzini Pemba. Tunaiomba wizara juhudi zifanyike vile vile katika kuwakomboa vijana kwenye upatikanaji wa masoko. Miradi kama hiyo huwa ni ya kuvutia na mara nyingi huwa na nafasi kubwa katika soko la ndani hata ikiwezekana soko la nje.

Mhe. Mwenyekiti, katika juhudi za kuwakomboa wanawake kiuchumi, SACCOS ya Konde imeweza kuanzisha Benki ya Wanawake. Jumla ya wanawake 70 wamejiunga na benki hiyo. Jambo hili ni zuri sana na linastahili kupongezwa.

Tunaishauri wizara kuwashajihisha akinamama katika maeneo mengine ili waweze kujikusanya na kuanzisha benki kama hizo katika maeneo mengi zaidi hasa katika sehemu za vijijini.

Mabaraza ya Watoto:

Mhe. Mwenyekiti, Mabaraza ya Watoto ni muhimu kwa lengo la kujitambua na kujua haki zao na kutoa taaluma ya haki hizo kwa wenziwao ndani ya jamii. Mabaraza haya yanasaidia kutoa elimu na kuwajengea uwezo watoto katika kuendesha mambo yao.

Mhe. Mwenyekiti, uwakilishi katika mabaraza haya inaonekana bado ni finyu na upo katika maeneo ya mjini zaidi kuliko vijijini ambapo kuna idadi kubwa ya watoto ukilinganisha na mjini. Kuna juhudi zipi za wizara katika kuhakikisha unapatikana uwiano katika Mabaraza ya Watoto. Ni vyema basi ikiwa Mabaraza haya yakagawa kwa kila wilaya au kimajimbo na Wajumbe wa Baraza lako Tukufu wapewe fursa ya kuyatambua na kufanya kazi nao pamoja.

Mapitio ya Sheria ya Mahakama ya Kazi:

Mhe. Mwenyekiti, kwa taarifa wizara imefanya mapitio ya sheria ya Mahakama ya Kazi ya mwaka 1985 kwa mashirikiano ya Wizara ya Katiba na Sheria na Afisi ya Mwanasheria Mkuu ili iendane na hali halisi ya mabadiliko ya dhana ya usawa ya jinsia bila ya kukiuka misingi ya dini ya Kiislamu.

Ushiriki wa maoni ya wadau mbali mbali ulitekelezwa hadi kupatikana rasimu ya mapendekezo ya mswada mpya. Tumeishuruku wizara kwa kutupa semina maalum juu ya hili na tunawaomba semina kama ile iwape Waheshimiwa Wawakilishi wote wa Baraza hili.

Na kwamba kamati yetu inaiomba serikali kwa jumla kutofanya haraka katika kuanzisha sheria ya Mahakama ya Kazi ili kupata mazingatio zaidi kwa sababu sheria hii inagusa masuala ya msingi ya dini yetu ya Kiislamu.

Mwisho kabisa Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dr. Ali Mohamed Shein amekuwa akihimiza kuhusu suala la utafiti katika taasisi za serikali kwa ajili ya kuweza kubaini vyanzo vinavyotukwaza kimaendeleo katika sekta tofauti na hatimaye kuweza kuvitafutia ufumbuzi.

Tunaipongeza Wizara ya Ustawi wa Jamii kwa kuanda jenda za tafiti za masuala muhimu mbali mbali yanyohusiana na wizara yake. Changamoto iliopo ni utekelezaji wa uendeshasji wa tafiti hizo hasa ukizingatia kuwa tafiti ni gharama kubwa/

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hotuba yangu ambayo nimewakilisha Kamati yangu kwa mujibu wa Kanuni sitopata nafasi tena ya kuchangia hotuba hii. Sasa kwa ruhusa yako basi naomba nichangie kwa niaba ya wanawake wa Mkoa wa Mjini/Magharibi.

Mhe. Mwenyekiti: Nimekuruhusu Mheshimiwa endelea.

Mhe. Amina Iddi Mabrouk (**Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii):** Mhe. Mwenyekiti, kwanza nianzie kwa kusema kwamba leo ni siku ya historia katika Baraza letu la Wawakilishi. Ninasema hivi kwa sababu hasa kwa kuwa leo Mwenyekiti ambaye unatuongoza katika Baraza letu hili tukufu ni mwanamke.

Lakini pia tunajadili hotuba ya bajeti ya Wizara ya Wanawake na Ustawi wa Jamii. Kama hilo halitoshi Makatibu wetu wasaidizi ambao wapo pale chini ni wanawake. Lakini mbeba rungu wetu ni mwanamke ambaye ameleta rungu asubuhi ya leo. Lakini kama hayatoshi hayo hata mimi mwenyewe Mwenyekiti wa Kamati hii ni mwanamke ambaye punde hivi nimewasilisha hotuba hii. Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli haijapata kutokea. (*Makofi*).

Sasa Mhe. Mwenyekiti, nichukue nafasi hii kwa heshima na taadhima niwaombe Waheshimiwa Wawakilishi wote wanawake waliokuwemo humu ndani tuichangie bajeti hii ili tuweze kutoa maoni yetu kwa ajili ya maendeleo ya nchi yetu. Lakini pia tumpe nguvu mama yetu ambaye ni mwanamke lakini mama huyu ni jasiri sana, yupo karibu sana katika kufuatilia kazi zake, mama hongera sana. (*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa leo tunajadili bajeti hii ya wanawake itakuwa si vizuri basi kama sijachukua nafasi hii ya dhati kabisa, nafasi adhimu kumpongeza kipenzi chetu Mhe. Dr. Ali Mohamed Shein kwa kuondosha ada ya malipo ya mama mjamzito. (*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, na Waheshimiwa Wajumbe kama tunavyokumbuka tulikuwa tunasema na kulalamika kwenye suala hili, lakini hatimaye Rais wetu na kipenzi chetu ametusikia. Kwa hivyo tunakushukuru.

Baada ya hayo machache Mhe. Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Ustawi wa Jamii ningekuwa kwenye kiriri ningesema akinamama oyee! Lakini kwa sababu ni Mwenyekiti basi naomba kwa muda ambao tunao kama dakika 35 tutapata wachangiaji kama wawili. Kwa hivyo namuomba Mhe. Makame Mshimba aanze kuchangia.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, sijui nijieleze namna gani kwa sababu Mheshimiwa Mwenyekiti alipoondoka hapa alisema kwamba wizara hii ni ya akinamama, na mimi nikijiona ni mwanamme. Kwa kweli Mhe. Mwenyekiti, nitapata shida kidogo. Lakini niseme kidogo tu Mhe. Mwenyekiti, naomba radhi sana wananchi wanaotusikiliza huko kuwa kuvaa miwani si mbwembwe tu isipokuwa ninaumwa na macho, kwa sababu wengi wanajiuliza mbona sura yake hatuioni, siku hizi kawa sharobaro, aah! Naumwa na macho tu Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti, nisipoteze muda wako lakini kwanza naomba niulize haya mabadiliko tuliyoletewa jee Kamati inatambua au mambo ambayo yaliyokuwa sasa hivi yanataka kuhojiwa kama alivyohojiwa jana Mheshimiwa aliyepita Mhe. Waziri, ndio mchezo wenyewe unataka uwe hivi. Naomba hili nije nipewe hoja ambayo iliyokuwa ni nzuri ili niweze kuipa baraka wizara hii.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, niende kuchangia kwenye ukurasa wa 14 Idara ya Uendeshaji na Utumishi. Mhe. Mwenyekiti, tumeambiwa kuwa idara hii ina majukumu ya kusimamia shughuli za kila siku za uendeshaji na utumishi wa wizara zikiwemo sheria, kanuni, utumishi, mafunzo na maslahi.

Mhe. Mwenyekiti, kusema ni kusema, kutunga ni kutunga, tatizo utekelezaji wenyewe upo. Nitatoa mfano mdogo Mhe. Mwenyekiti, nimuulize mama yangu tu.

Mhe. Mwenyekiti, anaendeshwa na dereva hapo ndio ninataka nianzie. Tumepiga sana maslahi ya madereva lakini hapa kuna mbinu nyengine ambayo jee hawa madereva nao haki zao wanapatiwa kwa kupitia kifungu hiki.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri huwa anakwenda kwenye semina lakini cha kushangaza kwenye semina kitu ambacho anachokumbuka Mhe. Waziri ni kumtafutia mlo tu wa siku ile dereva na sio posho. Sasa jee kwa nini na posho wanakuwa wanapewa katika zile semina wanazowapeleka viongozi wetu wakuu.

Sasa nalo na hili tuwafikirie kama wanapewa *minalfaidhina* na kama hawapewi basi wapewe tusiwatafutie ubwabwa tu wa kula, kwa sababu wewe Mheshimiwa unakwenda pale unakula na posho unalichukua. Sasa nikasema leo nianze kwa hapo kumwambia Waziri wangu ili aione ni jinsi gani nao hayo maslahi yanafanyika wanafanyiwa madereva halikadhalika na watendaji wengine.

Mhe. Mwenyekiti, kitengo hiki ni kigumu sana na ni kizito, anayepewa kitengo hiki ajue kuyafuatilia maslahi uzuri ya wafanyakazi kwa sababu wananchi wetu ni maskini wengi. Sasa unapopewa dhamana ya kitengo hiki, sharti uwe *smart* sana uhakikishe haya mambo yanafanyika na hasa hivi sasa hizi *change* za kada za mishahara ahakikishe kwa uwazi kabisa kuwa haya mambo yanatendeka kwa uadilifu na kwa mujibu wa sheria za utumishi.

Mhe. Mwenyekiti, sasa niende kwenye hiyo idara yenyewe ambayo tunayoambiwa. Mhe. Mwenyekiti, aliyeondoka hapo ameeleza mambo mengi sana ya akinamama na mukajinasibu sana akinamama na ndio wajibu wenu, lakini sisi akinababa tuna wajibu wa kukuteteeni nyinyi akinamama.

Katika safari yangu niliyoondoka kwenye kitabu hiki nitakuwa mkali sana, kuna baadhi ya mambo akinamama haki zao hawapewi na sio kutokana na akinababa aah! Akinababa tunatoa haki vizuri tu kwa akinamama, wala hatuwalazimishi. Lakini jee hii wizara yenyewe inatoa haki kweli kwa akinamama. Yapo mambo huko mbele lakini wacha niingie kwenye ukurasa wa 64 Idara ya Maendeleo ya Vijana.

Mhe. Mwenyekiti, idara hii kuna mambo hapa tumeyaweka hapa au idara imejipangia utekelezaji wa malengo yafuatayo, kukuza uwezo, kuendeleza vijana, kukamilisha uundaji wa Baraza la Vijana Zanzibar. Nijue tu hili Baraza tayari lishakuwa tayari Mhe. Waziri limeshaundwa.

Lakini vile vile niseme kuwa Mhe. Mwenyekiti, mara nyingi tunakuwa tuna mambo mengi ya kuyaeleza, kuendeleza na kuviimarisha vikundi vya vijana vya uzalishaji mali kwa kutoa mafunzo, uanzishaji wa SACCOS na utunzaji wa hesabu.

Mhe. Mwenyekiti, tuwe wakweli. Tumesema vya kusema lakini bado wimbi la vijana lipo nje kubwa. Vijana wa Kizanzibari Mhe. Mwenyekiti, wapo nje wengi hawana kazi wanakaa vijiweni, tuseme ukweli ulivyo. Mimi hutizama sana zile hesabu munazosema ni za *technician*, kwamba kwenye vijana watano mmoja anapata ajira, tunazungumza tu lakini ukweli hasa hatujakwenda *in deep* kabisa. Huo ukweli tuuseme.

Tukifanya ziara katika sehemu za kazi, tukafanya hiyo *evaluation* yenyewe kuangalia wangapi basi utakuta vijana wa Kizanzibari ni kidogo sana. Haki yao haipo.

Wimbi la wizi linaingia, vijana wanakula dawa za kulevya hawana ya kufanya. Tunawaacha tu kwa kweli hatujawa tayari au hatujakuwa *serious* ya kusema sasa tuwasaidie sasa vijana kikwelikweli. Tunaweza kwelikweli kwa sababu hivi sasa kazi nyingi zipo, hoteli zimejaa kibao lakini hawapati kazi. Wallahi mimi ninasikitika sana.

Lakini kwa nini tusiwatafutie nyenzo ambazo tuna uwezo, serikali ina uwezo bwana, tutakuja kuona kwenye mafungu yao hapa. Siku hizi tunakwenda hapa kwa mtindo huu. Na ndio maana tukaanza kuuliza mapema wanaijua hii Kamati.

Mhe. Mwenyekiti, mimi naomba vile vile niulize katika masuala yake ya vijana kwa kweli leo mimi ninasema kwa unyonge inanisikitisha katika idara yake hii bado vijana hatujawatendea haki, bado vijana elimu ya kutosha hatujawapa, bado vijana hatujawawekeza sehemu za kuwatafutia eneo la kuwaweka tukaamini kama hapa vijana tumewawekea eneo ambalo wanafanya miradi yao midogo midogo, mtu akitoke nje tunajua tunakwenda kuwapelekea sehemu hiyo na wanaona kama kweli serikali imetumia juhudi zake zote imewatafutia eneo na kuwatengenezea sehemu pazuri pa kufanya ajira zao kutosha ili kuweza kuweka na wao bidhaa bora kupeleka kwenye Sabasaba au katika nchi za nje. Hiyo bado.

Lakini niingie katika ukurasa wa 28, ninakwenda mbio mbio Mhe. Mwenyekiti. Hapa ukurasa huu Mhe. Waziri amesema kuwa wizara yake imefanya mazungumzo na wafanyabiashara wa ndani na mashirika ya umma juu ya upatikanaji wa ajira. Lakini jee hii hesabu kweli aliyoifanya humu au basi tu katuwekea kwa kuwa leo tutambue hivyo. Mimi sijaridhika na hesabu hii si kweli.

Mama yangu nikutake radhi sana si kweli kabisa. Lakini hebu tuchukulie wale askari wetu walioajiriwa pale Hospitali ya Mnazi Mmoja, Mheshimiwa wanaangalia wale maslahi yao au kwa kuwa wamepata ajira tu wale. Hebu waulizeni na wafuatilieni wana mshahara mzuri pale na wanafanya kazi, wanaitilia kweli serikali *alhamdulillah*, wanakusanya mapato, maana yake mapato yale wanayokusanya wale mpaka Wizara ya Fedha inaingia wivu wanayataka yale yale, wanayachukua. Sasa hebu tizama jee wanapata ajira, ajira ipo lakini kweli wanapata maslahi yao, usitizame kile kipato chake cha kuvuja jasho kina msingi.

Sasa mimi ningemuomba Mhe. Waziri hebu liangalie kwa makini ni kweli umefanya hiyo shughuli ninakushukuru sana kwa maelezo yako mazuri matamu mwanana, lakini ni kweli Mheshimiwa.

Mhe. Mwenyekiti, sasa tuende ukurasa wa 30, *wallahi* mama yangu ninakupenda sana na ndio maana leo ninakuwa mkali kwa sababu ni mama. Lakini kama isingekuwa hivyo ningezuia mafungu leo kweli kweli humu kwa sababu nimeshapitia nimeshakuta makosa mengi. Lakini naomba nisije nikakosa radhi na ndio maana ninasema kidogo kidogo.

Mhe. Mwenyekiti, ninakuja kwenye Idara ya Maendeleo ya Wanawake na Watoto. Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli bado utekelezaji wa sheria ya mtoto wa Zanzibar mimi naona bado, watoto wengi hivi sasa wanaendelea kudhalilishwa. Jambo hili linanisikitisha sana.

Biashara za mitaani watoto zimeingia, zinaendelea kukua Mhe. Mwenyekiti. Mhe. Mwenyekiti, na mimi kwa sababu ni mjasiriamali nikiona hali kama ile basi ile bidhaa huwa ninainunua hata thamani yake ni shilingi thalathini elfu ili yule mtoto asifanye tena biashara ile amwambie na mama yake na ujumbe huwa ninautoa.

Mhe. Mwenyekiti, tujikazeni tuwaambieni hawa akinamama wawe na uchungu na watoto wao wasiwadhalilishe kiasi hicho, kuwabebesha masufuria, masinia na vitu chungu nzima, haifai haikhalisi hai-*cost*. Itakuwaje wewe mzazi mwanao. Siku hizi akinamama hamna urembo, utaona kule marikiti akinamama wenyewe na *lipstick* zao wanauza biashara. Sasa inakuwaje mwanamama wewe unaona urembo unakwenda kumtoa mwanao, unakwenda kumuuza mwanao kwa bei rahisi tu.

Mhe. Mwenyekiti, hili naomba sana sheria hii ikamate mkondo wake tusifanye mchezo. Tunawapuputisha watoto. Ndio maana jana Mheshimiwa tulikaa mimi na wewe faragha, sio kwa kunilishia kutokana na bajeti yako, aah! Kuna kitu nilikwambia *attention* mapema nimekiomba hawa vijana wa skauti.

Mheshimiwa bwana kwa kweli Mkurugenzi husika nimeona barua ya kuwadhalilisha kwa makusudi kuzuia kwenye mikutano yao vijana maskini ya Mungu wanajikusanya kwa kutaka kujitoa maelimisho, na watoto wale wana mafundisho mazuri sana. Kwa nini anafika pahala anawadhalilisha vijana hawa na wakati yeye ndiye mlezi. Hawataki basi hawataki yeye, wenyewe kutaka awaachie huru.

Hilo ninasema nitakuwa mkali sana kwa hilo tu kwanza, awaachie hawa vijana mara moja kwa sababu kijana anapoanza kuji-*organize* mwenyewe wewe umuelekeze, ndio vijana wale wanaopewa visinia vikenda vikauza, leo yeye anakwenda kuzuia kwa makusudi tena kanilisha hasara na anilipe fedha zangu shilingi laki tatu kwa makusudio ya kwenda kufanya mkutano kwa nia nzuri tu. Hii ndio tabia yetu. Unajua siku hizi tuna tabia hata na sisi wengine humu ukisema sana, mara unaambiwa muamsho, ukisema sana mara unaambiwa CUF, kwa nini mtu asitetee haki. Ile ni haki yetu jamani tumeshaamka sasa hivi lazima tutetee haki ya Wazanzibari hapa na sisi ndio watetezi. (*Makofi*).

Hawa vijana kwa nia nzuri tu wakageuzwa jina hilo wakaambiwa aah! Ni skauti wa muamsho, muamsho wa nani? Tusiende huko, wakatiwa jina baya. Akaambiwa Kamanda Polisi yule wa Wilaya kwamba ahakikishe wasifanye mkutano hawa, eeh! Na mimi nishakuwa kiongozi wa muamsho *inshallah* kheri, maana yake ndio maana yake hiyo.

Kama utaratibu umekosewa tuite au waite wakusanye waelimishe vizuri waelekeze njia wafanye. Ndio nikakwambia viongozi tuwe na nia nzuri na insafu nzuri. Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri kwa hili ninakuomba sana wapeni uhuru vijana wafanye shughuli zao, ile ni NGO. Maana yake NGO ni maana yake nini. Tumepitisha na sheria hapa na Waziri wa Katiba ruksa, *registration.* Kama hawajafanya *registration okay* basi wafundishwe ili waweze kufanya *registration* hiyo. Lakini tunawahangaisha tu vijana, wale ni taifa la kesho. Mimi ninataka nirithiwe, kama mimi nilivyokuwa ninataka nirithi *and then* pengine nikawa ni *government* wa Zanzibar na ndio ilivyo huwezi kujua kama mimi ningeingia kwenye Baraza la Wawakilishi, pengine nyinyi mutasema kuwa Mhe. Mshimba ndiye *president* of Zanzibar, inawezekana hiyo.

Sasa na hawa ni taifa letu la kesho, ni lazima tuwafundishe na tuwakubali ili tuwaweke katika nafasi nzuri, tuwatafutie maeneo. Mhe. Mwenyekiti, hili mimi nitakufa nao hawa vijana na nitahakikisha tunatengeneza skauti ya kisasa na tutawatafutia maeneo, tutawaomba *donors* wapo wa kuweza kuwasaidia, tukawaweka watoto tukawafundisha mafunzo yote yanayotakiwa kwa mujibu wa taratibu.

Lakini kifungu hiki kwa kuwainua akinamama, sasa hapa ndio ninawaambia akinamama inatubidi sisi tukupigieni debe. Sasa ninakupigieni debe akinamama. Mhe. Mwenyekiti, pamoja na kuwa hii ni wizara ya akinamama na Katibu ni mwanamke lakini bado akinamama hatujataka kuwainua.

Mhe. Mwenyekiti, ukifanya hesabu ni ndogo sana wanaopata mikopo kwenye benki. Lakini ukienda Tanzania Bara ni tofauti sana. Sasa hapa ndio panaponiuma, mabenki yale yale yapo hapa Zanzibar wanatoa mikopo kule kwao Tanzania Bara wanawapa akinamama wanafanya maendeleo na kila biashara. Lakini mabenki haya haya sijui kwa nini wanashindwa au kwa sababu sisi hatuendi. Nendeni akinamama, Waziri nenda akinamama waite. Kuna tofauti gani na mimi sioni kama kuna tofauti yoyote.

Ndio maana utakuta hivi sasa akinamama kule Bara asilimia 99 wana kazi zao za binafsi. Lakini leo hapa Zanzibar asilimia ndogo tusidanganyane wanawake mbona hamupigi makofi, wanapiga makofi wanaume tu, mujue tunakuteteeni. Musisite akinamama muwe *serious* kuwatetea akinamama wenzenu.

Mimi ninajitolea muhanga kuwatetea akinamama na mimi ni baba, kwa sababu nimeona *effect* yake ni hiyo. Ukizunguka huku unadaiwa pesa lakini jee yule mama akiwa na kazi yake atakuomba pesa, hakuombi pesa. Akinamama hapa ni asilimia ndogo sana wanatafuta pesa zao wenyewe na wanagonga ukuta kwa sababu hawapati *support*, ni riba kubwa, vikwazo vingi mabenki. Tukifanya *evaluation* hapa ni nani akinamama anayemiliki nyumba, hata aweze akapate mkopo benki. Tusifanye mchezo.

Ndio maana wanakuwa changu doa na nini, inakuwa kwa sababu ya dhiki. Lakini penye shida laki tano atakumbuka mambo haya, hayakumbuki hata siku moja. Kwa hivyo mimi ninaiomba sana Wizara hii kwa heshima na taadhima kabisa, na mimi nitakuwa ni mfano historia kwa leo mwanababa kukaa akajitolea kuwapigia debe wanawake na mimi itakuwa historia leo, kwa sababu ninaamini hiyo wapo akinamama wanaojitolea, SACCOS zipo lakini *funds* zake ni ndogo. Tusidanganyane kwamba hii SACCOS si kweli.

Sasa mimi ninaamini kama wizara hii itakuwa *serious* kabisa ianze tu hapa ikimaliza bajeti yake tukipitisha ipite benki hadi benki waite. Wala usifanya mchezo mama yangu hili ndilo litakalokuokoa haki ya Mungu. Waite uwakusanye akinamama, sitaki nikufundisheni ujanja lakini inabidi nikufundisheni ujanja kwa sababu ya dhiki.

Mimi nina watoto wanawake zaidi ya wanne pengine na wao ikipita hii na wao watafaidika. Wananchi wa Jimbo la Kitope wapo chungu nzima tena wameji-*organize* vizuri tu. Kitu kimoja kinachonichekesha, wanazo SACCOS zinakwenda vizuri, hivyo kwa nini tushindwe.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri sitaki nikupigie buti na mara hii sikupigii buti *wallahi* ukinijibu vizuri mama yangu, unikiambia Mhe. Mshimba hata mimi niite muokozi tutakwenda kwenye mabenki tukawatafutia hawa ili waweze kunufaika. *Otherwise* vyovyote tutakuwa tunawasema vizuri lakini tunawa-*block* akinamama.
Mhe. Mwenyekiti, kama alivyosema Mwenyekiti wangu wa Kamati na mimi ningesema hivyo hivyo akinamama wawe, lakini ninashindwa kusema kwa sababu Kanuni hainiruhusu. Lakini ninachotaka kusema kuwa Mhe. Mwenyekiti, ninaomba sana hii Wizara hii mimi sitaki niitie mashakani na sikutaka kuchangia leo, lakini nimeumwa na uchungu sana kuona akinamama bado hatujawawezesha.

Kwa hivyo Mhe. Mwenyekiti, la mwisho tuliomba ile hati ya watoto wa kulelewa pale sijui ishakuwa tayari ile. Kama tayari Mhe. Mwenyekiti, utakapokuja utuletee ile hati tuione kuwa wale watoto wanaolelewa kwenye nyumba ya kulelea pale wameshapewa hati yao ili tuweze kuwasaidia.

Mhe. Mwenyekiti, ninaheshimu sana kiti chako kwa hayo machache ninataka niunge mkono hii hotuba lakini siiungi mkono mpaka aniambie akinamama kuwa sasa watakwenda mama benki hadi benki na kuweza kuwasaidia kuwakomboa akinamama katika hali ya uchumi.

Ahsante sana ninangoja jibu nimuunge mkono. (*Makofi*).

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwanza kabla kuniruhusu naomba niseme machache.

Mhe. Mwenyekiti, Wajumbe wako sisi wa Baraza tunapohoji serikali tunawatumikia wananchi, hatufanyi mambo ya kihuni. Vile vile sisi tumekula kiapo, kama alichokula Waziri, Naibu Waziri, sote tumekula kiapo cha utii cha Katiba ya Zanzibar.

Baada ya kuniruhusu hayo Mhe. Mwenyekiti, na mimi niungane na Mhe. Waziri na Mwenyekiti wangu kwa suala ambalo tumekuwa tunalipigia kelele kwa muda mrefu na hasa miongoni mwao nikiwa ni mimi. Nilithubutu kusema kuna watu wanaweka rehani vitu vyao katika hospitali ya Mnazi Mmoja ili kupata kujifungua, zikiwemo bangili zao za dhahabu, simu, na televisheni.

Mhe. Mwenyekiti, nashukuru hilo limeonekana ukweli wake na Mhe. Rais kalisikia. Kwa hivyo, hilo ni jambo la kutia moyo, kwa niaba ya Kamati vile vile ya wanawake na watoto ambayo na mimi ni Mjumbe wake nalipongeza sana suala hili, ni kilio ambacho kilikuwa ni cha muda mrefu, kwa hivyo hivi sasa itasaidia kupunguza vifo vya mama na watoto ni kitu cha kupongezwa sana tena sana kwa kuliona hilo.

Vile vile nataka nimpongeze tena Mhe. Rais kwa kukiona tena kilio cha wazee, kwa kuongeza milo mitatu kwa siku. Kwa kweli wale wazee kamati ilivyowatembelea ilisikitika na kutokwa na machozi kwa hali ilivyo katika nyumba za wazee huko kisiwani Pemba na Amani Welezo. Kwa hivyo, nimpongeze Mhe. Rais kwa kukiona hicho. Vile vile Mhe. Waziri nitahitaji maelezo kutoka kwako kuhusu wafanyakazi hawa 118 wanaopewa huduma katika vituo vya kutunza wazee kisiwani Unguja na Pemba, namuomba Mhe. Waziri wafanyakazi hawa wanalipwa posho kiasi gani kwa mwezi ili tuweze kuthamini kazi nzito wanazofanya kuhusu Idara ya Ustawi wa Jamii.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri, amesema katika kesi 689 za udhalilishaji watoto, zimepelekwa katika kituo cha *one stop center*, zikiwemo kesi 287 za kubakwa watoto na kupewa ujauzito kesi 82 wamepatikana. Lakini hujatueleza ni kesi ngapi zinazoendelea na vile vile zilizoko mahakamani katika kitabu chako hiki.

Mhe. Mwenyekiti, kukosekana kwa mashine ya kutambua vinasaba yaani (*DNA machine).* Je ni nani mwenye jukumu la kununua mashine hiyo, nataka kujua ni Wizara ya Afya, Wizara ya Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto au ni Wizara ya Mambo ya Ndani. Kwa hapo Mhe. Waziri nataka unieleze, la si hivyo niko tayari Mheshimiwa kama yaliyonikuta jana, kwa kuwatumikia wananchi, hata kwa kuvutwa shati niko tayari. Hapa nitahitaji maelezo ya kina Mhe. Waziri.

Mhe. Mwenyekiti, haiwezekanani serikali ikashindwa kununua, wakati tunapitisha bajeti ya viburudisho kwa kila wizara humu, kwa hili nitakuwa mkali tena Mhe. Mwenyekiti, kwa lolote niko tayari. Mtume (SAW) kapata shida kuisambaza dini hapa mpaka ikasimama, itakuwa hilo kuja kutukanwa tena na kushambuliwa mimi niko tayari. Ikiwa tunapitisha bajeti ya viburidishaji humu, tukaacha mashine ya *DNA.* Mhe. Waziri hapa nitahitaji maelezo ya kina kweli kweli, niko tayari kwa lolote litakalotokea kwa hilo Mwenyezi Mungu atanisaidia.

Mhe. Mwenyekiti, jengine ni kuhusu utendaji wa Baraza la Vijana Zanzibar, katika ukurasa wa 25, suala hili limekuwa ni la muda mrefu, lakini utekelezaji wake umekuwa ni tatizo kubwa sana.

Mhe. Mwenyekiti, chombo hiki kina umuhimu sana kwa vijana katika kujadili mipango ya maendeleo yao, na kutoa mchango katika kupambana na vita dhidi ya dawa za kulevya pamoja na maradhi ya ukimwi. Hiki chombo kinahitaji Mhe. Waziri unipe maelezo kwamba ni lini kitaanza.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kumalizia la mwisho kabisa ni suala la ombaomba. Mchango wangu kuhusu Idara ya Mipango ya Sera na Utafiti, naomba nichangie katika ukurasa wa 11. Katika ajenda zako 9, hili suala umelitaja la ombaomba, suala la ombaomba halihitaji utafiti Mhe. Waziri nataka nikueleze wazi. Hii ni kutokana na nchi yetu vijana wetu wengi kutokuwa na kazi, na baadhi ya familia kuporomoka vipato vyao. Hili halitaki utafiti kupoteza pesa za serikali bure Mhe. Waziri, suala hili ni zito.

Kwa hivyo, ushauri wangu ni kwamba serikali tatizo hili chimbuko lake ni umaskini, kazi ya kufanya hakuna, kipato katika familia kimeanguka na kuongezeka ombaomba. Vijana hivi sasa msingi wake ni kuimarisha kitengo chetu cha mafuta cha Zanzibar ili vijana wetu wapate ajira. Huu ndio ushauri wangu mimi, ambao hautaki hata kulipwa pesa na serikali. Suala letu ni kwamba mafuta Zanzibar yashughulikiwe ili vijana wetu wapate ajira.

Kwa hayo machache Mhe. Mwenyekiti, sitoipitisha hoja hii mpaka nipate maelezo ya *DNA.*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Mjumbe. Waheshimiwa Wajumbe, nafikiria kwa muda ambao tumeubakisha ni muda mdogo sana na Wajumbe wanaofuata naamini kwamba watataka kuchangia kwa upana. Kwa hivyo, nachukua fursa hii kuakhirisha Baraza hili hadi jioni saa 11:00.

Waheshimiwa Wajumbe, ombi langu ni kwamba wale Wajumbe wote ambao wamejiandikisha kwa ajili ya kuchangia jioni, basi wafike mapema ili utaratibu ambao hapa umepangwa utekelezeke. Nakushukuruni sana kwa utulivu wenu na mashirikiano mema, tunaakhirisha mpaka jioni ahsanteni.

(Saa 6:00 mchana Baraza liliakhirishwa hadi saa 11:00 jioni)

(Saa 11:00 jioni Baraza lilirudia)
(Majadiliano Yanaendelea)

Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak: Mhe. Naibu Spika, ahsante sana. Kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia afya na uzima kuweza kufika jioni hii na kutekeleza majukumu yetu ambayo tumejipangia kwa wakati huu.

Pili nimshukuru mama yetu Mhe. Zainab Omar Mohammed, huyu ni mama ambaye amepewa wizara ya ulezi wa watoto, vijana, wanawake, hivyo anao ulezi mkubwa. Kwa hivyo, nimpongeze tena anauweza huu ulezi, kwa sababu pale linapotokezea tatizo au janga kwa wanawake husimama kwenye chombo cha habari na kutoa hadhari. *(Makofi)*

Kwa mfano, jana nilimuona kwenye *television* akitoa hadhari juu ya udhalilishaji wa wanawake, kutokana na matukio ambayo yaliyotokea kuchukuliwa wanawake na watu na kwenda kuwatoa fahamu na kuwafanya vitendo ambavyo havina maana. Kwa hivyo, alitoa tahadhari kwenye ripoti yake ile kwa hili nampongeza, yaani ni Waziri ambaye ameonesha mfano juu ya kuwatetea wanawake na watoto. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, nianze kwenye kitabu hiki katika ukurasa wa 3. Katika ukurasa huu kuna sentensi hapa ambayo ameitumia Mhe. Waziri naomba kunukuu Mhe. Naibu Spika. "Wizara inaishukuru na kuipongeza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kufanikisha zoezi la kuwafariji na kutoa misaada kwa wahanga wa ajali ya Meli ya *MV. Spice Islander*, wakiwemo wanawake na watoto wengi waliopoteza maisha yao".

Mhe. Naibu Spika, nataka nimuulize Mhe. Waziri, wakati yeye ni mama na hii wizara yake inashughulikia wanawake na watoto. Je, inatosha kuipongeza serikali na kupongeza Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais.

Sasa basi nimuulize yeye kama wizara yake alijipanga vipi kuwasaidia hawa watoto na wanawake, ambao walikuwa wengi waliopata matatizo wakati wa kuzama kwa meli ile, kwa hiyo naomba aje anieleza hapa kwamba alifanya angalau kisomo kwa wale waliotangulia mbele ya haki katika msiba huu.

Kwa hiyo, namuomba Mhe. Waziri wakati atakapokuja kufanya majumuisho naomba anieleze, na sisi tumeamini kwamba ni mama yetu ambaye anatushughulikia watoto pamoja na wanawake ambao walikutwa na msiba huu.

Mhe. Naibu Spika, nikiendelea na mchango wangu niende kwenye ukurasa wa 9 naomba kunukuu kidogo Mhe. Naibu Spika. "Wizara imefanya mapitio ya Sheria ya Mahakama ya Kadhi ya mwaka 1985, ili iendane na hali halisi ya mabadiliko ya dhana ya usawa wa jinsia bila ya kukiuka misingi ya Dini ya Kiislamu".

Mhe. Naibu Spika, napenda kumuuliza Mhe. Waziri kwamba hiyo misingi ya Kiislamu ni ipi iliyokusudiwa hapa na pia katika hiyo misingi iliyokusudiwa itafuatwa misingi yote au baadhi tu ya misingi ya Dini ya Kiislamu?

Vile vile niende kwenye ukurasa wa 33 kuna suala ambalo mara nyingi naweza kusema labda ni nyimbo ambayo imeshazoeleka katika hili Baraza, Mhe. Naibu Spika naomba kunukuu kidogo. "Wizara ilifanya ziara katika taasisi za kifedha na *SACCOS*, ili uzoefu juu ya kuendesha mchakato wa uanzishwaji wa Benki ya Wanawake. Hadi hivi sasa tayari Mtaalamu Muelekezi kwa ajili ya kufanya tathmini ya uanzishaji wa Benki hiyo ameshapatikana na ameanza kazi katika hatua za awali".

Mhe. Naibu Spika, naomba kumuuliza Mhe. Waziri kwamba huyu mtaalamu anatoka nchi gani, na ilivyokuwa suala hili limekuwa kama ni nyimbo. Kwa hiyo, namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Naibu Spika wakati atakapokuja kufanya majumuisho anieleze ni lini hasa benki hii itakuwa tayari?

Suala jengine niende kwenye Idara ya Ustawi wa Jamii. Kwanza nimpongeze Mhe. Waziri kwa kuwekwa uzio sehemu ile ya wazee, kwa sababu kuwekwa uzio ule tayari yale madhara yaliyokuwa yakitokea pale yameshakuwa ni kinga, waswahili wanasema "*Nyumba isio na mlango kila mtu huingia, mwanzo huingia jibwa na paka hufuatia*". Kwa hivyo, hali ile hivi sasa imeshakuwa ni stara na ninakupongeza Mhe. Waziri. *(Makofi)*

Sambamba na hilo kuna suala zima la wazee wale wa Sebleni tumeweka kwamba ni kuwaenzi wale wazee wetu, na katika kuwaenzi wale wazee wetu basi tumejitahidi kuwawekea huduma mbali mbali. Lakini pamoja na huduma tulizowawekea Mhe. Waziri bado wazee wale wanataka huduma, kwa sababu mtu anapokuwa mzee ndio ameshakuwa mzee na kuna huduma za lazima azipate, wakati wowote kuna maradhi ya kila aina yanamnyemelea tena wakati wowote yanakuwa maradhi, na mwaka jana nililizungumza kwenye bajeti hii Mhe. Naibu Spika.

Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Naibu Spika, suala hili aje anijibu wakati atakapokuja kwa bajeti hii, kwa sababu mwaka jana nilizungumza na alinijibu lakini sikuridhika, kwani nilikuwa sijafundishwa kuzuia fungu na sasa nimeshafundishwa Mhe. Naibu Spika. *(Makofi)*

Kwa maana hiyo, naomba Mhe. Waziri aje anijibu pale kwenye Nyumba ya Wazee Sebleni kuna chumba cha daktari na nilizungumza kwamba wazee wale maradhi yanaweza kuwakuta saa 8 au 9 za usiku na kumtoa mzee yule kwa ajili ya kumpeleka hospitali ya nje. Lakini ikiwa daktari yumo mule ndani basi itakuwa umemrahisishia na mtu akishakuwa mzee maungo yote yanauma.

Je, suala hili limefikia wapi Mhe. Waziri, wakati mule ndani kipo chumba cha daktari, hivyo ni vyema kuweka daktari pamoja na kupatiwa dawa na kwa ajili ya kupatiwa huduma mule ndani, ikiwa saa 8 au 9 za usiku akishikwa na homa basi anapatiwa huduma, huku nako pia ni kumrahisishia mzee huyu na kumuepusha na matatizo.

Mhe. Naibu Spika, namuomba Mhe. Waziri aje anijibu suali hili, kwa sababu naona kumfanyia mzee huyu na kumuhangaisha kama hivi na wakati tuko tayari kuwaenzi wazee wale na hii ni huduma yao ya muhimu. Kwa hivyo, naomba kujua Mhe. Waziri kwamba hili limefikia wapi?

Sambamba na hili kwanza serikali niipongeze kwa kuwaona na kuwazidishia kuwapa hichi kima wazee cha kuwakimu kimaisha. Lakini Mhe. Waziri kuna wazee ambao wako majumbani, ambao walikuwa wakilipwa shilingi 5,000/=. Kwa kweli shilingi 5,000/= Mhe. Waziri nadhani sijui kwa matumizi ya kutwa utanunua kitu gani, hii haitoshi na wala haikidhi haja hata kidogo.

Kwa hivyo naomba na wazee hao watizamwe kama mpango ule wa kulipwa hawa wazee, kwa sababu kuna wazee wengine walifutwa majina yao hasa sehemu ya Wete walifutwa majina yao.

Kwa maana hiyo, kama upo ule mpango wa kusaidiwa hawa wazee ambao wako majumbani, Mhe. Naibu Spika naomba hii shilingi 5,000/= itizamwe kwa makini, yaani kiasi hiki cha fedha hakikidhi chochote hata ukimpa yule mtoto mdogo kwenda dukani na kurudi basi imeshakwisha. Mhe. Naibu Spika, nadhani vyema tukaliangalia kwa makini suala hili.

Mhe. Naibu Spika, nikiondoka hapo sasa nije kwenye Idara ya Vijana. Kwa kweli kama nilivyosema kwamba wizara hii huyu mama anao mzigo mkubwa, kwa sababu anao vijana, wanawake, watoto pamoja na wazee. Kwa upande mmoja ukiingia kwenye *Tauhid* ni wizara ambayo iliyopandishwa daraja na Mwenyezi Mungu, kwa sababu tukija kila nyanja basi Mwenyezi Mungu amemtukuza.

Kwa mfano, mzee Mwenyezi Mungu amemtukuza anamuonea haya, ukaja kijana ambaye ni Mchamungu Mwenyezi Mungu anamuonea haya, mtoto na hata mwanamke mwenye kumtii mumewe, basi Mwenyezi Mungu anamuonea haya. Kwa hivyo, hii ni Wizara ambayo naweza kusema kwamba ni wizara iliyotukuzwa. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, ikiwa hii ni Wizara inayoshughulika na vijana, mpaka hivi sasa kuna vijana wetu ambao wameshughulika na dawa za kulevya, suala hili linatusakama. Pamoja na kwamba suala hili liko katika Wizara ya

Nchi, Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais, wakati na Mhe. Waziri wa Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto naye anashughulika na vijana.

Je, Mhe. Waziri wizara yako juu ya mashaka haya waliyonayo vijana wetu, una mkakati gani ili kuwasaidia vijana hawa kwa ajili ya kuondokana na tatizo hili. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Naibu Spika, wakati atakapokuja kufanya majumuisho na hili nalo aje anisaidie.

Vile vile kuna vijana wetu wengi ambao wanazurura hawana kazi. Mhe. Naibu Spika, katika suala hili la vijana Mhe. Waziri anawasaidia vipi, kwa sababu vijana wengi sana wanahangaika tu hawana kazi yoyote ndipo mwisho wanaingia katika dawa za kulevya. Kwa hivyo, Mhe. Waziri anawasaidia vipi vijana hawa ambao hawana ajira yoyote.

Sasa nije kwenye Idara ya Wanawake na Watoto kuna suala zima la upoteaji wa watoto na wala sitaki kuzungumza mambo ya udhalilishaji na hayo tumezungumza sana. Kwa kweli kuna upoteaji wa watoto, kuna watoto wanaopotea na wala hazijulikani taarifa zao, lakini kuna watoto wanapotea na baadae mtoto huyo ameshapatikana na alimchukua bibi fulani na taarifa zinatolewa zote. *(Makofi)*

Kwa mfano, kama hivi karibuni aliibiwa mtoto Hospitali ya Mnazi Mmoja, kwa bahati mtoto yule amepatikana amerejeshwa. Lakini mwanamke yule aliyeiba yule mtoto hatukujua hukumu yoyote iliyochukuliwa, yaani hatukujua taarifa yoyote ya hukumu ya mwanamke huyu au hatua iliyochukuliwa, kwa sababu anapofanya mtu jambo ikiwa hakuchukuliwa hatua basi na mwengine anazoea, isipokuwa tunasikia tu yupo kwake Bububu *bukheri khamsa wa ishirini*. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, namuomba Mhe. Waziri atueleze na suala hili la kupotea watoto lipo kama mchezo ambao umeanza zamani. Kwa hivyo, naomba Mhe. Waziri atueleze suala hili, kwa sababu unaweza kusikia tu mtoto fulani amepotea na baadaye hupati taarifa kama mtoto yule ameonekana ama taarifa zake ziko vipi.

Sasa huyu ambaye alipatikana na kuchukuliwa na mchukuaji naye alipatikana, lakini hukumu gani ilitolewa kwa huyo ambaye alimchukua huyu mtoto na alimchukua kwa madhumuni gani. Kutokana na hali hiyo, namuomba Mhe. Waziri aje atusaidia na suala hili.
Mhe. Naibu Spika, suala jengine la mwisho ni kwamba Mhe. Waziri anayo majukumu mengi katika wizara yake, kwa sababu Mhe. Waziri anayeshughulikia wanawake, watoto, vijana na wazee. Kwa kweli ukimchukua huyu mwanamke tu basi ana jukumu kubwa mno na tafauti na mwanamme, kwa sababu anakuwa na mambo makubwa.

Kwa hivyo, naomba bajeti aliyopewa wakati wa bajeti atizamwe sana mama Mhe. Zainab Omar Mohammed, kwa sababu anashughulika nao watu wote ni wazito. Kwa maana hiyo hichi alichoomba apewe chote atizamwe sana katika bajeti yake. *(Makofi)*

Baada ya hayo, Mhe. Naibu Spika naomba niunge mkono Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto, mama mlezi pia ni kipenzi chetu kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Mjumbe, ahsante na sasa nafasi tunampa Mhe. Ismail Jussa Ladhu, ajiandae Mhe. Hamza Hassan Juma na baadae Mhe. Wanu Hafidh Ameir.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipatia fursa hii. Naanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu *Azza Wajalla* kwa kutujaalia Ijumaa ya leo jioni hii tukiwa hai, wazima bukheir wa afya tunaendelea na mjadala wa bajeti za wizara mbali mbali.

Mhe. Naibu Spika, uniruhusu pia nimpongeze Mhe. Waziri wa Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto kwa uwasilishaji wake mzuri wa hotuba ya bajeti ya wizara yake kama alivyosema Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak hivi punde. Kwa kweli Mhe. Zainab Omar Mohammed amepewa wizara muhimu katika kulea makundi muhimu kwenye jamii yetu. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, na mimi nitoe mchango wangu katika maeneo machache kwenye wizara hii. Jambo la kwanza kabisa ambalo nimeliona mimi wakati nilipokuwa nikimsikiliza Mhe. Waziri nikiangalia shughuli ambazo

zinafanywa na Wizara yake, na halafu nikiangalia na shughuli ambazo zinafanywa na Wizara ya Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika napata mashaka Mhe. Naibu Spika. *(Makofi)*

Kwa kweli unaona wazi wazi kwamba kazi kwa kiasi kikubwa ndio zile zile. Kwa mfano, ukisema kwamba kwa Mhe. Zainab Omar Mohammed kuna masuala ya wanawake, vijana, na ukienda kwa Mhe. Haroun Ali Suleiman, yeye anazungumzia uwezeshaji wa wananchi kwa ujumla wake, ambapo makundi hayo yamo ndani, labda kilichokuwa tofauti ni suala la watoto.

Mhe. Naibu Spika, mimi nataka nitumie fursa hii kutoa wito au ushauri niseme. Najua kwamba jukumu la kupanga wizara kikatiba ni jukumu la Mhe. Rais, lakini Baraza hili ndilo lililopewa dhamana ya kupitisha matumizi ya fedha za walipa kodi wa Zanzibar. Vile vile tunalo jukumu Mhe. Naibu Spika, kuona kwamba fedha hizi zinatumika vizuri, na kiasi kikubwa kikienda katika kuwahudumia wananchi wenyewe. *(Makofi)*

Sasa Mhe. Naibu Spika, hili linalipa mashaka, kwa sababu unaweza ukawa unahudumia makundi yale yale na shughuli unazofanya ni zile zile, lakini gharama za utawala ambazo mara nyingi katika Wizara ndio kubwa kuliko shughuli za maendeleo unakuta zinajirejea mara mbili basi na sababu. *(Makofi)*

Kwa hivyo, nimuombe sana Mhe. Rais wetu na ninamshauri kwamba hebu aangalie haja ya kuziunganisha tena wizara hizi mbili kama zilivyokuwa zamani. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, hata ukiangalia ufanisi wa kazi, na kama nilivyosema kwamba hili simwambii Mhe. Waziri kwa sababu si jukumu lake, imeundwa wizara na yeye amepewa jukumu la kumsaidia Mhe. Rais katika eneo hili.

Lakini naiambia serikali na hasa natoa ushauri kwa Mhe. Rais na kwa wale wanaomsaidia, kwamba ukitazama bajeti za wizara hizi mbili Mhe. Naibu Spika, wizara hii Mhe. Zainab Omar Mohammed ametuomba tumuidhinishie shilingi bilioni 3,915,000,000/= kwa shughuli za kawaida na zile za maendeleo.

Nikiangalia na hili Buku la Makadirio Wizara ya Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika, itakuwa kutuomba hapa Mhe. Naibu Spika shilingi bilioni 4,134,000,000/=. Kwa hivyo, ukizichanganya hizi Mhe. Naibu Spika, takriban ni zaidi kidogo ya bilioni 8.

Mhe. Naibu Spika, hizi zingekuwa pamoja zingeokoa lile fungu ambalo linalokwenda katika utawala, na badala yake kiasi kikubwa ungeona pengine kingeweza kufanya ile shughuli ambayo Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak kwamba angeongezewa bajeti angelifanya shughuli muhimu zaidi.

Kwa kweli suala hili Mhe. Naibu Spika, nataka litizamwe kwa undani wake katika masuala ya mipango ya nchi. Kutokana na hali hiyo inawezekana kabisa ikawa kwa utaratibu wa serikali zetu zinavyofanyakazi ikawa vikundi vile vinavyokwenda Wizara ya Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto, basi vile vikawa vinakwenda katika Wizara ya Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika na vikawa vinafaidika mara mbili wakati kuna vikundi vyengine havipati.

Lakini kama ingelikuwa ni Wizara moja, basi ingeweza kuratibu vizuri zaidi na kujua vikundi gani vinasaidiwa na kwa uwiano gani katika maeneo tofauti ya nchi yetu.

Kwa hivyo, hili Mhe. Naibu Spika nimeona niliseme kama nilivyosema kwamba natambua tena naheshimu kabisa kuwa Katiba yetu imetoa madaraka kwa Mhe. Rais, lakini chombo hiki cha Baraza la Wawakilishi jukumu lake moja ni kuishauri serikali juu ya namna bora ya matumizi ya fedha za walipa kodi na kuzisimamia, naamini zitasimamiwa vizuri zaidi fedha za walipa kodi ikiwa tutaweza kufikiria kuzichanganya wizara hizi mbili kama ilivyokuwa zamani. Mhe. Naibu Spika, hilo ni eneo langu la mwanzo ambalo nilikuwa nataka nilitolee maoni.

Eneo la pili Mhe. Naibu Spika, sasa naomba niende kwenye hotuba ya Mhe. Waziri. Mhe. Naibu Spika, tulisema hapa nadhani tulipokuwa tukiichangia Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, kwamba tuna tatizo la kuona wizara za serikali zinatuletea miradi ile ile ambayo imeshamalizika kila mwaka wa fedha. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, katika kitabu hiki ukitizama malengo ya mwaka jana ni kufanikisha kumalizika kuundwa kwa Baraza la Vijana Zanzibar. Tukiangalia mwaka huu jukumu lake ni kuratibu uanzishwaji wa Baraza la Vijana la Zanzibar. Sasa najiuliza mwaka mzima uliopita hapajakuwa na kitu. *(Makofi)*

Katika maelezo hupati ukaambiwa kwamba angalau katika mwaka kulifanyika kitu kadha katika kufanikisha hilo lengo la kukamilisha uundwaji wa Baraza la Vijana, sasa mwaka huu limerejea tena na hili linatupa mashaka Mhe. Naibu Spika.

Vile vile unakuta mwaka jana ni kusimamia kuanzishwa kwa Benki ya Wanawake, na mwaka huu tena katika malengo kusimamia kuanzishwa kwa Benki ya Wanawake.

Sasa najua kuna hatua nyingi za kupita, basi angalau tungeoneshwa kwamba kwa mwaka jana kimefanyika hiki, lakini hayaonekani Mhe. Naibu Spika, haya kidogo yanatupa mashaka. Kwa kweli sisi tunayasema haya kwa nia njema kabisa katika kuwasaidia Waheshimiwa Mawaziri wetu tunawapenda na tunajua wamebeba dhamana nzito, kwa sababu kuongoza wizara si kazi nyepesi hasa katika nchi zetu kama hizi masikini.

Lakini ninachosema tuone basi kuna *movement* au maendeleo (*progress*) katika hatua ambazo zinapigwa Mhe. Naibu Spika, kwa sababu mwaka mmoja wa fedha si kipindi kifupi. Kwa hivyo, hayo nilikuwa nataka kumwambia Mhe. Waziri kwamba ayatizame.

Mhe. Naibu Spika, eneo jengine ambalo napenda nilizungumze ni eneo la haya makundi na jinsi yanavyosaidia, kwanza ni kuji-*organize* kujumuika pamoja katika vikundi mbali mbali kujitolea na baadaye kupatiwa ajira ziwe za muda au za kudumu.

Mhe. Naibu Spika, nataka kusema tena kwa nia safi kabisa kwamba mwaka juzi tuliamua kubadilisha mfumo wetu wa siasa katika nchi yetu kuja katika Mfumo wa Umoja wa Kitaifa, kwa lengo la kuziunganisha nyoyo za Wazanzibari. Lakini Mhe. Naibu Spika, hatuwezi tukaziunga nyoyo huku juu na ikawa huku chini hatusaidii kuziunganisha.

Kwa mfano tunaona tunapokuja kuripotiwa utekelezaji hapa vikundi mbali mbali hapa, lakini husikii kutangazwa hizi fursa, sasa unapata wasi wasi kwamba kuna vikundi au makundi fulani ndiyo ambayo yamelengwa na ukitizama mjumuiko wake Mhe. Naibu Spika huachi kuona kwamba vina mrengo fulani wa kisiasa.

Sasa mimi nasema kama tumeamua kujenga umoja Mhe. Naibu Spika, basi tujenge katika kila ngazi na hasa huku chini kwenye wananchi, naomba sana hilo. Kwa kweli kuna vikundi Mhe. Naibu Spika Zanzibar ndogo tunajuana, tunaviona vinaanzishwa kupitia katika mrengo fulani halafu vinapewa huduma ya kujitolea na baadae vinaajiriwa. Kutokana na hali kama hiyo, ndipo tunapopata malalamiko kwamba sisi katika fursa kama hizo wa upande mwengine hatupati fursa hizo.

Kwa hivyo, kama ingekuwa zinatangazwa na watu ikawa wanashindana kwa mujibu wa vigezo na sifa zao, basi nadhani ingelikuwa ni rahisi kabisa kuona kwamba kuna uwazi na wala hakuna mtu ambaye angelalamika. Mhe. Naibu Spika, na hili niliona pia niliseme kwa ajili ya kuliangalia sana, kwa sababu linajenga zile dhana na inawezekana si kweli Mhe. Naibu Spika, lakini kama taswira inayojengwa ndio hiyo.

Kwa mfano, wataalamu wa *science* wa siasa wanasema. "*Politics is a game of perception*", yaani siasa ni mchezo wa hisia, kwa sababu inawezekana hata si kweli, lakini zile hisia tu zinajengwa na ukizijengea mazingira, basi zinatoa nguvu katika imani fulani ambazo tunakuwa nazo. Mhe. Naibu Spika, naomba suala hili kwamba viongozi wanaoziongoza hizi na hasa zile zinazotoa huduma kama hizi, watizame na waone kwamba makundi yote katika jamii yanafaidika kwa uwiano unaoweza kukubalika.

Mhe. Naibu Spika, eneo jengine ambalo nataka nilizungumzie kwenye Sheria ya Mtoto. Mhe. Naibu Spika, mwaka jana tulipitisha sheria hapa tena baada ya mbinde si ndogo, nafikiri kule kwa kina Mhe. Othman Masoud wangesema papatu ilikuwa si ndogo au kikwacha kilikuwa si kidogo. Tulibuburushana lakini mwisho Mhe. Waziri alitufanyia na semina na kutuonesha uzuri wa sheria na baadae tukaipitisha.

Mhe. Naibu Spika, atakumbuka Mhe. Waziri wakati nilipokuwa nikichangia katika mswada ule nilitahadharisha sana juu ya kubebeshwa dhana ambazo si zetu wengine. Kwa mfano, nilisema ni muhimu kulitizama, kwa sababu kila jamii inapotunga sheria inajitizama ile jamii yenyewe ilivyo maadili, historia, na utamaduni wake.

Mhe. Naibu Spika, moja ambalo tulitilia mkazo sana kwa wakati ule na Mhe. Waziri alitukosha katika kuwasilisha mswada, kwenye semina na wataalamu wake aliotuletea kwamba sheria ile ni tofauti na sheria za kwengine, kwa sababu haizungumzii tu haki za mtoto, pia inazungumzia wajibu wa mtoto, tulisema hilo kwa jamii kama wetu ni muhimu sana.

Lakini sasa Mhe. Naibu Spika, napata wasi wasi kwamba kumbe inawezekana tuliingiziwa vifungu vya wajibu, ili turidhike tu na sheria ipite. Kwa kweli katika ripoti za utekelezaji unarudi pale pale, kwamba uzito na msisitizo kila wakati ni haki za mtoto, ripoti katika hotuba kama hizi pamoja na ripoti nyengine kuhusu wajibu nao umetizamwa kiasi gani na wala hakuna ripoti hiyo.

Mhe. Naibu Spika, inaonekana hasa kwamba *focus* ya tathmini ya utekelezaji wa sheria imerudi pale kwenye haki kuliko upande wa sarafu ambao ni wajibu. Mhe. Naibu Spika, katika jamii zetu hizi haki na wajibu ni watoto pacha. Kwa hivyo, nasema na hasa kwa watoto, kwa sababu hapo ndipo tunapojenga jamii yetu.

Mhe. Naibu Spika, nilisema wakati ule kwamba ukienda katika nchi za wenzetu na wao wenyewe leo ukisoma tathmini zao wanajutia kutoa uhuru usiokuwa na mipaka katika jamii zao kwa watoto wao, kwamba leo wanasema wenyewe zime-*destroy* ile *moral fabric of the society,* yaani zimevuruga ule msingi wa kimaadili wa jamii zile. Kwa mfano, leo katika maskuli hakuna nidhamu katika nchi zao, katika familia hakuna nidhamu katika nchi zao na hata katika jamii hakuna nidhamu katika nchi zao.

Mhe. Naibu Spika, lilipotokezea vurugu nafikiri mwaka jana Uingereza kulikuwa na machafuko makubwa. Walipojitathimini hawakutizama mambo ya jumla jumla lakini pia walitizama msingi wa maadili. Ilikuwa wanajiuliza je, hivi tunavyo kweli ni sawa sawa. Nasema hata kitabu hichi cha bajeti kama vilivyokuwa vyengine. Bado *focus* ya ripoti yetu ipo kwenye haki, kwenye wajibu kama vile tulivyoingiza ndani ya sheria ili sheria ile ionekane kwamba tumetekeleza pia matakwa ya wananchi wa Zanzibar kwamba tunayo yote mawili. Lakini katika utekelezaji bado kabisa hakuna uwiano katika kuyatizama haya mambo mawili.

Nilikuwa naomba nitoe ushauri kwamba Mhe. Waziri alitizame katika Wizara yao wanapolitazama hili. Tusiwe wa kubeba ajenda za watu tu, tukaja tukafikia kule ambapo wamefika wenzetu ambalo leo wanakulalamikia na sisi wakatupeleke kule halafu tukaja tukajuta wakati majuto ni mjukuu.

Mhe. Naibu Spika, ukiacha hilo, Mhe. Jaku Hashim Ayoub alipokuwa akichangia asubuhi alizungumzia, naomba na mimi nilizungumzie kwa ufupi suala la matukio haya ambayo yanaongezeka. Masuala ya udhalilishaji hasa ubakaji, kulawitiwa, mvutano wa malezi, kukashfiana, kila pahala katika kesi za watoto yanaongezeka, haya katika jamii yetu ilikuwa ni mambo ya nadra sana kuzungumzwa. Nilikuwa naomba Mhe. Waziri aje atusaidie kwamba amefikia hatua gani.

Katwambia kwamba Baraza la Mapinduzi limeunda kamati ndogo kufuatilia suala hili. Wameamua kwenye kufanya utafiti. Mimi nilikuwa nadhani kwamba hali halisi inajulikana ndio maana ikaundiwa kamati kwenda kushughulikia kwamba hili tatizo limekuwa kubwa. Tukisema kwamba tunaunda Kamati tukajiridhishe au tufanye utafiti tukajiridhishe kwamba hili tatizo ni kubwa kiasi gani, kidogo linanipa mashaka, labda Waziri aje anisaidie. Kwani ile tahadhari ilikuwa kubwa kiasi gani mpaka kufanya chombo kikubwa cha maamuzi ya Sera na uendeshaji wa nchi hii Baraza la Mapinduzi, ikaundwa Kamati kwenda kufatilia tatizo hili. Mimi nilidhani kwamba walishaona ukubwa wa tatizo, ili kidogo aje atusaidie.

Mhe. Naibu Spika, vile vile hapa pamezungumzwa kwamba kuna haja ya kuona kuwa kuna msukumo. Huwezi kuingilia mfumo wa Mahakama katika kufanya kazi yake. Lakini tunachukua hatua gani kuona kwamba kesi hizi ushahidi wake hauvurugwi, utaratibu wake hauingiliwi na rushwa na kwamba hatimaye haki inatendeka ili kutoa funzo kwa wengine kwamba mambo kama haya yasije yakajirejea. Nilikuwa naomba na hilo pia akija ajeanisaidie.

Mwisho katika kitabu cha bajeti nilikuwa nataka kusema kitu kimoja kidogo lakini nadhani ni muhimu. Mhe. Naibu Spika, Wazanzibari wameshasema sana juu ya kuchoka kuendelea kuporwa mamlaka yao. Yaliyoporwa tunataka

tuyarejeshe, seuze kuyachukua mengine tukayapeleka. Katika ufahamu wangu sikumbuki miye kama katika masuala ya wanawake, vijana, watoto, kwamba haya yamo katika orodha ya muungano.

Mhe. Naibu Spika, sisi tumetangaza na tumefanya marekebisho ya katiba kusema kwamba Zanzibar ni nchi. Kama ni nchi na kwa mambo yasiyokuwa ya muungano kwa mujibu wa mkataba wa muungano kwa mujibu wa katiba ya muungano, kwa mujibu wa Katiba yetu ya Zanzibar tuna mamlaka kamili katika maeneo hayo.
Mhe. Naibu Spika, kidogo waziri kanitia mashaka kwamba katika kitabu chake ukurasa wa 33 anatwambia kwamba, "Tarehe 8 Marchi ya kila mwaka, nchi yetu huungana na nchi nyengine duniani kwa kuadhimisha siku ya wanawake duniani ambapo kwa mwaka huu ujumbe wa maadhimisho hayo ulikuwa ni "**Ondoa ukatili dhidi ya Wanawake Tanzania"**

Nikasema sisi tunaadhimisha siku ya wanawake ya Kimataifa lakini tupo Zanzibar. Je, tunatatizo kubwa kiasi hicho hapa Zanzibar, maana isiwe tunajikumbizia matatizo ya wenzetu na sisi ikawa ni kauli mbiu. Pengine wao kwa mila zao na jinsi walivyokulia na walivyotokea ukatili wa wanawake wengine ni sehemu ya mila zao. Kuna jamii kule kama hujapigwa wanasema hujapendwa bado na bwana. Tena sio kipigo unachokijua wewe Mhe. Naibu Spika, kipigo hichi cha kupiga hasa. Nilikuwa nasema kama ni hivyo wao inawezekana kauli mbiu hii ikawa sahihi kwa sababu wana kabili tatizo walilokua nalo, lakini kwa Zanzibar *focus* pengine ingekuwa nyengine.

Mhe. Naibu Spika, kwa haya mambo yasiyokuwa ya muungano hebu tusiendelee kujikumbiza. Tunataka yaliyochukuliwa tuyarejeshe ili tupate mamlaka yetu, sikwambia tena kuchukua mengine tukawapelekea, hata ya wanawake tena. Mimi naamini Mhe. Zainab ana uwezo mzuri kabisa ndio maana tukaibakisha katika Zanzibar na akapewa kuiongoza Wizara hii, kwa hiyo tusiipeleke huko Mhe. Naibu Spika. Nilikuwa naomba hilo tulitizame.

Mhe. Naibu Spika, nende katika hiki kitabu kinachotia homa siku hizi cha manambari. Mhe. Waziri katugaiya marekebisho, kama alivyosema mjumbe mmoja asubuhi kwamba inawezekana sasa hivi ikawa ndio utaratibu kila anayekuja anatupa marekebisho. Si tatizo, lakini nilikuwa naomba katika hayo marekebisho aliyotuletea atusaidie, kuna vifungu mimi bado vinanipa mashaka.
Kwanza ukurasa wa mwanzo kwenye Afisi Kuu Pemba. Vote 220200 Viburudishaji. Kuna sub vote 220201 Chakuna na Vinywaji. Mwaka jana ilikuwa laki nane, hamsini na tano elfu (855,000) mwaka huu kumi na tatu milioni (13,000,000) habu nilikuwa naomba aje anipe maelezo. Kwa sababu kama tunaambiwa kwamba haya ni kwa sababu ya Semina. Semina hazijaanza mwaka huu tu, kwa nini kunakuwa kuna kupanda kwa kasi kwa mafungu haya tuliyokuwa tunayataja kila wizara.

Eneo jengine nilikuwa naomba niliuliza katika Wizara iliyokuwa tumemaliza hapa na katika Wizara hii naliuliza tena. Ukurasa wa pili katika vote 220500 Vifanya na Huduma za Ofisi. Kuna ada ya ushauri, mimi ninavyodhani *consultancy fees* mara nyingi inahusu mara ya sera na mambo ya *organization* kwa jumla ambayo yanafanywa kupitia Makao Makuu ya Wizara. Sasa unapokuwa na fungu hili kwa upande wa Afisi Kuu Pemba najiuliza wao pia wanakuwa na *consultancy* yao tofauti inayofanywa na Makao Makuu ya Wizara. Kwa nini kuwe na fungu lile ambalo hapa lipo milioni mbili laki tano, hamsini elfu (2,550,000).

Mhe. Naibu Spika, vile vile naomba anisaidie katika fungu la Idara ya Mipango Sera na Utafiti kwenye Vote 211100 kwenye Mishahara ya Fedha Taslim. Kuna *vote* ndogo pale inazungumzia, Malipo ya Kujikimu na Malazi peke yake ni shilingi ishirini na mbili milioni, laki nane, thamanini elfu per DM peke yake ni (22,080,000) hii kwa Idara moja tu Mhe. Naibu Spika, sio la Wizara hili. Maana kuna Idara ya Uendeshaji mbali. Hili la Idara ya Mipango, Sera na Utafiti. Kuna fanywa shughuli gani hata ikawa malipo ya kujikimu na malazi kwenye fungu la mishahara sio fungu la safari likawa ni 22 milioni, hebu tusaidiwe hili Mhe. Naibu Spika.

Katika Idara hiyo hiyo pia niulize tena katika fungu la viburudishaji kuna shilingi ishirini na nne milioni, laki nne sabini na tano elfu (24,475,000) kwenye chakula na vinywaji, kwenye semina. Halafu katika fungu la jumla la viburudishaji ni shilingi milioni kumi na nne, lakini nne sitini na tano elfu (14,465,000). Jumla hapa ni shilingi thalathini na nane, milioni laki tisa arubaini elfu (38,940,000) kwa mwaka mmoja na kwa Idara moja. Nilikuwa naomba akija Mhe. Waziri aje anisaidie.

Mhe. Naibu Spika, vile kwenye fungu la safari la Idara ya Mipango Sera na Utafiri. Jumla ya fungu hili Nam. 220300 pana tisini na tatu milioni, laki mbili thamanini elfu (93,280,000) naomba Mhe. Waziri akija anisaidie. Pia katika *consultancy fees* katika fungu 220500 kuna thalathini na moja milioni, laki mbili (31,200,000) na juu huku

kuna milioni kumi na nne laki sita elfu tano (146,005,000) naomba fungu hili pia akija anisaidie maelezo. Naamini watendaji wake watakuwa wanamsaidia kuchukua maelezo.

Mhe. Naibu Spika, vile naomba akija anisaidie katika Idara ya Wanawake na Watoto katika ukurasa wa saba kwenye fungu la gharama za safari kuna jumla ya kumi na saba milioni na thamanini elfu (17,080,000). Vile vile kuna Ada ya Ushauri ni ishirini na tano milioni, laki tano (25, 500,000) kwenye vote 220500. Kila idara ina fungu lake la *consultacy fees* wakati Idara hii yote takriban iko katika jengo moja na shughuli zake zinafanyika pengine zimegawika kiidara lakini kwa ujumla zinafanana.

Mhe. Naibu Spika, nende katika Idara ya Maendeleo ya Vijana. Hapa pana malipo baada ya saa za kazi. Hili nataka akija anisaidie Waziri. Malipo baada ya saa za kazi katika idara nyingi ni fungu kubwa sana la linajirejea kila pahali. Lakini kuna baadhi ya idara hazina. Sasa nilikuwa najiuliza kuna ufanyaji kazi mkubwa kiasi hicho cha kuwa na *over time* katika Wizara hii mpaka ikawa fungu hili.

Kwa mfano hapa katika Idara ya Maendeleo ya Vijana kuna shilingi kumi na moja milioni, laki mbili thamanini elfu (11,280,000). Kama ni fungu la malipo baada ya saa za kazi, mbali ya posho maalum shilingi milioni kumi na mbili, laki moja sitini na nane elfu (12,168,000). Mbali ya posho la Vikao na Kamati shilingi kumi na tano milioni, laki sita na elfu kumi (15,610,000) katika fungu hili 211100 Idara ya Maendeleo na Vijana.

Mhe. Naibu Spika, unakuta vile vile katika fungu la viburudishaji katika Idara hii ya Maendeleo na Vijana *vote* 220200 kuna jumla ya shilingi milioni kumi na sita, laki nne, thamanini na tano elfu (16,485,000). Eneo jengine ambalo linatia mashaka tungeomba maelezo akija ni kwenye Idara ya Ustawi wa Jamii. Ukurasa wa 14 lakini fungu ninalolihoji liko ukurasa wa 15 wa waraka huu, kwenye vote 220400, gharama za mafuta na vilainisho. Kwenye gharama za umeme kuna shilingi kumi na saba milioni, laki tisa sitini na nane elfu (17,968,000). Najiuliza wanatumia umeme kiasi gani kwa mwaka katika Idara ya Ustawi wa Jamii hata kuwa na fungu kubwa kiasi hichi.

Lakini pia niulize katika Idara hii kumewekwa fungu linalowahusu huduma kwa wazee. Lakini katika fungu la maendeleo kuna fungu mbali la kuhudumia nyumba za wazee. Kwa nini kuna fungu la kuhudumia wazee katika fungu la kawaida lakini pia unalikuta katika kazi za maendeleo.

Mhe. Naibu Spika, naomba vile vile akija anisaidie maelezo katika Idara hiyo hiyo ya ustawi wa jamii ukurasa wa 16 wa Makadirio haya kwenye fungu la ruzuku. Kuna *vote* 263100 Mfuko Mkuu wa Ruzuku za Watoto kuna shilingi sitini milioni, laki tano kumi na moja elfu (60,511,000). Nataka kusaidiwa ruzuku hizi huwa zinashughulika na nini, ruzuku hizi za watoto. Najiuliza kwa sababu lipo katika upande wa Ustawi wa Jamii Pemba, hapa ndio nikapata mashaka nikalihoji fungu hili.

Mhe. Naibu Spika, ukiangalia ukurasa wa 17 kwenye ruzuku hivyo hivyo Pemba imewekwa ni shilingi milioni 4 tu. Sasa najiuliza hata kwa uwiano wa idadi ya watu vipi uwe una milioni 4 kwa Pemba, lakini uwe na milioni sitini, laki tano kumi na moja elfu (60,511,000) kwa upande wa Unguja. Imeandikwa Unguja na huku imeandikwa Pemba kila moja na fungu lake. Pananipa mashaka kwa sababu huku ndio kwenye Makao Makuu ya Wizara kwamba hapa kuna chaka la watu. Nilikuwa naomba hili akija anisaidie, kwa nini hakuna uwiyano wakati wanahudumiwa watu wan chi mmoja, visiwa viwili ambavyo ni pacha vinavyounda nchi hii.

Mhe. Naibu Spika, naomba nimalizie katika Idara ya Utawala na Uendeshaji, au Utumishi na Utawala ilivyoitwa humu. Kwanza nilikuwa naomba nisaidiwe maelezo katika fungu la Posho maalum ambao lipo ukurasa wa 18 katika vote 211100 hili lina shilingi thamanini na nne milioni, laki nne thalathini na mbili elfu (34,432,000) posho maalum. Pana nini hapa?

Vile vile kwenye huduma ya mtandao wa serikali *e-government* kwenye *vote* 220100 ukurasa wa 18 pana milioni 20 wakati juu hapo hapo kuna huduma za Mtandao *Internet services* kuna shilingi milioni tano na arubaini elfu (5,040,000). Sasa najiuliza kama unatumia huduma ya *e-government* tena kwa nini uwe na fungu mbali la mtandao wa *Internet services.* Mimi ninavyojua *e-government* umeweka *fiber optic* kwa hivyo huna haja tena ya kutumia *internet* ile kuwa inalipia kwa wanaotoa huduma hizi.
Mhe. Naibu Spika, katika Idara hiyo fungu la mwisho kabisa ambalo nalihoji lipo katika ukurasa wa 19 kwenye gharama za mafunzo, kuna mafunzo ya ndani shilingi milioni 18, kuna malipo ya ada shilingi milioni 6 na misaada

ya wanafunzi shilingi kumi na tisa milioni laki tano (19,500,000). Jumla arubaini na nne milioni, laki sita kumi na mbili elfu (44,612,000). Nilikuwa naomba maelezo.

Mhe. Naibu Spika, mimi sikupata kufahamu kwamba ukiondoa Wizara ya Elimu kuna na Wizara nyengine zinatoa misaada ya wanafunzi kwa maana ya s*tudent bursaries and allowances* kama ilivyoandikwa hapa. Kama ni hivyo kwa nini serikali isiweke katika fungu moja. Mhe. Naibu Spika, baada ya kusema maneno hayo naomba niseme naiyunga mkono hoja hii ya Mhe. Waziri wa Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto, lakini naomba maelezo katika vifungu hivyo ambavyo nimevitoa. Nakushukuru Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Naibu Spika, nikushukuru kunipa nafasi hii nikachangia hotuba ya Mhe. Waziri wa Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto. Mama angu, mlezi wangu Mhe. Bi Zainab Omar.

Mhe. Naibu Spika, leo itabidi nizungumze kwa nidhamu ya hali ya juu kwa sababu Wizara hii ni muhimu. Leo asubuhi nilipoondoka nyumbani niliagana na mama watoto, nilipofika barazani, Mwenyekiti juu ya kiti alikuwa ni mama, Waziri alikuwa mama, Makatibu Mezani walikuwa mama, mpaka mbeba rungu alikuwa mama. Nategemea nikirudi nyumbani nitapokelewa na mama. Leo itabidi niwe na nidhamu ya hali ya juu vyenginevyo nitakuja kufungiwa mlango nitakaporudi.

Mhe. Naibu Spika, nataka nimshukuru sana Mhe. Waziri, kwanza nataka katika kitabu ambacho kilichoandika hichi hata kama hukusoma maelezo ukianza kugeuza huku nyuma takwimu peke yake zinajitosheleza. Mhe. Mwenyekiti, nawapongeza sana Wizara hii kwa utaalamu wao na umahiri, ukiangalia *summary* tu kitabu chote umeshakisoma.

Mhe. Mwenyekiti, jengine nataka nimpongeze sana Mhe. Waziri kwa usikivu. Nampongeza zaidi Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Wizara hii pamoja na aliyoyasema Mhe. Ismail Jussa Ladhu lakini ni wizara ambayo imepwea majukumu ya kumuenzi Marehemu Mzee Abeid Amani Karume, Rais wa Zanzibar wa Mwanzo na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.
Mhe. Naibu Spika, Mhe. Mzee Karume, ndio aliyeanzisha nyumba za wazee, ndio aliyoanzisha nyumba za watoto, kwa hivyo Mhe. Waziri kapewa kazi ya kuwaenzi. Nampongeza sana kwani nyumba za Wazee zilikuwa hali mbaya baada ya kuingia yeye na sisi kuanza kusema tu hapa aliahidi kwamba atazishughulikia. Mheshimiwa tunakushukuru sana ukiahidi unatekeleza kuwa na moyo huo huo na sisi tupo nyuma yako watoto wako.

Mhe. Naibu Spika, kuna safari moja mimi nilipokuwa wizarani pale waliwahi kuja jamaa kutoka Zimbabwe na Namibia, walikuja kufanya *research* ya namna gani huduma za jamii zinavyotolewa. Walipofika Zanzibar wakasema kumbe nyinyi mmepiga hatua kubwa sana. Walishangaa kwamba Zanzibar tumepiga hatua kwamba tuna nyumba za kutunza wazee. Lakini vile vile tuna nyumba za kutunza watoto. Bado kuyaenzi matunda ya Mapinduzi ni kuenzi fikra na maazimio na vitendo pia vile ambavyo alivifanya marehemu Mzee Karume.

Kwa hivyo tunakushukuru sana Mheshimiwa kwa moyo wako huo. Tunashukuru Mzee Karume alijitahidi sana kuwashughulikia wazee katika nyumba za Welezo. Mhe. Waziri alipoingia yeye chini ya Utawala wa Dokta Sheni akasema naimarisha zaidi Nyumba za Wazee. Naomba sana katika vipaumbele vya mwakani tushashauri sana serikali kwamba bajeti ya mwakani tuletewe mapema ili tutoe vipaumbele. Tunategemea Mheshimiwa tutakuunga mkono katika kuongozo posho la wazee waliopo Nyumba za Wazee Sebleni, hili tutalisimamia Mheshimiwa.

Mheshimiwa lakini zaidi nataka nikupongeze kuwatunza watoto. Pamoja na yote lakini tunampongeza sana Mhe. Mama Shadiya kwa kuweza kuona kwamba katika hali ya sasa hivi, watoto wanatakiwa waishi karne hii ya 21. Tunashukuru kwa kujenga Jumba lile pale Mazizini, haya mambo mengine madogo madogo naamini Mhe. Waziri atayashughulikia bila ya matatizo yoyote.
Kubwa zaidi Mheshimiwa nilipoangalia katika kitabu hichi cha bajeti katika hili buku, niliona kwamba katika Bajeti ya mwaka uliopita kutunza Nyumba Wazee, walitenga bajeti karibu milioni karibu 36. Lakini mwaka huu Mhe. Naibu Spika, wameweka bajeti milioni 105. Kwa kweli tunakushukuru sana kwa kuweza kuendelea kuwaenzi wazee wetu.

Mhe. Naibu Spika, nataka vile vile niipongeze sana Serikali yetu ya Mapinduzi Zanzibar. Hivi juzi nilivyokuwa nikichangia bajeti ya Serikali nilichangia kuhusu kadhia waliyopata wananchi wa Bambi ambao eneo lao alitaka kupewa muwekezaji kwa ajili ya kufuga ng'ombe wa maziwa. Tunashukuru baada ya kuzungumza hapa Barazani walitupigia simu kwamba tayari wamefanya utaratibu, wameitwa nyumba kubwa na tayari wameshawekewa

utaratibu wa kuendeleza eneo lile kwa utaratibu maalum. Kama ingelikuwa si hivyo ningembana Mhe. Waziri nikamwambia aelekee Bambi akazungumze na akina mama ili kuhakikisha ile rasilimali wanayoitumia basi serikali iendelee kuwaachia waitumie kwa ajili ya kuendeleza vijana wetu hasa watoto.

Siku hizi kina mama mjini shughuli zao ni miradi, lakini Vijijini shughuli zao ni ukulima na ndio hizo hizo walizotusomeshea sisi mpaka leo tukafika kusimama hapa katika Baraza lako tukufu.
Mhe. Naibu Spika, ukiangalia katika kiambatanisho Nam. 8 kitabu cha Mhe. Waziri kwa kweli hapa kidogo nasikitika. Hapa kwa kweli bado mimi nataka kusema serikali yetu tunaiomba sana, jitihada zinazochukuliwa sasa hivi bado hatujaridhika nazo kwa kuwashughulikia watoto wanaodhalilishwa.

Mimi katika bajeti ya mwaka jana nilipendekeza ili kupunguza kadhia hii mtu akishakuthibitika kabaka mtoto aoneshwe kwenye TV *at least* hii ingelipunguza. Tatizo linalojitokeza sasa hivi maeneo wanayobakwa watoto yanakuwa ni maeneo maalum. Kuna watu wanakuwa tayari akili zao wameshachanganyikiwa. Leo mtu aende pale bandarini akaangalie pale, basi akitega pale mshipi wake hawezi kunasa hata mmoja, basi lazima akaparamie vitoto vidogo. Mimi nafikiri nadhani serikali yetu iwe makini sana.

Mhe. Waziri, alizungumza kwamba Baraza la Mapinduzi limeunda Kamati ya kufanya utafiti. Mhe. Mimi naona bado tunaendelea kuzunguka tatizo tunaendelea kuliacha likapea. Nameangalia hapa katika takwimu kuna kesi katika kiambatanisho Nam. 9, kesi za udhalilishaji watoto zilizopelekwa *One Stop Center* Unguja kwa mwaka 2011/2012.

Colum ya tatu kulawitiwa, halafu kwenye *Colum* ya wanaume 61, hii Mheshimiwa hii hesabu ni kubwa kweli kweli kwa Zanzibar. Mheshimiwa mimi mwaka jana nilisema, sisi tunawalaumu wale ambao kuwa sijui nitumie lugha gani ambayo itakuwa ndie lugha ya sitiari. Wenzetu kule Kenya wanawaita wachumba wachumba, yaani wale wanaume ambao mikono yao ambayo haikazani vizuri.

Mheshimiwa wale tusiwalaumu, wale hawakuanza ukubwani, walianzwa walipokuwa watoto wadogo walikuwa wanafanyiwa vitendo vile wao wenyewe hawana akili wala hawana maamuzi. Jambo lile kama tunavyosema, kawaida mtu akishaanzwa mapema hawezi kuliacha. Letu tutakuwa tunawalaumu hawa wakubwa kumbe tuwalaumu wale wanaowaharibu.

Naomba sana Mhe. Waziri mimi nafikiri Mhe. Asha Bakari sasa hivi hayupo, angelimpa ile mikoba wakati ule alipokuwa Waziri wa Wanawake na Watoto. Mheshimiwa alifatilia kitangi mpaka jela na hakumuachia mpaka kafa. Sasa tunaomba Mheshimiwa uzi huu hebu ukamate na wewe. Hawa vitangi hawa washughulikie, wafuate kuanzia huko wanapokamatwa na wazee wao polisi. Hakikisha unasimamia wewe mwenyewe hili suala. Mimi naamini watapungua hawa, vyenginevyo watatuharibia watu.
Mimi kwa nini nikasema, Baraza la Mapinduzi sawa wameunda kamati lakini sisi kila Wizara safari hii tumeundiwa Idara ya Mipango Sera na Utafiti. Sasa wanafanya utafiti gani, maana sasa hivi tatizo kama hili limeshaandikwa ina maana hapo utafiti umeshafanyika, kazi iliyobakia kuchukua hatua. Leo ndio kwanza tunaambiwa imeundwa kamati ianze kuangalia ukubwa wa tatizo. Ukubwa wa tatizo hili sisi tunaliona kubwa na utafiti umeshafanywa, hizi hatua zilizofikia zianze kuchukuliwa.

Mheshimiwa nakuomba sana mimi kamati yangu vile vile inashughulikia na mambo ya walemavu, watu wanaonyanyaswa, Ukimwi na vitu vyengine. Naomba Mheshimiwa fanya ziara wende Ole Kianga kuna ile Kamati ya Maimamu. Mheshimiwa wametusikitikia wanasema sasa hivi udhalilishwaji wa watoto wa kiume kuharibiwa umekuwa mkubwa. Hii takwimu uliyoandika hapa ni ndogo, nenda Ole Kianga utapata takwimu kubwa zaidi.

Tatizo limeshakuwa kubwa, lazima Waheshimiwa tufanye maamuzi magumu. Kama mtu kumuhasi kama itakuwa tunakiuka haki za binaadamu na yeye tayari mtoto mwanamme umeshamchafua, nako pia si kuvunja haki za binaadamu huko. Wao bado tunawaachia tu, hebu tuwapunguze kasi kidogo. Mimi nadhani bila ya kufanya hivyo, maana yake atakaekuja akasema tunavunja haki za binaadamu tutawauliza hawa watoto je, haki zao hazikuvunjwa. Mimi nadhani tuwe *serious* katika suala hili.

Mhe. Naibu Spika, baadaye nitakuja katika mafungu yako huku. Lakini safari hii mimi naomba wenye viti wote wa kamati kuna baadhi ya maeneo tuliyoyaomba kuna fedha zimewekwa maelezo yake hayajatutosheleza. Hasa katika maeneo ya vinywaji na viburudishaji, chakula na vinywaji, tunajua chakula na soda, maji, lakini viburudishaji ni

nini? Hakuna mziki, mimi sijawahi kwenda afisi hata moja kukawa kuna mziki, mziki ndio viburudishaji. Sasa fedha hizi kama alivyosema rafiki yangu, swahibu wangu Waziri Kivuli wa Afya Mhe. Jaku Hashim Ayoub, fedha hizi kila Kamati tuziangalie. Fedha hizi zimo nyingi, tena katika mafungu ambayo hayana maelezo yakututosheleza. Mafungu haya tutayapitisha lakini katika *incubator* tunayaweka yanakwenda kuchunguzwa, kama hayana maelezo ya kutosha.

Leo Mhe. Waziri kwa kuwa leo Ijumaa na wewe ni mama angu, lakini nataka kusema Mhe. Waziri kitu cha mwanzo nataka utuletee Bango kitita hapa ili, tuchambue kilainisho, tukijue nini na nini, sijui TV nini na nini, friji ni nini na nini. Lakini Mheshimiwa wewe nakuonea haya, nakuonea huruma. Lakini Waziri atakaekuja bajeti yake kuanzia Jumatatu tunaomba atuletee bajeti ya haya mambo ambayo tunayoyahoji sana, tuletee Bango kitita. Mimi najua Waheshimiwa Mawaziri siku hizi mahodari sana. Nasikia mnakaa mpaka saa 7 za usiku kwenye *Cabinet* mnachambua, ndio tunavyotaka.

Sasa na sisi hapa tusione tabu kukesha kwa kuwa Mhe. Rais anaweza kukaa mpaka saa 7 za usiku na sisi tumuoneshe kali yetu tukae bajeti moja hapa mpaka saa 10 alfajiri, tunachambua Bango kitita kujua matumizi ya fedha za umma. Ndio uwajibikaji, tusimuachie peke yake Rais kwani na yeye ni sehemu ya Baraza la Wawakilishi, kwa nini yeye kaonesha mfano na sisi tusimuoneshe mfano wetu hili naomba niliseme. Lakini fedha hizi waheshimiwa Kamati zote tutakazoziangalia vilainisho kama hatukuridhika navyo tunazichukua tunakwenda kuhakikisha kwamba serikali tunaiambia watafute mashine ya DNA.

Mhe. Naibu Spika, kesi za udhalilishaji. Kuna kesi ya mlemavu wa akili mmoja ametiwa mimba. Mtoto sura moja na baba yake anaambiwa ushahidi bado haujapatikana. DNA imepelekwa Tanzania Bara sasa hivi ni mwezi wa kumi haijaletwa jawabu, tunaambiwa kuna foleni kubwa.

Jamani kweli Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na sisi tumeweka vipaumbele, viashiria, Mkuza, Kupunguza Umaskini, *vision 2020*, *millenium goal*, tunashindwa kununua DNA. Hapa hizi tunazozikamuakamua tunamuomba Mhe. Waziri wa Afya atutafutie *estimate* ya mashine ya DNA inauzwa kiasi gani, tutakuchangia katika bango lenu kitita kila wizara ili tununue DNA, kesi inapelekwa leo jumatatu tayari DNA imeshapatikana.

Leo Mhe. Naibu Spika, mtoto mpaka anakaribia kwenda skuli ushahidi haujapatikana. Mhe. Naibu Spika, hospitali ya Mnazi Mmoja wanalalamika madaktari, kesi nyingi lakini hakuna hatua yoyote mahakamani. Mahakamani unaambiwa lete ushahidi wa DNA, halafu hiyo DNA yenyewe ile kuihifadhi hakuna utaratibu, DNA anaizuia Polisi na hana utaalamu wowote wa kukaa na damu ile ya DNA. Tunakwenda wapi.

Sasa Mhe. Naibu Spika, mimi ninadhani wakati umefika hivi sasa tubane matumizi ili matumizi yetu tuyalenge hasa katika yale malengo yanayoathiri watoto ili kumpunguzia kazi Mhe. Waziri wetu.

Mhe. Naibu Spika, ninakwenda haraka haraka. Mimi ninataka niseme kwamba wenzangu wamezungumza suala zima la kuwakomboa wanawake. Wanawake hatuwezi tukawakomboa kwa mikopo ya AK na JK au hizi SACCOS.

Mhe. Naibu Spika, uokozi wa wanawake ni kuanzisha Benki ya Wanawake. Nakuomba sana Mhe. Waziri, una utaalamu wengi sana akina Rahma pale afisini watumie. Jana mimi niliangalia TBC usiku, nimeona mwanana pale Dar es Salaam anashughulikia Benki ya Wanawake yaani kule Bara.

Mhe. Naibu Spika, kazi rahisi tu, anakwambia mtu aje kwa sababu wenzetu Tanzania Bara mtu hana vitambulisho, anasema aje na kadi yake ya kupigia kura, aje aoneshe mradi wake tukishamjua anakaa sehemu gani, mradi wake tu sio *guarantee* ya nyumba, sio baiskeli na wala sio kitu chochote, ni ile tathmini ya mradi wake.

Mhe. Naibu Spika, watumie wataalamu wako, waende wakaonane na meneja yule wa Benki ya Wanawake aje aangalie. Mhe. Naibu Spika, nimeangalia bajeti ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mwaka huu, mfuko mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na sisi hili ambalo tunataka twende huko kwenye *priorities* au vipaumbele vya pesa za wananchi.

Wenzetu kule Bara kuna fedha zinatoka katika mfuko mkuu wa serikali wamepatiwa zile benki wanaita TIB, na hapa kwetu tutoe fungu la fedha za serikali ianzishe benki za wanawake ili tuwakomboe hawa akinamama,

tutawalaumu bure tu wanapeleka watoto wakauze maandazi, mama hana kitu, baba kamkimbia na watoto wanane atafanya nini.

Lakini tukiwaanzishia benki yao, muuza kuni atakwenda kukopa benki, muuza maandazi na wanawake watakuwa na miradi mikubwa hawa. Lakini AK na JK siku zote watalalamika, mikopo imeshatoka mingi lakini nani aliyekuwa hasa kasaidia. Lakini mwenzetu kule anasema mtu anakopeshwa mpaka shilingi milioni 30 au 30, hapa kuna mkopo wa JK na AK mtu utakayempa shilingi milioni 30 na 40, kikubwa milioni mbili, tatu, nne au tano.

Sasa benki ya maendeleo ya wanawake Mhe. Naibu Spika, ninaamini Mhe. Waziri suala hili ukilisimamia mwakani tutakuja kukupigia makofi. Lakini sio wewe tu kuanzisha, hizi fedha lazima kwanza tukutayarishie sisi. Kwa sababu Mhe. Mshimba kazungumze uende katika benki na hizi benki ni za biashara. Lazima uweke *security*, itakwenda riba itakuwa kubwa lakini benki ya maendeleo ya wanawake itakuwa inaangalia zaidi fedha zile kuwaendeleza na halafu hata kura nyinyi ndio munaotupigia nyingi.

Sisi Mhe. Naibu Spika, kuna SACCOS kibao majimboni. Yaani ule usajili tu tunaofanya kila SACCOS laki moja moja. Tushatumia zaidi ya shilingi milioni mbili au tatu lakini SACCOS zote zinazosubiri mkopo hazijapata. Lakini jee tukiwa na benki yetu ya maendeleo ya akinamama, akinamama wanapata fedha nyingi wataweza kuekeza.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Waziri kazungumza suala la vijana hawa, mradi huu wa ZASOSE na hivi sasa kwa kuwa tumeondoa tofauti zetu, tumeanzisha Serikali ya Umoja wa Kitaifa. Mimi ninadhani hivi sasa kwa jumuia ya vijana tuachane na yale mambo sijui vijana wa CUF au CCM, katika zile siasa twende lakini tunapokwenda katika maendeleo, mimi ninafikiri hii ZASOSE imeonesha mfano mzuri sana. Kwa sababu wameanzisha kwa upande wa Unguja na Pemba na hawajelenga siasa, wanakwenda kuangalia kero za vijana, nini kuwatafutia ajira.

Lakini bado Mhe. Naibu Spika, Mhe. Waziri mimi bado ninasikitika kwenye taarifa yako, wale vijana wa pale hospitali ya Mnazi Mmoja wanafanya kazi nzuri sana. Zamani anapokwenda pale wazee wetu wengine wanatoka shamba, akenda pale hospitali ya Mnazi Mmoja hata hajui *reception* wapi, daktari wapi lakini tunashukuru wale vijana hivi sasa wamevaa vile vikoti vyao, ukienda pale wanakuongoza nenda, anaangalia kule ndani kama kuna mgonjwa kachelewa anamuuliza daktari kuwa huku wagonjwa wapo wengi sana, wanatusaidia sana.

Lakini Mhe. Naibu Spika, wale hawajaajiriwa, hebu fuatilia na Waziri wa Afya umuulize wale vijana keshawaajiri? Wanapigwa kiposho pale kidogo lakini posho lenyewe hata nauli hakiwatoshi lakini wanafanya kazi kubwa.

Jengine Mhe. Naibu Spika, hawa ZASOSE mimi naomba hivi sasa mji wetu haupo katika hali nzuri, hali ni ya uchafu. Vijana wanafanya kazi ya usafi. Baraza la Manispaa na sisi tumeshawaambia waachane tena na kazi hizi ndogo ndogo za kufagiafagia watafute zile kazi kubwa. Kazi kama hizi za usafi wa mji waache wapewe ZASOSE wakubaliane kuna kodi fulani wawape ili hawa vijana waweze kuifanya hii kazi.

Na tushasema ZASOSE isije tukaiona ina sura ya kisiasa, tunataka ZASOSE iende. Haya ndio malengo ya Mzee Karume. Mzee Karume zamani sisi tulikuwa na *ASP Youth League* pale. Kwa hivyo Mzee Karume alikuwa ajira lazima upitie *ASP Youth League*. Sasa na hizi ambazo hazitaki taaluma kubwa tuwatumie hawa ZASOSE, lakini vile vile kama nilivyosema wale viongozi wasiipeleke zaidi katika siasa.

Lakini jengine Mhe. Naibu Spika, kitu ambacho ninachotaka niseme kwamba hivi sasa kuna maonesho ya Saba Saba. Mhe. Naibu Spika, naomba sana hawa wanawake waliokwenda katika maonesho ya Saba Saba, tukijaaliwa siku ya tarehe 8 wanarudi na tukijaaliwa bajeti yako tutakuwa tushakupitishia kwa murua. Naomba uwaite uzungumze nao wana matatizo makubwa.

Mhe. Naibu Spika, Wizara ya Biashara, yupo wapi Mhe. Mazrui. Wizara ya Biashara kuna ahadi yao ya Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano tokea mwaka jana waliwaambia kuwa watapewa karibu shilingi milioni mia mbili mabanda ya Zanzibar mpaka leo. Kwa kuwa leo ninasema hapa Mhe. Waziri wa Biashara utakuwa na nafasi nzuri, tena uta-*quote* maneno yangu katika hiyo barua yako utakayomuandikia Mhe. Rais wa Jamhuri wa Muungano wa Tanzania kuhusu ahadi ya wale akinamama.

Safari hii wale wamekwenda wamechajiwa kama shilingi laki mbili na sitini, lakini wamesema safari hii kidogo biashara imekuwa ngumu. Wamenipigia simu wameniambia Mheshimiwa hivi sasa asubuhi tunanunua unga gani

sijui wanapika uji wanakunywa pamoja, biashara ngumu na kila banda kule inabidi uchukue na msaidizi. Mhe. Naibu Spika, wako kule karibu hawapungui karibu 47, na hao 47 kila banda inabidi amchukue na msaidizi wake pale.

Lakini hivi sasa pale biashara imekuwa ngumu. Kwa hivyo ninaomba Mhe. Naibu Spika, hawa wakirudi safari hii waitie kidogo kwa sababu wanajitahidi lakini bado mambo yapo magumu kidogo.

Mhe. Naibu Spika, ninataka niseme kwamba ZASOSE walitueleza kwamba wana kitu cha mboga mboga. Sasa nilikuwa ninataka niulize Mhe. Naibu Spika, hiki kituo cha mboga mboga, tayari wameshakuwa na umiliki wao hawa ZASOSE au wanalimalima tu hizi mbogamboga, isijekuwa kama wakulima wa Bambi mara wakaja wakaambiwa analetwa mtu aje kufuga mbuzi.

Sasa nilikuwa naomba kama hawajamilikishwa hili eneo, kwa kuwa vijana wameshaamua kujitolea, hawakusubiri ajira ya serikali basi hili eneo wamilikishwe ili hiki kituo chao kiwe cha kudumu waendeleze shughuli zao za mboga mboga.

Mhe. Naibu Spika, kitu chengine ambacho nilikuwa ninataka nimalizie kidogo kwa sababu kama nilivyosema wizara yako hii, sisi kwa kweli buti zitakuwa ni za kukusaidia tu lakini sio za kuzuia. Nilikuwa naomba tu niende kwenye hiki kiambatanisho kilicholetwa, na hili vile vile nilikuwa naomba wizara zilizobakia haya marekebisho yaliyobakia, haya marekebisho yanayoletwa nilikuwa naomba kwanza zile kamati husika, haya marekebisho wapewe mapema ili waangalie, kwa sababu kwenye buku kubwa pengine kulikuwa kumeandikwa vyengine na mtu ameshaweka *points* zake nyengine, halafu baadae huku katika marekebisho inakuja vyengine.

Sasa mimi ninakuja katika hili fungu nambari 28 ukurasa wa kwanza kabisa - Afisi Kuu Pemba. Nimeangalia hapa katika fungu 220200 – Chakula, Vinywaji, kuna ununuzi wa zawadi na chini fungu 220203 viburudishaji.

Mhe. Naibu Spika, hapa tutahitaji maelezo lakini kama nilivyosema nilitaka leo lazima tuletewe lile bango kitita, hili kwa upande wako naomba tupate maelezo lakini wizara itakayokuja itabidi watuletee na sisi tulichambue.

Hizi fedha kwa kweli zipo nyingi. Halafu bahati mbaya mwaka jana, kila bajeti mwaka zilikuwa kidogo, mwaka huu zimeongezeka marudufu. Mwaka jana ilikuwa chakula na vinywaji ilikuwa ni shilingi laki na hamsini na tano lakini mwaka huu ni shilingi milioni kumi tatu. Sasa kidogo mtu akiangalia kwa haraka haraka anakuwa anashtuka.

Lakini vile vile katika viburudishaji haijaomba ilikuwa ni shilingi milioni tatu, na mwaka huu vile vile imekuwa milioni tatu, lakini pamoja na hayo inabidi lazima tupate maelezo. Unajua unapopata mafunzo unatakiwa uyatumie vizuri, na haya mafunzo tukiyatumia vizuri kuna bakaa kubwa safari hii itabakia katika matumizi ya serikali ili kuongezea nyama vile vifungu vilikuwa havikufikia asilimia mia moja, au tunaweza tukavifanya katika matumizi mengine ambayo tutahisi yatakuwa ni muhimu zaidi.

Mhe. Naibu Spika: Bado dakika 5.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Ahsante sasa ninakuja katika ukurasa wa 4 vile vile, kifungu hichi hichi cha 28 kifungu 220200 kimejirejea tena hapa, kinasema miaka miwili iliyopita kulikuwa hakuna kitu lakini safari hii chakula na vinywaji ni shilingi milioni ishirini na nne.

Sasa kwa kweli hiki kidogo ni kitu ambacho lazima tukishtue. Halafu vile vile katika viburudishaji mwaka jana ilikuwa ni shilingi milioni nane, mwaka huu imekuja milioni ishirini na moja laki moja na hamsini. Sasa jumla hapa karibu shilingi milioni thalathini na nane, hicho ni chakula na viburudishaji tu.

Ninafikiri ndio maana siku hizi akinamama mawizarani wanatoka mashavu kwa sababu hivyo vyakula na viburudishaji vinaleta rutba kidogo.

Mhe. Naibu Spika, vile vile katika kifungu ukurasa wa 5 fungu hili linalosema 220500 – vifaa na huduma za ofisi. Fungu hili Mhe. Naibu Spika, kuna maeneo mengine, mfano ununuzi wa mabuku umefutwa, vifaa vya kompyuta vimefuta, sijui hivi vifaa vidogo vidogo. Lakini matokeo yake ukija ukiangalia *total* huku chini kabisa imeekwa ada ya ushauri, lakini imekuja karibu shilingi milioni thalathini na moja. Sasa bajeti ya mwaka jana hapa ilipitishwa

shilingi milioni 45 lakini hivi vyengine vyote vilitajwa. Bajeti ya mwaka huu imerudi ile ile shilingi milioni 45 wakati kuna vyengine vingi vimefutwa, lakini *total* imekuja ile ile. Lakini maeneo kama haya tutahitaji maelezo ya fungu hili ninafikiri *total* yake inakuja kifungu 220500, jumla yake inakuwa shilingi milioni 45, kwa hivyo kidogo tutahitaji maelezo.

Lakini ukurasa wa 6 Mhe. Naibu Spika, kifungu gharama za mafunzo. Kifungu 221102 mwaka jana mafunzo yalikuwa ni shilingi milioni 13 ambacho mimi hiki nilikiona ni muhimu, nilifikiria labda kizidi, lakini mwaka huu shilingi milioni 4,500,000/=. Sasa kwenye viburudishaji na vilaji tumeongeza lakini kwenye mafunzo huku tumepunguza. Mimi hapa kidogo nina mashaka itabidi nipate maelezo

Haya mafunzo safari hii yatakuwa hakuna, na kwa sababu sisi tumepitisha sheria ya Utumishi wa Umma, na moja katika sheria ya Utumishi wa Umma tuwafunze wafanyakazi wetu ili wafanye kazi ipasavyo. Lakini Mhe. Waziri kutoka shilingi milioni kumi na tatu umezipunguza mpaka shilingi milioni nne. Jee hawa watu safari hii hutaki kuwasomesha. Sasa hapa pia nilikuwa ninataka maelezo kwa sababu nisiseme tu katika kuongeza, lakini katika kupunguza vile vile nikuulize vile vile.

Mhe. Naibu Spika, nikija ukurasa huo huo wa 6, kuna posho maalum. Posho maalum kifungu 21110 shilingi milioni kumi na mbili laki nne na thalathini na nane. Hili vile vile tutahitaji maelezo, kwa sababu hizi posho maalum hizi tunajua mtu katika mshahara anatiliwa kila kitu. Sasa hii posho maalum tutahiji maelezo ya ziada vile vile.

Lakini vile vile ukurasa wa 7 Mhe. Naibu Spika, kifungu 220200 kimejirejea tena hiki. Kuna bajeti iliyopita hapa, hapa kidogo imepunguzwa ilikuwa shilingi milioni kumi na nne laki moja na sabini na tano, mwaka huu imekuja shilingi milioni kumi.

Lakini vile vile mwaka uliopita viburudishaji imetoka kwenye shilingi milioni kumi na moja imekuja kwenye shilingi milioni kumi. Hapa kidogo mwaka jana ilikuwa shilingi milioni ishirini na tano lakini bado kwa kuwa ni vyakula na viburudishaji tulikuwa tunaomba maelezo ya ziada.

Lakini vile vile katika kifungu 220509 *consultant fee*. Hapa Mhe. Naibu Spika, mwaka uliopita ilikuwa shilingi milioni kumi na mbili, mwaka huu shilingi milioni ishirini na tano. Kwa hivyo munategemea labda mutapata ma-*experts* zaidi katika kuboresha wizara yenu labda mutatupa maelezo vile vile.

Lakini vile vile hapa kwenye ukurasa wa 8 kifungu 272100 – Misaada ya Kijamii. Mhe. Naibu Spika, hapa kidogo nina masikitiko. Misaada ya jamii hapa kifungu 272109 – Maendeleo ya Wanawake na Watoto. Mwaka uliopita ilikuwa shilingi milioni kumi mwaka huu umeeka shilingi milioni nne.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Waziri maendeleo ya wanawake na watoto unayapunguza kasi haya. Sasa hebu tueleze kidogo. Mimi ninafikiri kama kuna fungu jengine kama kwenye vilainisho na viburudishaji tukiviona ni vingi, tunaweza tukakupunguzia, tukakuletea huku ili uimarishe maendeleo ya wanawake na watoto.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Waziri vifungu vyako hatukunyang'anyi tutavihaulisha tu, tutachukua huku tunakipeleka huku, wewe hatukunyang'anyi kwa sababu unalelea watoto, lakini tutawanyang'anya tutanunulia DNA.

Mhe. Naibu Spika: Mheshimiwa malizia muda wako umekwisha.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Naibu Spika, ninamalizia ukurasa wa 10 kifungu 211110 tena posho maalum. Kwa hivyo hizi shilingi milioni kumi na mbili mwaka jana ilikuwa hamna, safari hii shilingi milioni kumi na mbili laki moja na sitini na nane tutahitaji maelezo.

Halafu kifungu 22022 kinajirejea tena huku ukurasa wa 10. Kuna mwaka jana ilikuwa viburudishaji hakuna, safari hii ni shilingi milioni kumi laki mbili na ishirini na tano. Mhe. Naibu Spika, hili vile vile nitahitaji maelezo.

Mhe. Naibu Spika: Mheshimiwa tunashukuru kwa mchango wako.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Naibu Spika, baada ya hayo machache, baada ya maelezo ya Mhe. Waziri nitamshukuru sana ninaamini atajibu vizuri nitaunga mkono hoja. Ninakushukuru Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Wanu Hafidh Ameir: Mhe. Naibu Spika, kwanza nikushukuru kwa kunipatia nafasi kwa kuchangia hotuba hii ya Waziri wa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto.

Pili Mhe. Naibu Spika, nimpongeze Mhe. Waziri kwa uwasilishaji wake wa hotuba hii, lakini pia niwapongeze watendaji wake kwa kumsaidia katika kutekeleza majukumu yake.

Mhe. Naibu Spika, kwa kuanzia mimi nitaanza na Idara ya Maendeleo ya Vijana ukurasa wa 24. Mhe. Naibu Spika, niipongeze wizara kwa juhudi inazozichukua juu ya kadhia ya ajira kwa vijana. Tumeona kuwa katika hotuba kwamba kuna hatua tofauti ambazo wamezichukua katika kuhakikisha kuwa vijana wanapata ajira.

Lakini Mhe. Naibu Spika, niseme tu kwamba bado kazi ni kubwa. Vijana wengi bado wanazururа bila ya ajira. Lakini sambamba na hilo Mhe. Naibu Spika, na Mhe. Waziri wa Utumishi wa Umma ananisikiliza kwamba ajira za mikataba kwa kweli zinatubana vijana kupata kazi. Hivyo Mhe. Waziri wa Vijana akishirikiana na Mhe. Waziri wa Utumishi walitazame hilo, wawatizame vijana kuna vijana wengi wanamaliza vyuo kila mwaka wanaingia katika soko la ajira, lakini ajira zenyewe hamna, wazee wanabana. Kwa kweli vijana tunakula kwetu, maneno yao.

Lakini Mhe. Naibu Spika, nikitoka hapo naomba nizungumzie kuhusu Baraza la Vijana. Mhe. Naibu Spika, Mhe. Waziri naomba niungane na Mhe. Jussa kusema kwamba Baraza la Vijana kwa kweli limechukua muda mkubwa mno kuzinduliwa.

Mhe. Waziri katika hotuba yake ya mwaka jana alikuwa anasema kwamba wizara inaandaa rasimu, lakini kila siku tunaambiwa hayo hayo kuwa inaandaa rasimu, mara inaratibu rasimu, inafuatilia rasimu almuradi uundwaji wa Baraza hili tokea serikali hii imeingia madarakani kuunda tu Baraza la Vijana imechukua miaka miwili na nusu hivi tunaelekea, bado Baraza la Vijana halijaundwa.

Mhe. Naibu Spika, naomba Mhe. Waziri alisimamie hili, mimi ninaamini anaweza kwa sababu akinamama tunaweza, alisimamie hili angalau katika bajeti 2013/14 aje atwambie hapa Baraza tayari limeshazinduliwa. Maana Mhe. Naibu Spika, kwa kweli tunaona vibaya watoto wana Baraza la Watoto, vijana wanashindwa kuwa na Baraza lao.

Hivyo hao watoto wakimaliza kwenye hilo Baraza lao wataenda wapi, hakuna Baraza la Vijana huku. Kwa hivyo ipo haja ya kuanzisha Baraza la Vijana kwa haraka sana ili hawa watoto wakitoka huko angalau wanaingia kwenye Baraza la Vijana.

Lakini pia Mhe. Naibu Spika, sambamba wenzetu wa Tanzania Bara ambao ndio wanaotuwakilisha katika mahusiano ya nje, hivi karibuni wameridhia mkataba wa vijana (*African Youth Charter*), ambao moja ya matakwa nchi ambazo zinaridhia mkataba huo wanatakiwa wawe na Mabaraza ya Vijana.

Hii nimesema hivyo Mhe. Naibu Spika, kwamba Mhe. Waziri aone umuhimu wa kuwa na Baraza la Vijana, ili vijana tusikose fursa zitakazopatikana katika hiyo *African Youth Charter.*

Mhe. Naibu Spika, nikitoka hapo naomba niingie katika Idara ya Maendeleo ya Wanawake na Watoto kwenye ukurasa wa 30. Mhe. Naibu Spika, kwanza nilikuwa ninamuomba Mhe. Waziri akija kufanya majumuisho hapa atufafanulie japo kwa ufupi matokeo ya utafiti ya udhalilishaji wa watoto. Kwa vile katika hotuba yake amesema kwamba wizara imezindua rasmi matokeo ya utafiti huo, lakini hajatuelezea yaliyojiri katika huo utafiti.

Mhe. Naibu Spika, ninasema hayo kwa sababu tunataka kujua udhalilishaji wa watoto hivi sasa umekithiri. Mara wamebakwa, mara wameng'olewa pua na vitovu, wanaibiwa, *child labour* bado ipo. Cha kusikitisha Mhe. Naibu Spika, ni kwamba haki haitendeki.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Mtumwa hapa amezungumzia kuhusu yule mama aliyeiba mtoto katika hospitali ya Mnazi Mmoja. Sitaki kuingilia kazi za Mahakama na Mhe. Mtumwa alisema yeye hana taarifa, mimi taarifa niliyonayo kwamba yule mama yupo nje anadunda kama ninavyodunda mimi hapa. Hapa sijui ushahidi gani unaotakiwa, maana angalau ingekuwa yule mama kakutwa na *baby show*, tungesema kakutwa na ngozi. Lakini kakutwa na ng'ombe mzima hasa kambeba. Ushahidi gani mwengine unaotakiwa.

Hili nilikuwa ninamuomba Mhe. Waziri kwa kweli alifuatilie sana kupitia kwa wadau anaoshirikiana nao, ninajua hawezi akaingilia ule muhimili mwengine lakini anashirikiana na Polisi na wadau wengine ambao wanafika huko. Kwa hivyo alisimamie, alishughulikie.

Lakini Mhe. Naibu Spika, nikitoka hapo ninataka kuzungumzia Benki ya Wanawake. Mhe. Hamza hapa ameizungumzia benki hii na vizuri. Lakini mimi niseme tu kama niungane na Mhe. Jussa alivyosema kwamba hili pia *process* yake ipo *slow* sana, halina tofauti la lile Baraza la Vijana kila siku wanaratibu, wanashajihisha, hamna jipya. Kwa hivyo mimi ninaamini kwamba Mhe. Waziri anaweza kwa sababu ni mwanamke. Kwa hivyo alifuatilie hili ili awakwamue wanawake wenzake ambao wana hali duni ya kimaisha.

Mhe. Naibu Spika, nikimaliza hapo naomba niingie kidogo katika Ustawi wa Jamii. Ustawi wa Jamii mimi nitagusia Pemba. Mhe. Naibu Spika, kwa kweli ipo sijui nisemeje haifanyi chochote. Kuna NGO moja pale Chake-Chake ndio inayoshughulikia kila siku kuhusu watoto walioathirika na HIV na pia wanaoishi katika mazingira magumu. Wamediriki kusema kwamba wao ndio ustawi wa jamii wa Pemba kwa sababu kila kitu wanafanya wao.

Mhe. Naibu Spika, Ustawi wa Jamii Pemba kwa kweli ipo haja ya kujitutumua angalau na nyinyi mukafanya kitu mukaonekana. Mzigo mkubwa munaitisha hii NGO, kwa hivyo nilikuwa ninamuomba Mhe. Waziri akija hapa atueleze kuna nini Idara ya Ustawi wa Jamii Pemba, kila kitu munaitupia ile NGO ifanye kazi, na ubaya zaidi kwamba kuwezeshwa pia haiwezeshwi, angalau mukawa-*support* wakaweza kuwashughulikia hao watoto wanaoishi katika mazingira magumu.

Mhe. Naibu Spika, nikitoka hapo naomba niingie kwenye buku kidogo mambo ya viburudishaji na mambo mengine ambayo Mhe. Jussa na Mhe. Hamza wamezungumzia, sitogusia lakini pia niseme ujumla safari za ndani pia zimenona. Nilikuwa ninamuomba Mhe. Waziri akija labda atuelezee wanataka kufanya nini na nini ili tujue hizi pesa. Kwa sababu safari za ndani hazina tofauti na safari za nje, *almost* zinakutana.

Kwa hivyo zimenona sana, hivyo kuna lipi ambalo lilikuwa linataka lifanyike humu labda atuelezee. Lakini jengine ni kifungu 272100 – Misaada ya Kijamii katika Afisi Kuu Pemba. Ndio yale niliyokuwa ninasema kwamba Ustawi wa Jamii haufanyi kitu Pemba. Kuthibitisha hilo hakijaombwa chochote katika mwaka huu wa fedha. Jee, Ustawi wa Jamii upo sawa Pemba kwamba hawahitaji fedha zozote za kutoa misaada ya kijamii.

Baada ya hayo Mhe. Naibu Spika, kwa niaba ya vijana wa Mkoa wangu wa Kusini Unguja na wote vijana ninaunga mkono hoja. Ahsante sana Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Mgeni Hassan Juma: Ninakushukuru sana Mhe. Naibu Spika, na mimi kunipa fursa hii adhimu ya kuchangia hotuba ya Waziri wa Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Wanawake na Watoto.

Awali ya yote na mimi nimshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehma aliyetujaalia hapa leo tukiwa wazima wa afya, na kuweza kusimama kutetea na kusimamia haki za wananchi wote wa Zanzibar kwa ujumla.

Mhe. Naibu Spika, ninachukua fursa hii adhimu kumpongeza Mhe. Waziri wa wizara hii pamoja na watendaji wake wote, kwa kazi kubwa ambayo wanaifanya katika kuhakikisha kwamba majukumu waliyopewa wanayatekeleza vizuri, lakini wanatengeneza mustakabali wa taifa hili.

Mhe. Naibu Spika, pia nachukua nafasi hii kumshukuru sana na kumpongeza Rais wetu wa Zanzibar Mhe. Ali Mohammed Shein kwa uamuzi wake aliouchukua wa kufuta ada ya uzazi kwa kinamama na kutoa maamuzi ya kuwaombea wazee wetu angalau wapate milo mitatu kwa siku. Kwa kweli nampongeza sana Mhe. Rais na kama alivyogusia Mhe. Hamza Hassan Juma amesema kwamba anatekeleza yale ambayo Marehemu Mzee Abeid Amani Karume Muasisi wa Mapinduzi ya Zanzibar aliyaanza. Kwa hivyo tunamshukuru sana.

Vile vile naipongeza sana wizara kwa kushirikiana na asasi za kiraia kwa kutekeleza malengo mbali mbali yaliyowekwa katika *millennium*, katika MKUZA pampoja na Ilani ya Chama cha Mapinduzi. Kwa kweli wizara hii ni moja katika wizara ambayo naweza kusema kwamba wanakwenda bega kwa began a asasi za kiraia ili kuhakikisha kwamba maendeleo ya nchi hii yanapatikana nawashukuru sana.

Mhe. Naibu Spika, mimi nitaanza na ukurasa wa 24 Idara ya Maendeleo ya Vijana. Mhe. Naibu Spika, wizara hii imebeba makundi mawili makubwa na laiti ingelikuwa si makundi haya mawili makubwa ya wanawake na vijana leo pengine tusingekuwa tumesimama hapa tunaizungumzia Serikali ya Umoja wa Kitaifa. Hawa ndio waliopiga kura kwa wingi kuhakikisha kwamba serikali hii imesimama. Kwa hivyo, Mhe. Naibu Spika, makundi haya mawili ni ya kuyapongeza na ndio yaliyotufanya leo Zanzibar tumekuwa na amani na utulivu katika nchi yetu.

Mhe. Naibu Spika, mimi nampongeza sana waziri, namfahamu ujasiri wake alionao, namfahamu waziri uwezo wake alionao lakini pia namfahamu mapenzi yake aliyonayo kwa vijana. Waziri akipata nafasi ya kutumia ya kusaidia vijana kwa kweli anafanya vile ambavyo anatakiwa kufanya. Kwa kweli tumpe sifa Mhe. Waziri anaweza kufanya na anafanya kazi kwa moyo wake wote.

Sasa tuna changamoto kubwa ya vijana wetu, tuna changamoto kwa sababu vijana wetu tunasema kwamba wanaporomoka. Amesema Mhe. Ismail Jussa hapa maadili yanaporomoka, lakini wakulaumiwa sio wao vijana kuna Muaustralia mmoja alifanya *research* katika nchi ambazo zinaendelea kuhusiana na vijana na aliangalia sana kwa nini vijana wetu wengi sasa hivi wanajiingiza katika masuala ya dawa za kulevya. Alisema nchi zinazoendelea zimeshindwa kumu *occupy* kijana, zimeshindwa kumtizama kijana kumjua maumbile ya kijana na kuweza kumtengenezea mazingira ya kumdhibiti kijana yule asiende katika matendo maovu na hilo ni kweli.

Naweza kusema hivyo kwa sababu leo katika maeneo mbali mbali ambayo tunajenga majumba tunasahau kuweka hata viwanja vya mpira vijana wetu wakenda kule wakacheza mpira au wakafanya *activity* yoyote ya kuwafanya vijana wale badala ya kukaa kwenye mabaraza na kuanza kufanya mambo ambayo hayakubaliki lakini wanafanya hivyo. Kwa sababu maeneo yote tumejenga majumba na tumeweka tunavyotaka sisi lakini tumesahau kuwawekea vijana sehemu za kukutana na kufanya shughuli mbali mbali za kuweza kutoa lile jasho lao la ujana. Ujana ni ujana lazima kijana awe *active* tukitaka tusitake, kuna mambo kimaumbile kijana lazima ayafanye na kama hakufanya basi atachukua ule ujana wake ataupeleka kwengine. Sasa Mhe. Waziri kazi unayo kubwa kwa sababu tumeteleza lakini haina maana kwamba hawa tulioanao hatuwezi kuwasaidia kuwaelekeza katika njia nzuri.

Wenzangu waliotangulia wamesema Baraza la Vijana limechukua muda mpaka hivi leo Baraza hilo halijasimama wima, tunakaa vikao vingi lakini bado halijajengewa nguzo za kutosha na baraza hili kuanza kufanya shughuli zake. Mimi namuomba Mhe. Waziri ahakikishe mwaka huu kabla ya kumalizika Baraza hili lisimame wima na lianze kufanya shughuli zake na lisimamie shughuli zote za vijana. Mhe. Waziri nakuomba sana kwa hilo.

Lakini nikiendelea Mhe. Waziri sisi tunakutana na matatizo mengi sana mitaani na nafikiri na wewe unajua na kila mtu hapa anajua. Vijana wetu wanataka kufanya mambo mengi sana, na huwa saa nyengine yananishangaza mambo ambayo vijana wanakuja kunambia kuomba wasaidiwe lakini wanawekewa vikwazo. Vijana sasa hivi katika kila jimbo wamejikusanya wanasema sisi basi tutasafisha mazingira yetu, sisi tutafanya hivi lakini tupeni muongozo tusaidieni. Kuna baadhi ya taasisi kuna baadhi ya idara wanakwenda wanavunjwa moyo inasikitisha. Sasa kijana ameshasema mwenyewe atafanya leo unamdharau ukimdharau maana yake unampeleka kwengine kubaya. Kuna vijana wetu wengi mfano wametoa kuna vijana *ZASOSE,* kuna vijana *ILO* ambao wako tayari kabisa tena wanajua kila kitu kuhusu Mjini Magharibi na wako tayari kushirikiana na Manispaa kusafisha mji, kukusanya mapato lakini Mhe. Waziri mpaja hii leo vijana hao wamekaa hakuna mtu wa kuwasimamia wala kuwasaidia.

Sasa hayo ndio ninasema kwamba hawa mwisho wake wanaishia pahala pabaya. Vijana Mhe. Waziri wanasema tunataka kujiunga, tunataka kutengeneza ushirika lakini wanashindwa hawajui wapi wende, wakienda ushirika wanaambiwa lazima mtoe kiasi fulani wakitaka kuanzisha vikundi mbali mbali wanaambiwa lazima wawe na katiba lazima wawe na nini ilimradi kuna mambo mengi sana yanawakwaza. Hakuna sehemu vijana hawa wanayoweza kwenda wakapewa *directions* fanyeni hivi, fanyeni hivi mtafanikiwa, kwa kweli tunawatupa vijana sana tena. Mimi nakuomba Mhe.Waziri hebu watizame hawa vijana, hebu tutafute mbinu ya kutafuta kituo maalum.

Juzi nilimuomba Waziri wa Nchi (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora nikazungumzia hayo hayo hatuna *centre* ambayo itamfanya kijana yeyote Mzanzibari mwenye uwezo na aliyekuwa hana uwezo ile *centre* ambayo itawakusanya vijana wetu wote pale watapata *information* mbali mbali kuhusu ajira ikiwa kuhusu namna ya kuunda kikundi ikiwa kuhusu jambo lolote ambalo linawahusu wao hatuna ni shaghala baghala, kila mmoja anakwendea kwake na sivyo. Wenzetu nchi zilizoendelea wamejipanga hivyo, kijana anapomaliza skuli anajua anakwenda wapi nikienda pahala fulani nitafanikiwa hapa nitapata nitakwenda kila siku lakini anakwenda pale anaangalia anaambiwa

hapa pana hiki na hiki ukitaka kufanya hiki utasaidiwa, lakini hawa vijana tunawaacha tu. Kwa hivyo, Mhe. Naibu Spika, mimi naona Mhe. Waziri ana kazi kubwa.

Jengine hawa hawa vijana ambao tunasema kuwa wakimaliza elimu zao za juu mimi nashanaa sana kwa sababu nafasi nyingi ziko hata nyengine za nje za kufanya kazi, lakini vijana wetu wengi wanashindwa hata kwenda kufanya *interview* kwa sababu hawana ujuzi wa kufanyia *interview*. Kwa hiyo mambo kama haya ni sisi kuwatayarishia hawa vijana, sisi kuwapa mafunzo vijana hawa ili waweze na wao kupata ajira na kufanya shughuli mbali mbali za kimaendeleo.

Mhe. Naibu Spika, niingie katika ukurasa wa 30 Idara ya Maendeleo ya Wanawake na Watoto. Mhe. Naibu Spika, idara hii ina shughuli nyingi sana na kwa kweli idara hii haijapewa uwezo wa kutosha. Kwanza mimi nataka kusema tu kwamba kila siku kesi zinaongezeka zinazohusiana na udhalilishwaji wa wanawake na watoto. Kwa kuwa zinaongezeka basi iko haja ya kuongeza nguvu kwa idara hii sasa ina uzaidi wa wafanyakazi hamna, nyezo hamna, sasa ikiwa kama idara hii haina rasilimali watu kazi zitafanyika vipi, idara hii ina kazi kubwa.

Nasikitika kusema kwamba sasa hivi Zanzibar tumetiwa katika kundi la nchi ambayo udhalilishaji wa wanawake na watoto upo kwa kiasi kikubwa inasikitisha sana. Hakuna sababu sisi Zanzibar ni kidogo hakuna sababu ya kuwa na matokeo kama hayo, lakini kwa sababu watendaji wa shughuli hizi hamna ni kidogo sana na kwa sababu haya mambo yanaendelea kila siku inabidi sasa tufanye juhudi za makusudia za kuhakikisha kwamba idara hii tunaizidishia uwezo. Idara hii inahitaji kuwepo katika kila kitongoji sio wilaya ni kila kitongoji iwe na uwezo wa kufika kule na kuweza kuwapa elimu wananchi walioko kule, lakini idara hii kama tutaibania ina maana watashindwa kufanya kazi zao. Kwa hivyo, mimi namuomba Mhe. Waziri mwaka huu sijui kama tutaweza kwa hiyo kasma ambayo wamepewa ni kasma bado mimi naona ndogo lakini najua na kazi itafanywa kwa ugumu labda mwakani tutaangalia tena na kuhakikisha kwamba idara hii inapewa kasma kubwa zaidi ya hii ya mwaka huu.

Mhe. Waziri tatizo la udhalilishaji watoto limekuwa kubwa sana na mimi nakumbuka vizuri mwaka jana nilisema hivi, hebu tuangalie sasa hivi ni makundi gani ya watu ambao wanafanya vitendo vya kudhalilisha watoto. Taarifa tunazipata nyengine zinasema kuwa hata walimu baadhi sio wote, baadhi ya walimu waovu wa vyuo vyetu, wa madrasa zetu ndio waharibifu wakubwa wa watoto na tena sio watoto wa kike tu, bali sasa kuna mtidno wa kuharibu watoto wa kiume. Nitaomba wizara jambo moja, sasa hivi umeshafika wakati hawa walimu wote wa vyuo, wa madrasa wawe wamesajiliwa lakini la pili wafanyiwe *police check.*

Kwa sababu mtu anaweza akatoka pengine Makunduchi akawa na chuo kaharibu mtoto mmoja au wawili akapenya, akenda zake sehemu nyengine Kaskazini nako akapenya, lakini anajulikana na taarifa zake zinajulikana, huyo huyo akaja Mjini Magharibi akafanya yale yale. Sasa hayo ni mambo ambayo tunafanya kwa kweli ikiwa tutayafumbia macho ina maana kwamba tunafanya makusudi.

Mimi ningewaomba wananchi jamani tushirikiane wanaoharibika ni watoto wetu, nawaomba wazee na wananchi kwa ujumla masuala haya tusiyafiche yanapotokea tuyapeleke kwa wanaohusika. Kwa sababu moja ni kwamba kweli kuwa wizara inakuwa haina taarifa ya masuala haya ya kuzalilisha watoto. Kuna watu hawapeleki taarifa za kutosha lakini pia pale ambapo mtu anatakiwa kutoa ushahidi wengi wanakimbia. Sisi kamati tumepata bahati kwenda katika kitengo cha *Save the Children* kilichokuwepo Hospitali ya Mnazi Mmoja, wametwambia kwa mwezi mmoja wanapata watoto wa kike *under age* 20 kwa mwezi yaani hiyo ni *maximum* 20 ambao wamepata ujauzito wakiwa wengine wamekamatwa kwa nguvu.

Wametwambia kuwa kesi nyingi nyengine zinaishia hewani lakini kesi ambazo zimeripotiwa za kuzalilishwa nyingi hazipati hukumu. Tatizo moja wamesema ni hilo la *DNA*, lakini mimi nashukuru tumepata taarifa nakumbuka vizuri sana Mhe. Waziri alitwambia kwamba serikali iko njiani kuhakikisha kwamba hiyo mashine itapatikana na hivi karibuni itapatikana. Nafikiri itakuwa ni faraja sana kwetu kupatikana kwa mashine hiyo kwa sababu itawapeleka wengi ambao wanazalilisha watoto sehemu ambazo wanatakiwa kuwepo.

Mhe. Naibu Spika, suala la uzalilishaji wa watoto linapofika katika sehemu ambazo sheria zinawaruhusu kufanya uchunguzi tatizo kubwa linajitokeza kwamba uchunguzi ule haufanyiki ilivyo. Kwanza wenyewe polisi mara nyingi wanakuwa bado hawajawa na uwezo na utaalamu mzuri wa kuweza kuzishughulikia kesi hizo. Hilo moja.

Lakini la pili, uwekaji wa vidhibiti yaani *evidence.* Tumekuta kesi moja ya mlemavu ambaye kabakwa na katiwa mamba, tumekuta kesi ambayo wale madaktari wa *Save the Children* walikuwa wanasema tuna hakika baada ya kumtoa damu yule kwa ajili ya *DNA* ile damu imechukuliwa na wanaokamata ule ushahidi ni polisi. Lakini wanasema tuna hakika hawana uwezo huo, sio uwezo wa kisheria lakini uwezo wa kuweka, imechukua wiki kama tatu ndio ile damu imepelekwa Dar es Salaam kwa ajili ya kufanyiwa uchunguzi wa *DNA.* Sasa sijui katika mazingira gani ambayo ile damu imewekwa au ile *sample* kwa sababu sio lazima damu *DNA* unaweza kutoa hata kwenye mate, ile *sample* imewekwa katika mazingira gani. Sasa katika matokeo yake inaweza pia kusababisha kwamba ile *sample* ikaja sivyo ambavyo mmetegemea.

Tulipokwenda polisi wakasema wao ndio wamepewa mamlaka na sheria ndio inaowaruhusu kukamara vile vidhibiti. Kwa hivyo mimi nafikiri sheria hizi nyengine tuziangalia upya sasa hivi, tuzitizame na tuone kama kweli, Mhe. Naibu Spika, bahati mbaya Mwanasheria Mkuu hayupo hapa lakini tuzitizame upya. Kwa sababu polisi wanafanya wao kwa kuwa sheria zinawaruhusu lakini inawezekana njia hii au sheria hiyo inayotumika kwa kweli inasababisha kesi nyingi sana kuwa zinashindwa kupatikana hukumu zake na haki inashindwa kutendeka.

Mhe. Naibu Spika, sasa nitazungumzia Benki ya wanawake. Kama walivyosema wenzangu waliotangulia kwamba mwaka jana tulikuja, mwaka juzi nakumbuka sasa hivi ilikuwa Benki ya Wanawake mpaka kwenye Ilani ya Uchaguzi Rais wetu alizungumzia suala hilo hilo la Benki ya Wanawake. Sasa imekuwa changamoto ni kubwa hatujui ni kitu gani ambacho kinafanya hii benki ya wanawake kuwa bado inashindwa kuanzishwa. Kwa kweli inasikitisha, Waheshimiwa wengi walizungumza kuhusu benki hii inasikitisha lakini inanitia wivu kuwa wenzetu Tanzania Bara kama alivyosema Mhe. Hamza Hassan hawajawekewa vikwazo, benki hii ipo na hakuna vikwazo vingi sasa kwa nini sisi kuwe na vikwazo si benki hii tu lakini benki nyengine pia zina vikwazo wanawake wanashindwa kwenda kuchukua mikopo unaambiwa uwe na hiki, uwe na hiki lakini kule tofauti kwa nini iwe hivyo na sisi ndio nchi mmoja, Tanzania moja. Kwa nini iwe wao wanapewa nafasi nzuri ya kupata mikopo wanawake lakini huku tofauti.

Lakini na hii benki mimi naamini tukianzisha benki yetu ya wanawake naamini kwamba itasaidia sana katika kuleta maendeleo ya wanawake wa Zanzibar na ya kiuchumi kwa sababu tatizo kubwa linalojitokeza sasa hivi kwa wanawake ni tatizo la kiuchumi na moja katika sababu ambayo wanasema watu wa Haki za Binadamu kwamba moja katika sababu ya kuwafanya wanawake wazalilishwe ni hali ya wanawake ya kiuchumi bado ni ndogo sana. Kwa hivyo, mimi Mhe. Waziri namuomba tena wizara yake ilisimamie hili kidete ihakikishe kwamba hii benki isiwe ni benki ya maneno bali iwe ni benki itakayokuwa inatoa fedha kuwakopesha wanawake na kuwasaidia katika masuala yao ya kiuchumi.

Maneno Mhe. Waziri basi, hapa sasa hivi wakati wa maneno umekwisha sasa hivi ni wakati wa sayansi na teknolojia na utekelezaji. Mhe. Waziri nakuomba sana hili ulisimamie na najua unaweza na Mwenyezi Mungu atakujalia utaweza *Inshaallah*.

Lakini la mwisho kabisa nilikuwa nataka nichukue fursa hii adhimu kumpongeza tena Mhe. Waziri wetu wa vijana kwa moyo wake wa huruma kwa kuwasaidia vijana. Tumeona kweli anawasaidia vijana mbali mbali ametoa taarifa humu ndefu kabisa ya kuwasaidia vijana wakiwemo vikundi kutoka Pemba na Unguja na vikundi vyote hivi vinajishughulisha zaidi katika masuala ya kujiajiri wenyewe. Ajira sasa hivi ya kujiajiri wenyewe ndio ajira tunayoizungumzia. Kwa hivyo, Mhe. Waziri anasaidia sana maendeleo ya taifa hili kwa sababu anawapa mwelekeo mzuri vijana wetu na wao vile vile wamenituma nimwambie waziri vijana mimi si vijana lakini nina vijana wengi nawalea wamesema nikwambie uendelee kukaza kamba na wao wako nyuma yako wanakushukuru sana kwa bidii na jitihada yako ambayo unaionesha na mapenzi yako kwao.

Baada ya kusema hayo machache nakushukuru Mhe. Naibu Spika na ninachukua fursa hii kukubali bajeti hii kwa asilimia mia moja ahsante.

Mhe. Fatma Mbarouk Said: Ahsante Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa fursa hii ya kuchangia hotuba hii ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Mwaka wa Fedha 2012/2013. Mhe. Naibu Spika, kwanza na mimi kama wenzangu walivyoanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuweza kufika hapa saa hizi na nikawa na pumzi.

Mhe. Naibu Spika, na mimi pia nichukue fursa tena ya kumpongeza Rais kwa kumchagua mama Zainab Omar kwa kuwa Waziri wa wizara hii. Kwa kweli wizara hii ni lazima awepo mwanamama ambaye anajua matatizo ya

wanawake, watoto na pia na wazee. Kwa sababu mwanamke ni kila kitu, mwamke ni mama, mwanamke ni mtunzaji wa familia na pia ni mtu ambaye Mwenyezi Mungu kamjaalia na huruma na ni mtu ambaye ni dhaifu au dhalili na wakati wowote huwa anahitaji kusaidiwa.

Kwa kwalei Mhe. Rais ameona hapa matatizo mengi ambayo yanawakumba na hasa wazee na niipongeze wizara hii kwa imani kubwa ambayo ameiona Rais kwa kuwashughulikia wazee na kupitia wizara hii Mhe. Waziri ameweza kuwahifadhi wazee na hasa pale katika maeneo ya Sebleni.

Mhe. Naibu Spika, kwa kweli nikienda na Idara ya Mipango na Sera. Hii nitasema katika wizara ni lazima iwepo Idara ya Mipango na Sera, na kwamba hata waziri mwenyewe anakuwa yupo chini ya Idara hii. Kwa kweli ina majukumu makubwa. Moja ni katika hayo hayo ya kuandaa bajeti hizi zinazoletwa na watendaji ambao wao ndio wanaokuwa wasimamizi.

Vile vile Idara nyengine ambayo nimeiona ni muhimu katika kila wizara ni Idara ya Utumishi, ambayo maslahi wafanyakazi wote yanakuwepo hapa. Kwa kuwa maslahi ya wafanyakazi jana nilisema, lakini mimi sina kawaida ya kupiga buti lakini ni kusema tu, wala kama sikujibiwa sifanyi pingamizi labda nipige mabuti au vipi, kwa sababu nimeshaeleza na jambo limeshajulikana, nitajua kwamba nimeshachangia katika Baraza hili.

Mhe. Naibu Spika, nikienda kwenye ukurasa wa 13 ambao unasema programu ya kukuza ukusanyaji na uchambuzi wa takwimu. Niipongeze sana wizara kwa kuanzisha programu hii ambayo lengo lake kuu ni kusaidia Serikali ya Zanzibar katika jitihada za kukuza usawa wa kijinsia.

Kwa hivyo nimshukuru sana Mhe. Waziri kwa programu hii ambayo imejionesha hapa na kazi nyengine ni muhimu ya kukusanya, kuzichambua na kuzisambaza takwimu za kijinsia.

Mhe. Naibu Spika, katika majukumu ya Idara hizi mbali mbali ikiwemo hii ya utumishi ambayo nimeona majukumu yake ni kama nilivyokwisha kuyaeleza. Moja ni utunzaji wa mali za wizara. Kwa hivyo nikiseme tu kwamba tumepita kama sisi kamati ya PAC tumeona matatizo mbali mbali ambayo mali za serikali zinakuwa kwa kweli hazipo katika *register*. Kwa hivyo Idara hii ningesema kwamba sasa ichukue juhudi za makusudi ili sasa tuone kwamba hizi rasilimali za serikali zinatunzwa kwa kutiwa kwenye vile vitabu maalum.

Pia kutayarisha mpango wa mafunzo wa wizara na kuutekeleza. Kwa kweli mafunzo ni muhimu. Bila ya kumpa mtu mafunzo naona kama ile *efficiency* ya wizara ambayo imejipangia kwa kweli haitoleta faida. Hakutakuwa na faida kama hatukuwasomesha na kuwawezesha, kwa sababu kufanya kazi bila ya elimu ni sawa sawa na kumpa mtu mzigo ambao hukumsaidia namna gani ya kuubeba. Kwa hivyo hili ni jmbo muhimu la kuwasomesha.

Vile vile niipongeze wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo kushughulikia na kuwapatia posho la mazingira magumu wafanyakazi 118. Kwa kweli hili ni jambo la kupongezwa na kwa sababu wanashughulikia wazee hawa, kwa sababu mzee siku zote nitasema anataka kuengwaengwa na kushughulikiwa. Wazee wanapokuwa ni wazee kwa kweli wanasema akili zinakuwa zinarudi uchanga.

Kwa hivyo suala la kuwashughulikia wazee ni jambo la muhimu na ni lazima sote tuwe wakarimu na wapole kwa wazee wetu hawa. Kwa sababu hawa ndio waliotuletea utulivu wa nchi yetu, wakatulea mpaka kufika hapa leo tukafika kwenye Mabaraza haya ya Kutunga Sheria, ni ule ustahamilivu wa wazee na kutulea kwa uzuri sana. Hakuna mzee hata mmoja anayethubutu kumnyanyasa mtoto wake. Kwa hivyo na sisi ni lazima hapa tulipofika tuwaone kuwa wazee ni muhimu kwetu.

Mhe. Naibu Spika, ninakuja kwenye Idara ya Ustawi wa Jamii ukurasa wa 19. Tumeona vile vile Idara hii ilivyojipangia malengo yake. Moja ni hiyo hiyo ni kuimarisha huduma za wazee. Kwa kweli wazee kama nilivyokwisha kusema kwamba wazee ni muhimu na tusiwanyanyapae.

Mhe. Naibu Spika, nikienda kwenye ukurasa wa 21, niende na nimeona kuna ukumbi huu wa Sebleni. Kwa kweli nimeona hapa kuwa umeshafanyiwa ukarabati. Nimshukuru sana Mkurugenzi ambaye anashughulikia suala hili kwamba ukumbi huu unatusaidia, na kama tutauhuisha basi tutapata *revenue* katika serikali ambayo ni mambo ambayo tunayatafuta ili kuendesha mambo yetu mbali mbali. Kwa sababu *revenue* inaingia katika mfuko mkuu wa serikali, kwa hivyo tutajipangia kwenye kazi zetu za kawaida na kazi za maendeleo kwa serikali yetu hii.

Kwa hivyo niseme kwamba kwa kweli kitabu hiki kimekusanya mambo mengi. Mhe. Naibu Spika, niseme kuna udhalilishaji huu wa watoto. Kwa kweli haya ni mambo ambayo kila pahala na kila siku tunasema. Kila mmoja hivi sasa ni lazima tubadilike. Mtu anayefanya matatizo kama haya kama alivyosema Mhe. Hamza kuwa hawa watu wahasiwe, kweli haya matatizo yapo.

Mimi ninakumbuka siku moja Mhe. Naibu Spika, yule kitangi *original* wakati nina umri mdogo sana, ninafikiri sherehe zilikuwa za miaka 10 kulikuwa na sarakasi ya Kichina pale Uwanjani Mao-Tse-Tung, kwa hivyo nimesimama hivi, sasa ninahisi huku nyuma ugumu ugumu, nikageuka yule bwana nikamtizama kumbe ndiye yule, sasa alipokuja kutolewa hadharani nikasema ndiye mtu yule nikamjua yule bwana. Kwa kweli yule mtu alikuwa ni hatari sana Mwenyezi Mungu amrahamu hivi sasa. Kwa kweli matatizo haya yapo ya kuwabaka watoto na sijui kwa kitu gani, ndugu, kaka na baba zetu kufanya masuala haya kwa sababu suala kama hili baya ukawa unamfanyia mtoto wa mwenzio, kwa kweli inakuwa haileti sura nzuri. Kama mzazi hawezi kufanya masuala kama haya hapa.

Kwa hivyo ni lazima sheria zifuate mkondo wake na zile kesi ambazo tunasema kwamba zinachukua muda mrefu hazipatikani kwisha kwake, na watu wale zaidi tunaona hivi vitendo vinaongezeka.

Hivyo ni lazima zile kesi zifuatiliwe. Mimi ninayo kesi moja pale Amani, kila siku nikimuuliza yule mama mara anaambiwa sijui *file* yule Jaji anayeshughulikia yupo wapi, ni mwaka wa pili unafika mpaka leo ile kesi kila nikimuuliza anasema bado haijapata ufumbuzi. Na mwenyewe yule mtoto si mdogo kamuelezea kuwa huyu ndiye aliyenifanya hiki kitendo.

Mhe. Naibu Spika, kwenye Idara ya Maendeleo ya Vijana. Kama walivyokwishasema wenzangu kwamba ni lazima tuwatafutie kazi vijana hawa, tuwaelimishe na kuwapeleka sehemu mbali mbali kwenda kuwapa mafunzo ya amali. Lakini ikisha hapo imekuwa ni basi hatuwaendelezi tena, tunawaacha watoto wale wakibabaika huku na kule na mpaka inapelekea kujitia katika vitendo mbali mbali vya dawa za kulevya. Kwa kweli wakijitia kwenye vitendo hivi vya dawa za kulevya inakuwa ni matatizo na inakuwa ni balaa kwa serikali kwa kweli. Inakuwa ni mzigo mkubwa. Kwa hivyo ni lazima tunapowapa haya mafunzo ya amali basi baadae tuone ni namna gani ku-*empower* ili kutafuta mambo mbali mbali angalau tukaanzia.

Mhe. Naibu Spika, nikienda kwenye ukurasa wa 30 Idara ya Maendeleo ya Wanawake na Watoto. Idara hii ina jukumu la kuratibu na kusimamia utekelezaji wake wa haki za wanawake na watoto.

Kwa kweli kama tunavyojua mwanamke ana mambo mengi na ukimsomesha mwanamke mmoja ni kama umesomesha jamii. Kwa hivyo ni lazima wanawake wapewe uwezo wa kufanya au kuanzishiwa mambo mbali mbali, kwa sababu hii ndio tukasema *catalyst* kwa jamii. Bila ya kuwepo mama basi familia kwa kweli inakuwa haina maendeleo mazuri, lakini baba akiwa hayupo anaweza kukaa hata wiki mbili tatu bila ya kuwepo baba, basi nyumba ikawa inaendelea vizuri. Lakini kutokuwepo mama muda mchache tu basi nyumba itasambaratika.

Kwa hivyo ni lazima wanawake tufuate Mtume (SAW) na kama sisi ni waumini humu kama tunakumbushwa kwamba tunavyosomeshwa alikuwa ni mtu hodari katika nyumba zake. Kwa hivyo akina baba vile vile niombe kwamba wawe mahodari na wawe chini ya akinamama, wawasikilize, wawezeshe ili ile familia isipate kusambaratika. Tuwe karibu na familia zetu akina baba.

Unajua wanawake ni mambo madogo tu ambayo yanawakwaza, lakini kama utakuwa karibu na mama basi kila siku familia itaendelea kuwa vizuri na itajengeka katika ule utamaduni wetu wa kuwa baba ukiwepo karibu na mama basi adabu na heshima itapatikana. Huwa tunasema kuwa unapotaka kutengeneza familia nzuri watoto uwafanye kama marafiki ndani ya nyumba, usiwe mkali tu. Kwa sababu ukiwa mkali kisaikilojia mtoto anajenga hofu kwako. Kwa hivyo ni lazima tuwe kama marafiki na watoto ndani ya majumba yetu. Wakifikwa na kadhia yoyote wasione taabu kukuelezea.

Kwa hivyo hili ni jambo ambalo ni zuri katika kujifunza. Familia ya baba na mama kukaa pahala pamoja. Mtoto mkiwa mbali mbali kwa kweli, mmoja wapo ikiwa mumeachana kidogo basi ndani ya nyumba ile kutakuwa hamna maendeleo mazuri.

Kwa hivyo Mhe. Naibu Spika, niseme kwamba kwa maelezo hayo mafupi ambayo nimeyaelezea kupitia kwenye kitabu hiki niseme naunga mkono hoja, kwa niaba ya wananchi wangu wa Jimbo la Amaani asilimia mia kwa mia.

Mhe. Bikame Yussuf Hamad: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwanza sina budi nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia afya njema tukaweza tukakutana jioni hii katika ukumbi huu mtukufu tukiwa tumo ndani ya kujadili maslahi ya nchi yetu.

Lakini pia nikushukuru wewe Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa fursa hii kuweza kuchangia machache katika bajeti hii ya Wizara ya Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto.

Mhe. Naibu Spika, kwanza nataka nichukue fursa hii kumpongeza Mhe. Waziri na watendaji wake wote kwa jumla kwa kazi yao nzuri waliyoifanya katika kitabu hiki, na waliyotueleza ndani yake yana ukweli kiasi fulani. Kwa hivyo ninamshukuru yeye pamoja na watendaji wake wote kwa jumla.

Mhe. Naibu Spika, naanza katika mchangio wangu ninataka niingie kwenye ukurasa wa 4 hapa kifungu cha 11, kasema Mhe. Waziri kuwa “hotuba hii ya makadirio ya mapato na matumizi imezingatia mipango mikuu ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ambayo ni dira ya maendeleo 2020, mkakati wa kukuza uchumi na kupunguza umaskini.

Ni kweli Mhe. Naibu Spika, kwenye kitabu hiki basi Mhe. Waziri na watendaji wake kwa kiasi fulani wamelenga matendo yao katika maeneo hayo au katika mpango mzima huu. Kwa sababu ukiangalia ndani ya viambatanisho hivi utakuta maendeleo mengi ambayo yamesaidia katika jamii nyingi sana ambazo kuwa ni watoto wanaoishi katika hali ngumu, lakini watu wasiojiweza, mambo tele kayaeleza humu. Kwa hivyo hii ninaona kidogo imezingatia.

Lakini katika malengo yao makuu takriban niseme wizara nyingi huwa malengo yao makuu bado, malengo yanayokuja kipindi cha bajeti cha mwaka jana na huu, huwa ni yale yale yanajirudiarudia. Badala ya kuwa kwenye kitabu kilichopita malengo yao makuu waliyoyafanya watueleze wamefikia hatua gani, lakini hili huwa bado katika vitabu vyengine vya bajeti huwa hatulioni.

Mhe. Naibu Spika, niendelee huu katika ukurasa wa 7. Ukurasa huu kasema Mhe. Waziri kuwa masuala ya malezi na makuzi ya mtoto mwenye umri kati ya miaka zero-nane. Sasa mimi hapa sijafahamu kidogo ninataka akija anieleze. Huu kuanzia mwaka zero - nane ni kuwa malengo yao ataanza kuhudumikiwa mtoto aliomo ndani ya tumbo, kwa kuweza kupatiwa pengine mama yule mja mzito lishe bora na kuweza kukikuza kile kizazi kilichomo tumboni na kufikia umri huo au ni kuanzia pale atakapozaliwa.

Kwa sababu unapomkuza mtoto anapokuwa ndani ya tumbo la mama yake basi pale kinapozaliwa kizazi kizuri na hatimaye ukapungua ulezi wa matatizo mengi. Kwa hivyo akija hapa Mhe. Waziri anieleze alivyokusudia.

Lakini Mhe. Naibu Spika, kwenye ukurasa wa 11 Mhe. Waziri amezungumzia hapa kwamba katika kifungu cha 24, “Maandiko haya yanahusu programu ya kukuza ukusanyaji na uchambuzi wa takwimu, jinsia, kuanzisha benki ya wanawake na kuwajengea uwezo na mbele ameendelea.”

Lakini mimi Mhe. Naibu Spika, katika hili kuanzisha benki hizi za wanawake. Imekuwa hadithi ndefu ambayo ukija kwa Waziri wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi ana malengo haya ya kuanzisha benki hizi, lakini pia ukija Waziri wa Ustawi wa Jamii na yeye ana lengo hili. Lengo hili si kwa kuwa ni la mwaka huu limeanza, lengo hili limeshaanzia tangu kitabu cha bajeti kilichopita cha mwaka jana, tayari lengo hili limo la kuanzishwa kwa benki hii ya wanawake.

Lakini ilikuwa angalau mwaka huu watwambie wameshaanzia wapi au wamefikia wapi, lakini la kusikitisha ni kuwa bado kuna uanzishwaji tu uliokuwa hatujui utakapoanzia na wala utakapofikia.

Mhe. Naibu Spika, hii benki ni benki muhimu sana. Wanawake wengi tunahangaika kutokana na kuwa hatuna hii benki ya wanawake. Kuna vikundi vingi ambavyo kuwa ni vikundi vya SACCOS lakini hatimae vinashindwa wapi vikapatie mikopo.

Kuna vikundi vyengine Mhe. Naibu Spika, unakwenda kuchukua kikundi kiliopo kijijini, unakwenda kuiunganisha na benki iliopo Dar Es Salaam, pengine kiongozi yule atakayechaguliwa pale hana uwezo wa kufika kule. Sasa wanashindwa kufuatilia masuala yao katika benki ile. Benki zenyewe ukienda siku zote wafanyakazi wanabadilishwa.

Kwa hivyo Mhe. Naibu Spika, ninamuomba sana Mhe. Waziri akishirikiana na Mhe. Waziri wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi, hebu hili suala waliamue watufanyie, wawafanyie na wanawake wa Zanzibar hili suala la kuanzishwa hii benki ya wanawake ili na wao wapate kujikomboa.

Naomba sana Mhe. Naibu Spika, Mhe. Waziri hili suala alitilie mkazo, kwa sababu ukiangalia hizi SACCOS ziliomo ndani ya hichi kitabu tu, kwa nini ushindwe useme ishindwe kuanzishwa benki hapa Zanzibar. Utaona ni SACCOS nyingi na SACCOS ni kuwa zina akiba, lakini hakuna muelekeo au ni vikundi tu hivi vilivyomo humu, ni vikundi majina tu havina maendeleo na uzalishaji.

Maana vikundi tele viliomo tena vya SACCOS vyengine. Sasa kwa nini tushindwe kuanzisha hii benki. Kwa hivyo Mhe. Waziri hilo uliangalie kwa kina sana kabisa ukishirikiana na Waziri wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi.

Lakini pia nichukue fursa hii kumpongeza Mhe. Rais na wizara yako kwa jumla kuhusu posho la wazee ambalo kuwa mumewaongezea, wazee wa kale wanasema *mtu lake hupewa*. Na hili tunawashukuru kwani na wao ni wazee wetu, tuna majukumu ya kuwaenzi na kuwatunza. Lakini nichukue fursa kukushukuru wewe Mhe. Waziri na watendaji kwa kuanzisha hiki kituo cha mkono kwa mkono. Pia ninaona kitatusaidia kwa kiasi fulani.

Lakini Mhe. Waziri nikienda ukurasa wa 25 kuna Idara ya Maendeleo ya Vijana. Kitabu cha mwaka jana ulitwambia. Ndio yale tunayosema malengo ya mwaka jana na mwaka huu ni yale yale. Sasa kitabu cha mwaka huu nambari 8 kinasema, "Kuendeleza mashirikiano na uhusiano wa taasisi za vijana ndani na nje ya nchi".

Lakini na kile kilichopita kuna ile ile, "Kuendeleza mashirikiano na mahusiano". Tutafikia wapi. Kwa hivyo Mhe. Waziri hebu njoo utwambie bado kuendeleza huku hakujafikia hatua ya mafanikio angalau ukatueleza mara ile tumefanya hivi na mara hii tumefikia hapa. Hilo ni moja.

Jengine Mhe. Naibu Spika, kuna kiambatanisho hiki sijui nambari 8 kuhusu udhalilishaji wa watoto. Katika kitabu cha mwaka jana kulikuwa kesi karibu 74, aina za kesi za udhalilishaji watoto. Kipindi hiki kesi hizi zimepitilia lakini hujatueleza katika kitabu chako hiki cha bajeti kuwa kesi hizi zimepatiwa ufumbuzi namna gani. Ni wangapi waliochukuliwa hatua hawa, hizi kesi zimefikia hatua gani. Kwa sababu tusisikie tu kama kuna hizi kesi lakini hajui hatma yake ni ipi. Kwa hivyo Mhe. Waziri ukija utueleze hizi kesi ambazo umetueleza hapa za kudhalilisha watoto 74 na hizi nyengine zinazokuja, hizi zimefikia wapi?

Lakini jengine Mhe. Naibu Spika, mimi ninataka Mhe. Waziri akija kuna katika lile buku kubwa lile, Afisi Kuu Pemba. Kuna pahali kumeandikwa posho, vikao na kamati. Mwaka uliopita waliingiziwa karibu shilingi milioni 3 lakini mwaka huu hakuna kilichoingizwa. Sasa sijui hiyo Afisi Kuu ya Pemba itafanya vipi shughuli zake, ijapokuwa na mambo mengine lakini posho, vikao na kamati ni kitu muhimu katika idara.

Halafu sehemu nyengine kuna Idara ya Ustawi wa Jamii. Kuna kitu kimeandikwa posho la nguo za heshima. Sasa ninauliza mimi posho la nguo za heshima wanapewa nani? Halafu mwaka jana posho hili halikuwepo lakini mara hii kuna karibuni shilingi laki tisa na kumi kama hivi. Kwa hivyo ukija Mhe. Waziri uje unieleze posho hili la nguo za heshima ni nani wanaopewa na kwa madhumuni gani.

Mhe. Naibu Spika, mimi kwa hayo machache, niseme tu naunga mkono hotuba hii asilimia mia kwa mia.

Mhe. Mussa Ali Hassan: Ahsante Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa nafasi ya kuweza kuchangia Wizara hii ya Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Wanawake na Watoto.

Mhe. Naibu Spika, nafasi ya kwanza nawapa kinamama kwa kuweza kupata nafasi ya kujifungua bure, ambapo suala hili limetokea kihistoria katika Mkoa wangu wa Kusini na Jimbo langu la Koani.

Pia Mhe. Naibu Spika, nampongeza Mhe. Rais kwa kuweza kutoa tamko hili ndani ya jimbo langu la Koani, naweza kusema kwamba alifika jimbo dume ambalo hutoa maamuzi yake bila wasi wasi. Nikifikiria suala la kupewa nafasi kinamama kuweza kutochangia fedha katika uzazi ni jambo la kihistoria, ambapo jambo hili ni adimu sana kutokea katika nchi nyingi duniani, kuweza kupewa uhuru kwamba mwanamke kujifungua asitoe chochote katika hospitali. Kweli jambo hili ni la kujipongeza na la kulitolea mfano katika nchi yetu kwa kusema kwamba limetoka wakati mzuri na wakati wa faraja kwa kuwasaidia kinamama kutotoa mchango wowote katika kuongeza uzazi wa watoto, hasa hapa Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, zaidi ya hayo nachangia Wizara hii inavyohifadhi wazee wetu kwa vizuri sana kwa kufuata nyayo za mzee wetu Marehemu Mzee Abeid Aman Karume, ambapo Waziri hivi sasa analiendeleza vizuri na kwa kweli ni jambo la kupewa mfano, hasa ukienda kuwaangalia wazee wetu wanavyoishi pale Amani, sio wengi waliopata maisha kama yale, hata sisi wenyewe tunaojitunza hatuwezi kujitunza kama wanavyotunzwa wazee hawa.

Mhe. Naibu Spika, hivi sasa ukifika pale Amani ukiwaangalia wazee wanavyopumzika hasa saa hizi, basi utashangaa utafikiri wako katika Victoria ya Marekani. Kwa kweli hili ni jambo la historia katika nchi yetu ambapo ni nchi ambayo inaleta maendeleo na yanaonekana hasa. Sio nchi nyingi duniani ambazo utakuta watu kama hawa wanatunzwa kama hivi wanavyotunzwa hapa Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, hili ni jambo la kuomba kwa Mhe. Waziri sio tuhakikishe kuwa wanatunzwa wazazi wetu hapa Zanzibar, lakini tushukuru au tufurahie zaidi tutakapoona kwamba wazazi hawa wanatunzwa mpaka katika mikoa yetu, zinajengwa nyumba za kuwahifadhi wazee hawa. Ukizingatia hivi sasa sijakuta jimbo hata moja ambalo utakuta majumba ya kulelea wazee. Kwa hivyo, Mhe. Waziri naomba suala hili alipe uzito zaidi katika maendeleo yake ambayo anatunza, ili ahakikishe kwamba wazee katika majimbo nao wanapata majumba haya ya kulelewa, hasa tunapopata malalamiko kwa sisi Wawakilishi na Wabunge kwamba wazazi wengi wanatupwa katika majimbo, kumbe vile Wizara imesahau kuwa inahitajika kupata majengo kama hayo katika majimbo yetu na mikoa.

Mhe. Naibu Spika, nitaunga mkono sana bajeti yake Mhe. Waziri kama nitasikia kwamba mwaka huu wa fedha ameweza kujenga angalau jengo moja katika Mkoa wa Kusini. Mhe. Waziri nakupongeza sana kwa malipo ya wazee wetu yanavyolipwa hivi sasa, hasa kwa kusema kwamba umewaongezea posho. Lakini ilikuwa posho la wazee ni dogo sana ambalo wanapata. Katika jimbo langu mara nyingi husikia wazee wanapata shilingi 5,000 na ndizo wanazopata. Jambo hili nashangaa sana na kama hujafuatilia suala hili basi elewa kwamba suala hili lipo wazee mpaka leo wanapokea shilingi 5,000, ingawa umetangaza umeongeza posho kwa wazee, lakini mpaka sasa wazee wanapokea shilingi 5,000 tu kwa mwezi. Ushahidi ninao na wazee wengi huwafuata Wawakilishi kuwalalamikia matatizo haya.

Kwa hivyo, nakuomba Mhe. Waziri ulihakikishe suala hili unalipitia katika mikoa au unawashirikisha Wawakilishi ili kuhakikisha mambo haya wanafuatilia na kujua ili waweze kulitatua katika majimbo yetu.

Vile vile Mhe. Naibu Spika, nasikia sekta hizi huwa zinalipwa kwa mwezi zinapita kwa masheha, lakini hao masheha wanapopewa hizo pesa wanakaa nazo, mpaka siku anapenda mwenyewe ndio anampelekea yule mzee na akiamua mwezi huu amempa basi atakaa miezi mitatu hampi hiyo shilingi 5,000. Hapo anangojwa Mwakilishi apite ama Mbunge ndio amsaidie mtu yule angalau apate posho, ingawa umetangaza posho limekua kwa mlo wa mara tatu kwa siku. Kwa hivyo, wazee wetu katika majimbo na mikoa hawapati hata mlo wa mara moja.

Mhe. Naibu Spika, zaidi nasisitiza kuhusu sensa ambayo itakuwa tarehe 26/08/2012. Sensa ni jambo zuri sana na ni jambo sahihi katika nchi yoyote duniani, hasa kwa vile sensa ndio inayojumlisha orodha ya watu wote katika nchi. Hii inasaidia kwa sisi wenyewe kuhakikisha serikali yetu inatibu vipi wananchi wake, kujua idadi ambayo ipo katika nchi yake, kuna idadi ya wananchi milioni ngapi au tuna malazi mangapi.

Kwa hivyo, kama mtu hawezi kwenda kujiandikisha ujue amepoteza nafasi kubwa ya kupata matibabu au ya kupata mlo wake wa siku, kwa sababu nchi yetu hivi sasa chakula kingi tunaagiza nje na tunaagiza kwa idadi maalum, sasa unapokuwa wewe hukujiandikisha katika sensa basi ni wazi utadhulumu wenzako ambao wamejiandikisha. Kwa hivyo, tutakuwa tunajua sisi tuko milioni moja na nusu, kumbe vile watu waliojiandikisha ni milioni moja, basi watakuwa wametupotezea nafasi kubwa ya kupata mlo wetu au matibabu ya kuweza kutibiwa kila wakati au kwa siku, utakuwa umepoteza nafasi kubwa ya wananchi sote wa nchi hii ya Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, niingie kwenye matatizo ya watoto kudhalilishwa. Katika kifungu cha 5 kuna kesi 215 za watoto ambao wamedhalilishwa kijinsia, kulawitiwa ama mimba. Lakini utashangaa sana kesi hizi zimetangazwa kwamba watu 215, lakini ukitafuta watu wangapi ambao wameshtakiwa na kuchukuliwa hatua hata ukurasa mmoja sijaona kuwa watu wangapi ambao wako Chuo cha Mafunzo wanatumikia kesi hizi, sasa kesi hizi naona zinatangazwa kama *picnic* tu humu, kwa sababu ni kuwafurahisha watu kwamba tunaaibika kwamba watu wetu zaidi ya mia mbili wamekamatwa au wamedhalilishwa. Lakini ukienda katika sehemu ambazo wanatunzwa hao wahalifu hukuti hata watatu au wawili.

Mhe. Naibu Spika, mimi mwenyewe niko katika Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala ambapo napitia Magereza kila wakati, lakini sijakuta Gereza hata moja ambalo mtu amekamatwa amemlawiti mtu yeyote, ni kesi ngumu sana kukuta mtu amelawitiwa na ni jambo la aibu sana hasa kwa nchi yetu. Lakini ukienda katika Magereza utakuta mtu kakamatwa amekunywa bia amelewa jana kucha, sasa kulewa sio jambo la aibu katika nchi hata katika dini. Mimi ninaloona jambo la aibu ni mtu kusikia amelawitiwa, kwa sababu mtu kama amelawitiwa katika familia yake kwa dini yetu sisi anafukuzwa hasa hapa Unguja, kama una ukoo ndugu yako au mwanao unasikia mwanao amelawiti unamwambia ondoka, unafukuzwa kabisa.

Mhe. Naibu Spika, siku moja nakumbuka Mheshimiwa ametangaza kwamba kisiwa chetu cha pili cha Pemba kuna watu wengi wa aina hii, na hivi sasa mimi ninapokwenda Pemba nikiyatafuta kwa kweli nayaona katika mji pale ambao wengi wamelegealegea, lakini wengi wao utakuta unaambiwa watu hao wengi wameshakimbia wako Unguja. Sasa mimi naona kwamba hawa watu kama hawa ni wazi wadhibitiwe sana, kwa sababu tunajua wanakotokea ni wapi, kisiwa chetu cha Pemba ndicho kinacholeta watu wengi wa aina hii.

Kwa hivyo, wadhibitiwe wasije katika maeneo kuwafundisha wenzao, kwa sababu wao ndio waliokuja kufundisha hili tendo ambalo sio zuri nchini. Kwa hivyo, nashangaa sana Mheshimiwa alifika kulitangaza hili suala, ni bora tu wahakikishe kwamba katika Magereza hawa waliolawiti wako wangapi. Lakini unawakuta walolawitiwa wako njiani, kwa kweli hili suala sio zuri.

Mhe. Naibu Spika, nikiendelea katika ukurasa wa 15, kuhusu kupoteza watoto. Nchi yetu hivi sasa mara nyingi utasikia matangazo ya kupotea watoto. Tunaamini kweli watoto wanapotea, lakini je hawa watoto wanaonekana au hawaonekani, kwa sababu husikii tangazo la pili kwamba mtoto fulani ameonekana. Huku ni kutushtusha nchini, kwamba labda tunasema yale matatizo ya muumiani yamerudi Unguja au vipi, kwa sababu anapopotea mtoto, basi utasikia amepotea, lakini husikii kutangazwa siku ya pili kwamba mtoto yule ameonekana. Lakini kama unakaa naye jirani unamuona yule mtoto anacheza. Jee amepatikana vipi, hujui ni namna gani amepatikana.

Kwa hivyo, Mhe. Waziri ningekuomba ufuatilie hili suala la tangazo, kwamba watoto wanapotangazwa kupotea je, wanapopatikana na kurudi mitaani huwa wanatangazwa tena, kama hawatangazwi basi huyo mtu aliyetangaza hilo suala la kuwa amepoteza mtoto ni afadhali ashtakiwe kwa sababu ametishia amani ya nchi. Kwa sababu kama hukutangaza kuwa mtoto ameonekana ni kwamba nchi yetu unaitia mashaka, kwamba watoto wakipotea wanakwenda wapi, wanaibiwa na kupotea wanachukuliwa wanachinjwa ama wanakwenda kuchukuliwa mtu hana mtoto anaamini japo mtoto wa kuiba awe mtoto wake, hilo ni tishio la nchi. Kwa hivyo, Mhe. Waziri suala hili ulitizame sana kujua watoto wakishapotea je, wanaonekana tena katika mitaa huwa wanatangazwa ama hawatangazwi.

Mhe. Naibu Spika, tukizingatia mambo ya upotevu ni jambo gumu sana, hasa wengine utakuta ni watoto wanaotangazwa kuwa wamepotea ni wale wasiokuwa na akili na wanaoneshwa katika televisheni, kwamba mtoto hana akili amepotea. Lakini sasa hupati tangazo kwa yule mtoto mwenye akili ameonekana kwa mazingira gani, ameonekana yuko hai au ameonekana amevutwa na maji kwenye mitaro alikuwa ametupwa baharini, ama ameonekana kivipi. Hiyo ingesaidia kuondosha matishio makubwa ambayo watu wanatishika.

Mhe. Naibu Spika, hivi sasa watoto wengi ikifika saa 12 wanafungiwa milango, kwa sababu inaonekana nje kuna vibaka ambao wanaiba watoto ama vipi. Kumbe vile mtoto amekwenda kutembea kwa jirani baada ya masaa fulani ameonekana, lakini tangazo la kuwa ameonekana hakuna. Kwa hivyo, tunaomba Mhe. Waziri suala hili ulitilie nguvu kuhusu watoto wakati wanapopotea ni lazima watangazwe, na wakati wanapoonekanwa pia watangazwe.

Mhe. Naibu Spika, nikirudia tena suala la wazazi wetu wanaotunzwa na serikali. Kwa hivi sasa katika majibu tuna maskitiko makubwa sana kuona kila jimbo angalau tutajiwe Mhe. Waziri atuhakikishie katika Jimbo la Koani kuna

wazee wangapi wanawatunza, katika Jimbo la Kikwajuni kuna watu wangapi au kwa mkoa mmoja kuna watu wangapi. Lakini ni vigumu sana tunaposikia wazee wanatunzwa, lakini tuna wasi wasi kuwa wazee hao ni wa mjini peke yake. Kwa sababu sijasikia mzee wa Makunduchi kuwa yuko pale kwenye zile nyumba anatunzwa hatujui idadi yao.

Sisi tunavyoamini labda wazee wengi wanaotunzwa ni kutoka Mji Mkongwe hadi Kwamtipura ndio tunaamini hao wazee wa mjini tu ndio wanaohitaji kutunzwa kumbe vile na mikoa yetu wazee wetu wanahitaji kutunzwa. Kwa hivyo, tuoneshwe orodha hasa ya kila mkoa ni wazee wangapi wako pale Amani wanatunzwa na wanatunzwa na serikali, ama tujue anatakiwa mzee awe na sifa gani ndio anachukuliwa kutunzwa na serikali. Kwa sababu kama hatujui hivyo, basi sisi wengine tunaweza kusema kwamba ni ubaguzi wa jinsia kwamba wazee wa mjini ndio wanaotunzwa, wazee wa shamba hawatunzwi kabisa.

Nafikiri Mhe. Naibu Spika, kwa hayo ni mchango wangu mzuri, wa muda mfupi, lakini unaoeleweka nini kilichokusudiwa. Vile vile naunga mkono hoja kwa asilimia mia kwa mia pamoja na wananchi wangu wa Jimbo la Koani, ahsante sana. *(Makofi).*

Mhe. Asha Abdu Haji: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, jioni hii kunipa fursa. Kwanza kabisa napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutupa afya njema. Pili napenda kulishukuru Baraza hili ambalo leo lilikuwa ni Baraza la historia. Mwenyekiti ni mwanamke, mshika rungu mwanamke na makatibu wetu wanawake, Waziri wetu mwanamke na katibu wa wizara ni mwanamke. Mhe. Naibu Spika, naipongeza sana wizara hii kweli ni Wizara ya wanawake na Watoto. *(Makofi).*

Vile vile nampongeza Mhe. Rais kwa kuitoa kauli yake ya kuweka huduma ya bure kwa mama wajawazito ambao wanazaa kwa operesheni. Namshukuru sana na nampongeza Rais wetu kwa kulisikia tatizo la akinamama hawa. Pili nampongeza Mhe. Waziri kwa kutembelea vikundi vyetu vya Unguja na Pemba kwa vijana na wanawake. Nampongeza sana Mhe. Waziri kwa vile vikundi hivi sio kuwa viko katika wizara yake, lakini yeye kwa imani yake na kwamba yuko katika wanawake, watoto na vijana anajishughulisha sana na vikundi hivi ili kuondoa tatizo kwa wanawake.

Mhe. Naibu Spika, nakipongeza kituo cha kulelea watoto Mazizini na kituo cha kuwalea wazee Welezo. Kwa kweli watu hawa wenye kutoa huduma hizi ni watu ambao inafaa wapewe pongezi kubwa sana, ni watu ambao wanapata shida sana kwa watoto, watoto wanakuja pale ni wachanga kabisa, wengine walemavu na wengine hali inakuwa mbaya, na watoa huduma ile wanafanyakazi kwa moyo mmoja wala hawana kinyongo, wala hawahisi kwamba huyu sio mtoto wangu na huyu sio wa jamaa yangu, wanakaa nao vizuri sana. Kwa hivyo, inafaa katika wizara hii iongezwe posho kwa wahudumu wale.

Vile vile Mhe. Naibu Spika, nawapongeza tena wahudumu ambao wanakaa na wazee ambao hawajiwezi kabisa. Ni wazee ambao hawajiwezi wengine hawaoni, wengine kwenda hawawezi, hii ni wizara yangu nimeona mwenyewe namna wazee wanavyokaa, huwezi kukubali kwamba hawa ni watu ambao hawa wazee sio jamaa zao na wanawahudumia. Utafika pale wewe mzee wako unaishi naye nyumbani kwako basi anakushinda unafika pale anatoa harufu, lakini tumekwenda pale hakuna harufu ya aina yoyote. Yuko mzee haoni hata kidogo, basi tumeshangaa sisi, tumefika pale tunashangaa. Hee, hawa wazee wanakaa hivi na hawa wahudumu wanakaa hivi huwezi kukubali. Kwa hivyo, naipongeza sana na ningeiomba wizara hii katika sehemu ile iwaongezee posho na iwaone sana.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli sina mengi, mengi yameshazungumzwa na wenzangu. Kwa leo naishia hapa naunga mkono hoja, ahsante.

Mhe. Naibu Spika: Ahsanteni sana Waheshimiwa Wajumbe kwa michango yenu na naomba kutoa taarifa kwamba tuna wachangiaji 12. Kwa hivyo, tunaomba siku ya Jumatatu tufike mapema tuichangie na baadae tuimalize hotuba ya Mhe. Waziri wetu.

Baada ya maelezo hayo naakhirisha kikao chetu hiki hadi Jumatatu tarehe 09/07/2012 saa 3:00 za asubuhi.

(Saa 1:45 Baraza liliakhirishwa hadi
tarehe 09/07/2012 saa 3:00 asubuhi)